

TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

**KIMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD
JAWAD MUGHNIYYA**

KIMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA

KIMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED

KUPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU

UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI

**KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU, MWINGI WA REHEMA,
MWENYE KUREHEMU.**

Kitabu hiki kilichoko mikononi mwako hivi sasa ni juhud ya miaka mingi sana ya watu walijitolea kuona kazi hii imefanikiwa bila ya kumsahau Marhum Abu Muhammad wa London.

Kama lilivyo jina la Tafsiri yenye ndivyo ilivyo Tafsiri yenye ambayo mwanachuoni huyu mahiri kabisa aliyeifafanua ni mtu aliyebolea katika fani zote ambazo mfasiri (Mfafanuzi) anatakiwa awe nazo. Sheikh Muhammad Jawad Mughniyya ameonesha cheche zake katika vitabu vingi alivyoviandika katika maudhui mbali mbalimbali na hivyo kujipatia wasomaji wengi sana.

Msomi huyu, mwenye fikra huru na anayetetea kile anachokiamini, ni mtu mwenye mawazo mapana na kuyaangalia mambo kwa undani sana, kipaumbele chake ni katika maslahi ya umma huu na amejaribu sana kwenda na wakati.

Sifa kubwa pekee ya mwanachuoni huyu ni kuwa yeye hakujihusisha sana na kung'ang'ania madhehebu fulani tu, labda hii yatokana na wadhifa wake wa ukadhi aliokuwa nao katika nchi ya Lebanon ambayo ina madhehebu mengi, ambapo sula la madhehebu ni nyeti nchini humo, hata hivyo yeye aliweza kuamua matatizo ya watu kwenye ofisi yake kulingana na madhehebu yao pale walipomwendea, hiyo ilimsaidia sana hata kuweza kutoa kitabu kitwacho Al-Fiqh a'laa madhaahabil-khamsah (Fikhi ya madhehebu matano) yaani ya Hanafi, Maaliki, Shafi, Hambali na Shia (ambacho twataraji kitatoka hivi karibuni Inshaallah).

Jambo lililotupa msukumo wa kukifasiri kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili ni zile faida nydingi atakazozipata msomaji na kujuu mambo mengi na ya ajabu yaliyo mapya kwake ambayo si rahisi kuyapata kwa wafasiri wengine.

Msomaji atapata faida katika fani za Sayansi, Siasa, Historia, Mashairi, visa vizuri, na Saikolojia miongoni mwa mengine; ndiyo maana msomaji atashangaa kidogo anapoisoma Tafsiri hii atakapoona mwandishi amewataja na kuwanukuu watu kama kina Mfalme Edward, wanasyansi kama kina Enstein, Charlie Champlin (Mchekeshaji maarufu), na wengineo, hali inayoifanya tafsiri hii kuwa ni ya kipekee kabisa.

Mtindo alioutumia mwandishi ni sahali uliokusudiwa watu wa tabaka mbalimbali, wanavyuoni na watu wa kawaida.

Nia yetu ni kukigawanya kitabu hiki bure lakini tumelazimika kukiiza kwa bei nafuu ili kurudisha gharama za uchapishaji.

Mwisho: Shukrani kubwa iwaendee bila ya kuwataja watu waliojitolea usiku na mchana, jopo la wafasiri, wahariri, wachapaji, waliotupa moyo na kutoa maoni yao na walioisimamia ili kuhakikisha kwamba kitabu kimemfikia msomaji.

MAKOSA YA CHAPA

Sikumbuki kama nimewahi kusoma kitabu kilichotoka kupigwa chapa, cha zamani au cha sasa, bila ya kukuta makosa ya chapa. Nafikiri sitasoma kitabu kisichokuwa hivyo. Nimejaribu sana kuliepuka hilo katika tungo zangu, lakini sikufanikiwa.

Nilikuwa sifirkii kama ninaweza kuona makosa haya katika maandishi ya msahafu mtukufu, kama yale yaliyo katika baadhi ya chapa; kwa mfano neno yabswatu kwa swad, badala ya yabsutu kwa sin, na katika chapa ya Tafsir Arrazi ya Misr ya mwaka 1935, Sura ya (2:146). Imeandikwa La Ya'alamuun, (hawajui) badala ya Ya'alamuun (wanajua). Mfano wa makosa haya hausameheki.

Katika Tafsir Al-Manar, chapa ya Pili, sura (5:212), imeandikwa Fawqahum ila yawmil qiyama badala ya Fawqahum yawamal qiyama. Hatuwezi kusema kosa hili ni kubwa zaidi kuliko lile.

Lakini mkosaji atatuletea udhuru kwa msemo mashuhuri huko kwetu jabal amail 'Makosa ya chapa.' Katika Tafsiri Majmau chapa ya Urfan, Sura (46:15), imeandikwa: Hatta idha balagha arbai' na sanah badala ya: Hattaidha balagha ashuddahu arbai' na sanah"

Kusema hivi sio kama ninajitetea kutokana na makosa ya chapa atakayoyakuta msomaji katika kitabu hiki, ijapokuwa naomba msamaha kama litatokea hili, lakini makusudio yangu hasa ni kumwambia yule atakayefungua macho yake kwenye makosa ya matamko na kuufungia macho uzuri wa maana. Vilevile ninamwambia yule ambaye siku moja aliniambia: "Vitabu vyako vimejaa makosa ya chapa, kama kwamba hakuna kitu chochote katika vitabu hivyo isipokuwa makosa ya chapa tu. Wote hao ninawaambia: Mungu awasamehe na aniongoze mimi na nyinyi.

Vyovyyote iwavyo, mimi ninaomba msamaha kutokana na makosa ya kifira na ya chapa. Anasema Amirul Muminiin ^(a.s): "**Watu wote ni wapungufu wenye kuchanganyikiwa, isipokuwa yule aliyehifadhiwa na Mwenyezi Mungu.**" Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye mwenye jukumu la kunikubalia.

TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

﴿لَا يُحِبُّ اللَّهُ الْجُهْرَ بِالسُّوءِ مِنَ الْقَوْلِ إِلَّا مَنْ ظَلِمَ وَكَانَ اللَّهُ سَيِّئًا عَلَيْهِ﴾

148. Hapendi Mwenyezi Mungu maneno ya kutangaza uovu ila kwa mwenye kudhulumiwa; na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kusikia, Mjuzi.

﴿إِنْ تُبْدُوا حَيْرًا أَوْ تُخْفُوا أَوْ تَعْفُوا عَنْ سُوءٍ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفُوًّا قَدِيرًا﴾

149. Mkidhihirisha heri au mkiificha au mkisamehe uovu, basi hakika Mwenyezi Mungu ndiye mwingi wa kusamehe, Muweza.

DHALIMU HAHESHIMIWI

Aya 148 - 149

MAANA

Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kuharamisha kusengenya amesema:

﴿وَلَا يَغْتَبْ بَعْضُكُمْ بَعْضًا﴾

"Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine" (49:12)

Na katika aliyojasema kuhusu kuharimisha dhulma ni: "Laana ya Mwenyezi Mungu iwapate madhalimu." (7:44)

Na amesema katika Aya tulio nayo: Hapendi Mwenyezi Mungu maneno ya kutangaza uovu ila kwa mwenye kudhulumiwa.

Tukiunganisha Aya hii na Aya ya kusengenya, maana yanakuwa ni mtu asitaje aibu na maovu ya mwingine, ila yule aliyedhulumiwa, anaweza kutangaza na kudhihirsha uovu kwa kudhulumiwa.

Maana ya dhulma ni maarufu. Ama kusengenya kuliko haramu, mafakihi wamekueleza kuwa ni kumtaja mwingine kwa jambo analolichukia akiwa hayuko; kama vile kumvunja heshima yake na watu wamcheke; ni sawa hilo awe analo au ni uongo na uzushi. Wameuondoa uharamu wa kumsengenya dhalimu na mwenye kujidhulumu, kwa kuudhihirisha ule uovu wake na kutojali kwake yanayosemwa na anayoambwa.

Katika Kitabu Makasib cha Sheikh Ansari, imesemwa kuwa sehemu zinazoondolewa hazina idadi; Kwa sababu kusengenya kunakuwa haramu pale tu ikiwa kutangaza huko hakuna masilahi yenyenuguu, Vinginevyo, basi itakuwa wajibu kutangaza na kueneza kwa kuangalia masilahi yenyenuguu zaidi, kama ilivyo katika kila maasi ya haki za Mwenyezi Mungu na haki za binadamu.

Kwa hali hiyo basi inajuzu kisharia migomo na maandamano dhidi ya serikali dhalimu, bali itakuwa ni wajibu ikiwa hakuna njia nyingine ya kuondoa dhulma isiyokuwa hiyo, kwa sharti ya kuwa isilet ghasia na madhara kwa wengine. Kwa sababu Mwenyezi Mungu hatiiwi pale anapoasiwa. Na Uislamu unachunga hadhi na heshima ya binadamu mpaka aingilie heshima ya mwenzake. Hapo heshima inaondoka na kuwa halali kuvunjwa na kudhalilishwa.

Ilivyo hasa ni kwamba dhuluma haihusiki tu na serikali dhalimu na vibaraka wao. Mtu yeote aliyemchokoza mwengine kwa kauli au kitendo au akamnyima haki yake au akaichelewesha basi yeye ni dhalimu. Mtume wa Mwenyezi Mungu anasema: "Kubabaisha deni ni dhulma ". Katika Hadith nyingine anasema: "Mbabaishaji deni ni halali kumvunja heshiTafsir ma". Mbabaishaji deni hapa ni yule asiyelipa deni na huku ana uwezo wa kuilipa.

Wamepokea Ahlul - Bait kutokana na babu yao amesema: "**Mwenye kuishi na watu asiwadhulumu, akizungumza nao hawawadanganyi na akiwaahidi hawakhalifu, basi huyo ni katika ambao umekamilika murua wake, ni wajibu kumfanya ndugu na ni haramu kumsengenya mwongo na mvunja ahadi hana heshima.**"

Hivi ndivyo ulivyo Uislamu unachunga haki ya mtu maadamu naye anachunga haki za kibinadamu zilizoko kwa wenzake na kwake. Akipuza basi naye atastahili kupuuzwa na kudharauliwa.

Mkidhirishia kheri au mkificha.

Hili ni himizo la kufanya kheri kwa siri au dhahiri.

Au mkisamehe uovu, basi hakika Mwenyezi Mungu ndiye mwingi wa kusamehe, muweza.

Ni kweli kuwa ni vizuri kusamehe maovu, lakini ni pale utakapokuwa msamaha ni heri kwake wala hauna madhara kwa jamii. Ama ikiwa ni njia ya kumhimiza muovu aendelee na uovu na kueneza ufisadi, basi kumwadhibu ndiko kunakotakikana. Vinginevyo hakutakuwa na nidhamu na maovu yataenea. Mwenyezi Mungu anasema:

"**Mna uhai katika kulipiza kisasi enyi wenye akili ili msalimike**" (2:179) na amesema tena: "**Na piganeni nao mpaka kusiwe na fitna**" (2:193)

﴿إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُقْرِبُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَيَقُولُونَ نُؤْمِنُ بِبَعْضٍ وَنَكْفُرُ بِبَعْضٍ وَيُرِيدُونَ أَنْ يَتَخَذُوا بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا﴾

150. Hakika ambao humkataa Mwenyezi Mungu na Mitume wake na wanataka kufarikisha baina ya Mwenyezi Mungu na mitume wake na wakasema: tumeamini baadhi na kukataa baadhi; na wakataka kushika njia iliyo katikati ya haya.

﴿أُولَئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ حَقًّا وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُهِينًا﴾

151. Hao ndio makafiri kweli kweli na tumewaandalia makafiri adhabu idhalilishayo.

﴿وَالَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَلَمْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ أَحَدٍ مِنْهُمْ أُولَئِكَ سَوْفَ يُؤْتَيْهِمْ أُجُورَهُمْ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا﴾

152. Na wale ambao wamemwamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake wala wasifarikishe baina ya yeote katika wao, hao atawapa ujira wao. Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghfira, mwenye kurehemu.

WANAAMINI BAADHI NA KUKANUSHA BAADHI

Aya 150 - 152

MAANA

Hakika ambao humkataa Mwenyezi Mungu na Mitume wake na wanataka kufarikisha baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume wake na wakasema: **Tumeamini baadhi na kukataa baadhi.**

Mayahudi walimwamini Musa na Taurat, wakamkana Isa na Muhammad. Wakristo walimwamini Isa na Injil wakamkana Muhammad na Qur'an. Na Waislamu wamewaamini wote.

Kwa sababu, imani katika mtazamo wa kiislamu ni moja haigawanyiki wala hakuna njia ya kuigawanya. Imani hiyo ni kumwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na Malaika wake na Mitume wake wote na vitabu vyake. Mwenye Kukikana kimojawapo basi amekana vyote.

Na wakataka kushika njia iliyo katikati ya haya.

Yaani baina ya ukafiri na imani, ingawaje hakuna njia baina yake; hata mwenye kutia shaka tu anahisabiwa kuwa kafiri. Muulizaji akiuliza kuhusu hukumu ya asiyejua utume wa mmojawapo wa Mitume, basi tumeyafafanua hayo katika kufasiri (3:115) kifungu "Hukumu ya mwenye kuacha Uislamu". Hao ndio makafiri kweli kweli Hata kama wataamini baadhi, kwa sababu imani ni kwa vyote haigawanyiki. Na wale ambao wamemwamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake wala wasifarikishe baina ya yejote katika wao, hao atawapa ujira wao.

Hawa ni Waislamu, wafuasi wa Muhammad bin Abdullah, ambaye amewaamrisha kuamini Mitume yote na akasema Mitume yote ni ndugu, dini yao ni moja na umma zao ni mbali mbali. Umetangulia ufanuzi katika kufasiri Aya 136 ya Sura hii na (2:285).

﴿يَسْأَلُ أَهْلُ الْكِتَابِ أَنْ تُرِّئَنِي هُمْ كِتَابًا مِنَ السَّمَاءِ فَقَدْ سَأَلُوا مُوسَى أَكْبَرَ مِنْ ذَلِكَ فَقَالُوا أَرِنَا اللَّهَ بَعْدَهُ فَأَخَذَنَاهُ الصَّاعِقَةَ بِطُلْمٍ هُمْ ثُمَّ أَخْذَدُوا الْعِجْلَ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمُ الْبَيِّنَاتُ فَعَوَّنَتَا عَنْ ذَلِكَ وَآتَيْنَا مُوسَى سُلْطَانًا مُّبِينًا﴾

153. Watu wa Kitabu wanakutaka uwateremshie Kitabu kutoka mbinguni. Hakika walimtaka Musa makubwa kuliko hayo. Walisema: Tuonyeshe Mwenyezi Mungu waziwazi. Wakapigwa na radi kwa sababu ya dhulma yao. Kisha wakamfanya ndama (kuwa Mungu) baada ya kuwafikia hoja. Na tukawasamehe hayo Na tukampa Musa hoja zilizo wazi.

﴿وَرَفَعْنَا فَوْقَهُمُ الْطُورَ بِمِثَاقِهِمْ وَقُلْنَا لَهُمْ لَا تَعْدُوا فِي السَّبِّ وَأَخْدَنَا مِنْهُمْ مِثَاقًا غَلِيلًا﴾

154. Na Tukanyanya Tur juu yao kwa ahadi yao. Na tukawaambia: Ingilieni mlangoni kwa unyenyekevu. Na tukawaambia msipetuke mipaka ya Sabato. Na tukachukua kwao ahadi madhubuti.

WALISEMA TUONYESHE MWENYEZI MUNGU WAZIWAZI

Aya 153-154

LUGHA

Neno Taadu lina maana ya kupetuka mpaka. Makusudio yake hapa ni kutofanya kazi siku ya Jumamosi. Na limesomwa Tauddu kwa maana ya kufanya uadui.

MAANA

Watu wa Kitabu wanakutaka uwateremshie Kitabu kutoka mbinguni.

Makusudio ya watu wa Kitabu hapa ni Mayahudi wa Madina waliokuwa na msimamo wa kiadui na ukaidi kwa Mtume na wakamfanyia vitimbi vy a kuendelea. Mionganoni mwa ukaidi na balaa zao ni yale aliyoyaashiria Mwenyezi Mungu (swt) katika Aya hii - kutaka wateremshiwe Kitabu kutoka mbinguni kitakachomshuhudia na kwamba wakione wao na macho yao.

Kwa dhahiri ni kwamba walisema hivyo kwa njia ya kusumbua na ukaidi na wala sio kutaka hoja na ukweli. Kwa sababu miujiza yake iliyotangulia inatosha kumkinaisha mwenye kuitafuta haki kwa njia ya haki.

Mwenyezi Mungu akamjibia Mtume wake kwa kusema: **Hakika walimtaka Musa makubwa kuliko hayo.**

Yaani hakuna geni wala ajabu, ewe Muhammad, kukutaka uwateremshie Kitabu kutoka mbinguni, kwani walikwishamuuliza Musa makubwa kuliko hayo, walimtaka awaonyeshe Mwenyezi Mungu hasa. Walisema:

Tuonyeshe Mwenyezi Mungu waziwazi. Wakapigwa na radi kwa sababu ya dhulma yao. Kisha wakamfanya ndama (kuwa Mungu) baada ya kuwafikia hoja.

Imetangulia tafsiri ya matakwa yao haya na kumfanya kwao ndama kuwa Mungu katika (2:54-57) na pia tukazungumzia kauli za madhehebu kuhusu kuonekana Mwenyezi Mungu.

Inajulikana wazi kwamba waliotaka kumwona Mungu waziwazi na kumfanya ndama kuwa Mungu ni Mayahudi wa kwanza na wala sio wa Madina. Lakini hawa waliridhia na kuamini kila walilofanya mababu zao. Kwa hiyo ikafaa kunasibishiwa wao.

Na tukampa Musa hoja zilizo wazi.

Lakini Mayahudi wanadharau kila kitu wala hawalipi umuhimu jambo lolote ila likiwa lina moja kati ya mawili: Ama manufaa au nguvu. Kwa ajili hii ndipo Mwenyezi Mungu akawahofisha kwa jabali ambalo ameliashiria kwa kauli yake: **Tukanyanya Tur juu yao kwa ahadi yao.**

Tur ni jina la mlima ambaao Musa alizungumza na Mola wake. Mwenyezi Mungu anasema: "**Na kwa Tur sininin (95:2)**" Sinin na Sinai ni majina ya mahali palipo na mlima huo. Mwenyezi Mungu aliwaamrisha wana wa Israil kuptitia kwa Musa waitumie Taurat wakakataa ndipo Mwenyezi Mungu akawainulia mlima juu yao mpaka wakakubali.

Kauli ya Mwenyezi Mungu; **kwa ahadi yao**, makusudio yake ni kuvunja ahadi yao juu yao wenyewe ya kulazimiana na dini kisha wakaacha. **Lau si mlima wasingelirudia.**

Kwa hiyo hapana ajabu kwa Israil kuasi nidhamu za kimataifa na kukataa maazimio ya Umoja wa mataifa na Baraza la usalama. Wamevunja ahadi na makubaliano mara kadhaa. Lau si kuwa na hofu wasingelitulia. Hapana ajabu wala geni! Hilo linalingana na historia ya wakale wao ambaao Mwenyezi Mungu aliwainulia mlima ili watekeleze ahadi.

Na tukawaambia: Ingieni mlangoni kwa unyenyekevu. Imepita tafsir yake katika (2:58)

Na tukawaambia msipetuke mipaka ya Sabato. Vilevile imepita tafsir yake katika (2:65)

﴿فِيمَا نَقْضِهِمْ مِّيَتَاقُهُمْ وَكُفَّرُهُمْ بِآيَاتِ اللَّهِ وَقَتْلُهُمُ الْأَنْبِيَاءَ بِغَيْرِ حَقٍّ وَقَوْلُهُمْ قُلُوبُنَا غُلْفٌ
بَلْ طَبَعَ اللَّهُ عَلَيْهَا بِكُفْرِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا﴾

155. Basi (tuliwalaani) kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao, na kuzikufuru kwao ishara za Mwenyezi Mungu, na kuua kwao manabii pasi na haki, na kusema kwao nyoyo zetu zimefumbwa; bali Mwenyezi Mungu amezipiga muhuri kwa kufuru yao. Basi hawataamini ila wachache tu.

﴿وَبِكُفْرِهِمْ وَقَوْلُهُمْ عَلَى مَرِيمَ بُهْتَانًا عَظِيمًا﴾

156. Na kwa kufuru yao na kumsingizia kwao Maryam uwongo mkubwa.

﴿وَقَوْلُهُمْ إِنَّا قَاتَلْنَا الْمَسِيحَ عِيسَى ابْنَ مَرِيمَ رَسُولَ اللَّهِ وَمَا قَاتَلُوهُ وَمَا حَلَّ بُوْهُ وَلَكِنْ شَيْءٌ
لَّهُمْ وَإِنَّ الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِيهِ لَفِي شَيْءٍ مَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا اتِّبَاعُ الظَّنِّ وَمَا قَاتَلُوهُ يَقِينًا﴾

157. Na kwa kusema kwao: sisi tumemuua Masih Isa, mwana wa Maryam Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na hawakumuua wala hawakumsulubu, lakini alifananishwa kwao. Na hakika wale waliohitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo; hawana ujuzi ila kufuata dhana tu. Wala hawakumuua kwa yakini.

﴿بَلْ رَّفِعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا﴾

158. Bali Mwenyezi Mungu alimwinua kwake, na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mwenye hekima.

﴿وَإِنْ مَنْ أَهْلُ الْكِتَابِ إِلَّا لَيُؤْمِنَّ بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكُونُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا﴾

159. Na hakuna katika watu wa Kitabu ila humwamini yeze kabla ya kufa kwake, na Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.

KUVUNJA KWAO AHADI

Aya 155-159

MAANA

Basi (tuliwalaani) kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi yao.

Yaani tuliwalaani kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi waliyojilazimisha nayo na kuihakikisha katika nafsi zao, ambayo ni kuamini na kuyatumia mafunzo aliyokuja nayo Musa ^(a.s). Kisha wakageuza na kubadilisha, wakaharamisha aliyoyahalalisha Mwenyezi Mungu na wakahalalisha aliyoyaharamisha.

Na kuzikufuru kwao ishara za Mwenyezi Mungu

Yaani kuzikataa hoja na dalili juu ya utume wa Isa na Muhammad (s.a.w.w)

Na kuwaa kwao Manabii pasi na haki

Kama vile Zakariya na Yahya, baada ya kuweko hoja ya utume wao.

Na kusema kwao nyoyo zetu zimefumbwa

Yaani zimezibwa haziingii chochote kutokana na wito wa Muhammad.

Waliyasema haya kwa Mtume Mtukufu kwa kukatisha tamaa kuwa wataamini utume wake na kuitikia mwito wake.

Bali Mwenyezi Mungu amezipiga muhuri kwa kufuru yao.

Ni jumla iliyoingia kati iliyokuja kujibu kauli yao kuwa nyoyo zetu zimefumbwa. Maana yake ni kuwa, nyoyo zenu hazikufumbika kimaumbile,

isipokuwa kwa sababu ya kumkufuru kwenu Muhammad na kuboea kwenu kwenye upotofu ndiko kulikowafanya wagumu kama mawe na wagumu zaidi kuliko mawe.

Baada ya nyoyo zao kufikilia kiwango cha kutofunguka na haki kwa hali yoyote, wamekuwa kama wameumbwa na Mwenyezi Mungu bila ya nyoyo. Kwa kuzingatia hivi ndipo ikafaa kuambiwa kuwa Mwenyezi Mungu amezipiga muhuri nyoyo zao. Tazama tafsiri (2:7)

Basi hawataamini ila wachache tu.

Kama vile Abdallah bin Salaam, Thaalab bin Saaya, Asad bin Ubaidullah na wengineo.

Na kwa kufuru yao na kumsingizia kwao Maryam uwongo mkubwa.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekariri mara tatu kunasibisha ukafiri kwa Mayahudi:

Kwanza: kwa mnasaba wa kutaja ukanusho wao wa ishara za Mwenyezi Mungu na kuua Mitume.

Pili: Kwa mnasaba wa kusema kwao "Nyoyo zetu zimefumbwa."

Tatu: Kauli yao juu ya Maryam ambayo hawaisemi ila Wayahudi walioingizwa kwenye ukiristo na Amerika, na kuwapa silaha ili waingilie Baitul Maqdis na wavunjie heshima nembo za dini amabazo wanazitukuzwa Wakristo na Waislamu, hasa makanisa na makaburi ya Wakristo¹.

1Ninaadikia maneno haya leo hii tarehe 28.4.1968 na Israil imepanga kufanya maonyesho makubwa ya kijeshi mnamo tarehe, 2.5.1968 kwenye mji wa Qudus; ingawaje Baraza la usalama limepitisha kwa kauli moja kutofanyika maonyesho hayo.

Na kwa kusema kwao: Sisi tumemua Masih Isa, mwana wa Maryam, Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Wamemsifu kwa jina la Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa kumchezea tu.

Na hawakumuua wala hawakumsulubu, lakini alifananishwa.

Mayahudi walipong'ang'ania kumua Bwana Masih (Isa), Mwenyezi Mungu alimfananisha mmoja wa wenyе makosa anayestahiki kuuliwa. Inasemekana kuwa mkosaji huyo alikuwa ni Yuda ambaye aliongoza shambulio dhidi ya Bwana Masih. Mayahudi wakamkamata wakamwadhibu na kumsulubu kwa kufikiria kuwa ni Bwana Masih. Baada ya kumsulubu wakawa hamwonı mwenzao (Yuda) wakaduwaa na kusema ikiwa aliyesulubiwa ni Masih, basi yuko wapi mwenzetu? Na kama mwenzetu ndiye aliyesulubiwa, yuwapi Masih?

Na hakika wale waliokhitilifiana katika haya, wamo katika shaka nayo. Walihitilafiana Mayahudi na Wakristo kuhusu Bwana Masih ^(a.s) wakawa na misimamo ya kupingana. Mayahudi wakasema ni mwanaaharamu; na Wakristo wakasema ni mwana wa Mungu.

Vile vile Mayahudi walisema: Tumemslubu na kumzika ardhini bila ya kufufuka; na Wakristo wakasema:

Yeye alisulubiwa na kuzikwa kisha akafufuka baada ya siki tatu.

1 Ninaadikia maneno haya leo hii tarehe 28.4.1968 na Israil imepanga kufanya maonyesho makubwa ya kijeshi mnamo tarehe, 2.5.1968 kwenye mji wa Qudus; ingawaje Baraza la usalama limepitisha kwa kauli moja kutofanyika maonyesho hayo.

Mwenyezi Mungu akawajibu wote hawa kwa kusema: Hawana ujuzi wowote ila kufuata dhana tu. Na dhana haitoshelezeki haki kabisa. Na haki ya yakini isiyo na shaka ni ile aliyotuelezea Mwenyezi Mungu katika kauli yake:

Wala hawakumuua kwa yakini, bali Mwenyezi Mungu alimwinua kwake.

Hii ndiyo hakika, sio kuuwa wala kusulubu. Yamekuja maswali kuhusu hilo: Vipi alivyoinuliwa? Lini? Kabla ya kusulubiwa yule aliyefananishwa au baada.? Je, kulikuwa ni kuinuliwa kwa roho au kwa roho na mwili? Na je, aliinuliwa mbinguni siku ya pili, ya tatu au nyingineyo? Na kwamba je, huko aliko anafanya nini? Na je, atashuka duniani muda mfupi kabla ya Kiyama? Na maswali mengi mengine ambayo wasimulizi wa visa wamejibu kwa majibu yanayofanana na vigano.

Qur'an Tukufu haikuonesha chochote katika hayo si kwa karibu wala kwa mbali. Lililofahamishwa na Aya ni kwamba Bwana Masih hakuuwawa wala hawakusulubiwa na kwamba Mwenyezi Mungu alimnyanyua kwake na kwamba aliyesulubiwa na kuuawa ni mtu mwengine aliyedhaniwa kuwa ni Masih.

Hakuna katika Qur'an zaidi ya hayo na sisi hatuwezi kutoka nje katika mfano wa maudhui kama haya ila kwa Hadith Mutawatir. Bali hatutilii muhimu maswali haya na majibu yake, madamu hatutaulizwa kesho wala kukalifishwa nayo. Tumetangulia kueleza yaliyosemwa kuhusu Masih katika kufasiri (3:58) kifungu (tofauti kuhusu Isa).

Hebu tuwachekeshe kidogo kwa kunukuu kigano hiki kilichotokana na baadhi ya wafasiri: Hakika Mwenyezi Mungu alimwinua Isa kwake akamvisha vazi la nuru akamwotesha mbawa, akamfanya asile na asinywe, akamchaganya na Malaika akawa anaruka nao pembeni mwa Arsh na akamfanya na tabia mbili ya kibinadamu na Malaika.

Na hakuna katika watu wa Kitabu ila humwamini yeye kabla ya kufa kwake.

Yaani hakuna yeyote katika watu wa Kitabu ila humwamini Isa kabla ya kufa mtu huyo wa kitabu. Makusudio ya watu wa Kitabu ni Mayahudi na Wakristo. Imeelezwa katika baadhi ya Hadith kwamba kila mtu anapokuwa katika maumivu ya kukata roho.

humfunukia haki ya aliyokuwa akiyaitakidi duniani. Aya hii inashuhudia riwaya hizo, ambapo dhahiri yake inafahamishia kuwa kila mtu wa Kitabu awe Myahudi au Mkristo hana budi kumwamini Isa kwa imani sahihi baada ya maumivu ya kukata roho.

Myahudi ambaye alikuwa akisema kwamba Isa ni mchawi na mtoto wa zina, atabadilika na kuamini kwamba yeye ni Mtume aliyetumwa, na kwamba mama yake ni mkweli. Na Mkristo aliyeokuwa akisema kwamba yeye ni mwana wa Mwenyezi Mungu na ni watatu katika utatu ataamini kuwa ni mja mionganoni mwa waja wema.

Hili si muhali katika mtazamo wa akili na limeelezewa na wahyi na kila lililoelezewa na wahyi na lisikanushwe na akili ni wajibu kusadikiwa na kila mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Ama asiyeamini ila yanaonekana kwa darubini hataamini kabisa. Basi na asimwamini yule atakayemwambia: Unayo akili, roho, utambuzi na hisia,

kwa sababu zote hizo hazingii katika vipimo vingine. Amesema kweli aliyesema: Mwenye kukosa imani ya kumwamini Mwenyezi Mungu, basi amejikosa yeeye mwenyewe.

Unaweza kuuliza: Kuna faida gani ya kuelezea kuwa haki inawafunukia watu wa Kitabu wakati wa maumivu ya kukaa roho ambapo inajulikana kuwa wao katika hali hii hawawezi kufanya lolote?

Jibu: Lengo la hilo ni kuhimiza kufanya haraka kusahihisha imani yao kabla ya kupata hasara ya kupitwa na wakati na maumivu ya kukata roho; sawa na lengo la kuelezea pepo na moto.

Na Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.

Kesho Isa ^(a.s) atawatolea ushahidi Mayahudi kwamba wao walimfanyia uadui kwa ukafiri na inadi kwa yale aliyokuja nayo kutoka kwa Mwenyezi Mungu; na atawashuhudilia Wakristo kwamba wao walizidi sana kiasi cha kupetuka yale aliyowaamrisha kumwabudu Mwenyezi Mungu peke yake:

﴿مَا قُلْتُ لَهُمْ إِلَّا مَا أَمْرَتَنِي بِهِ أَنْ اعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ﴾

"Sikuwaambia ila yale uliyoniamrisha kuwa mwambuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu" (5:117)

Mitume wote, Muhammad akiwa mstari wa mbele, watamshuhudulia kila mwenye kukengeuka na yale aliyokuja nayo na kuwfikishia:

﴿وَيَوْمَ نَبْعَثُ فِي كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا عَلَيْهِمْ مِّنْ أَنفُسِهِمْ وَجِئْنَا بِكَ شَهِيدًا عَلَىٰ هُؤُلَاءِ﴾

"Na siku tutakapompeleka shahidi katika kila umma juu yao kutoka mionganoni mwao na wewe tutakuleta uwe shahidi juu ya hawa" (16:89)

﴿فَقِظْلُمٌ مِّنَ الَّذِينَ هَادُوا حَرَمَنَا عَلَيْهِمْ طَيِّبَاتٍ أَحْلَلْنَاهُمْ وَرَصَدْهُمْ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ كَثِيرًا﴾

160. Basi kwa dhuluma ya ambao ni Mayahudi tuliwaharamisha vitu vizuri walivyohalalishiwa, na kwa sababu ya kuzuilia kwao wengi na njia ya Mwenyezi Mungu.

﴿وَأَخْذِهِمُ الرِّبَا وَقَدْ نُهُوا عَنْهُ وَأَكْلِهِمْ أَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ مِنْهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا﴾

161. Na kuchukua kwao riba nao wamekatazwa, na kula kwao mali za watu kwa batili, na tumewaandalia makafiri adhabu yenyeye uchungu.

﴿لَكِنَ الرَّاسِخُونَ فِي الْعِلْمِ مِنْهُمْ وَالْمُؤْمِنُونَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلِكَ وَالْمُقْيِمِينَ الصَّلَاةَ وَالْمُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ أُولَئِكَ سَوْتِيهِمْ أَجْرًا عَظِيمًا﴾

162. Lakini waliobobea katika elimu mionganoni mwao na waumini, wanaamini uliyoteremshiwa na yaliyoteremshwa kabla yako. Na wenye kusimamisha Swala na wenye kutoa Zaka na wenye kumwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho hao tutawapa ujira mkubwa.

DHULMA YA MAYAHUDI

Aya 160 - 162

IRABU

Neno: **wenye kusimamisha Swala** ni yambwa (maf'ul) na kiima (fail) yuko kwenye kitendo kililichokadiriwa kuwa ni: Ninakusudia au ninasifu wenye kusimamisha Swala.

Lakini kuna msemaji aliyesema kuwa hili ni kosa la waandishi: Na akajibiwa kuwa Maimamu, wasomaji na maulama hawakubali hata kukosea umma wa Muhammad (**s.a.w.w**) katika yasiyokuwa maandishi ya Qur'an sembuse, kwenye maandishi yake! Swali hili limekuja kuwa kwa nini neno Muqimin limenasibishwa kwenye kusifiwa, lakini mengine yanayoungana nalo haya kunasibishwa?

Tunajibu: Huenda hilo ni kwa ajili ya kudhihirisha kima cha Swala na utukufu wake, na kwamba hiyo Swala ni nguzo ya dini na imani, ikikubaliwa hukubaliwa mengine na ikirudishwa hurudishwa mengine.

MAANA

Basi kwa dhuluma za ambaao ni **Mayahudi tuliwaharamishia** vitu vizuri walivyohalalishiwa, na kwa sababu ya kuzuilia kwao wengi na njia ya Mwenyezi Mungu.

Bado maneno yanaendelea juu ya Mayahudi na uovu wao. Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika Aya zilizotangulia ametaja ufedhuli wao wa kutaka kumuona Mwenyezi Mungu waziwazi, kumwabudu ndama, kukiuka miko ya Jumamosi, kuvunja ahadi na kuzikufuru ishara za Mwenyezi Mungu. Vilevile kuwaua kwao mitume, kusema, nyoyo zetu zimefumbwa, kumzulia Maryam na kujigamba kwao kumuua Masihi.

Na hapa ametaja kuwazuilia kwao watu na njia ya Mwenyezi Mungu na kula riba na rushwa; na kwamba yeye Mwenyezi Mungu kwa sababu ya uovu huu na fedheha hii, amewaharamisha katika duniya baadhi ya vitu vizuri vilivyokuwa halali kwao na kwa wengineo.

Na kuchukua kwao riba nao wamekatazwa.

Hayo yanaungana na 'basi kwa dhuluma.' Inasemekana kuwa Mayahudi ndio wa kwanza kuanzisha riba na kuihalalisha. Tumezungumzia hayo kwa ufafanuzi katika kufasiri Aya (2:275).

Na kula kwao mali za watu kwa batili; kama vile rushwa na njia nyinginezo za haramu. Mwenyezi Mungu amewasifu kuwa wao ni

"Wasikiao sana uwongo, walao sana haramu" (5:42)

Ama vizuri alivyowaharamishia ni vile alivyoviashiria Mwenyezi Mungu kwa kusema kwake:

﴿وَعَلَى الَّذِينَ هَادُوا حَرَمْنَا كُلَّ ذِي ظُفْرٍ وَمِنَ الْبَقَرِ وَالْغَنَمِ حَرَمْنَا عَلَيْهِمْ شُحُومَهُمَا إِلَّا مَا حَمَلَتْ ظُهُورُهُمَا أَوِ الْحُوَابِيَا أَوْ مَا اخْتَلَطَ بِعَظِيمٍ ذَلِكَ جَرِيَاتُهُمْ بِيَغْيِيهِمْ وَإِنَّا لَصَادِقُونَ﴾

"Na kwa wale walio Mayahudi tuliharimisha kila (mnyama) mwenye kucha, Na katika ng'ombe na kondoo na mbuzi tukawaharimishia shahamu yao isipokuwa ile iliyobeba migongo yao au matumbo au ile iliyogandamana na mifupa. Tuliwalipa hivyo kwa sababu ya uasi wao. Na hakika sisi ndio wa kweli" (6:146)

Tukilinganisha sera za Mayahudi wa tangu zamani, hasa katika zama za Musa, Isa na Muhammad na njia zao wanazotumia leo, hatuwezi kupata tofauti yoyote baina ya Mayahudi wa jana na wa leo, ikiwa ni pamoja na

upotevu, ujisadi, uadui kwa ubinadamu na heshima yake na kuacha kunyenyekaa mpaka wanyanyuliwe jabali vichwani mwao.

Hakuna jambo linalofahamishwa na hayo zaidi ya kuwa shari ni tabia ya asili katika uyahudi na ni umbile lisiloepukana nao; kadiri zama zigeukavyo na hali ziendeleavyo, sawa na nge asivyoweza kuacha kuuma na nyoka kudunga sumu yake.

Ikiwa kila mtu ana mwelekeo wa heri na shari, basi tabia ya Mayahudi inahusika na shari tu. Ikiwa utampata katika wao anayeijua haki na kuitumia basi hilo ni nadra sana, na nadra haivunji desturi bali ndio inaiimarisha. Amewavua Mwenyezi Mungu (s.w.t) hawa wachache kwa kauli yake:

Lakini waliobobeaa katika elimu miiongoni mwao na waumini, wanaamini uliyoteremshiwa na yaliyoteremshwa kabla yako.

Wenye kubobeaa katika elimu ni wale maulama wanaoitumia elimu yao, sio wale wanaoyajua yaliyoandikwa vitabuni tu, na wahakiki wanaozama katika utafiti wao na nadharia zao tu. Maana haya tumeyatoa katika kauli ya Amirul-muminin Ali ^(a.s): "**Elimu hukua kwa vitendo, vinginevyo itamuhamma.**"

Unaweza kuuliza: kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameunganisha waumini na wenye kubobeaa katika elimu na akaeleza kuwa wao kwa pamoja wanaamini Qur'an, Taurat na Injil. Na maelezo hayo yatafaa ikiwa ni kwa Mayahudi, wala hayafai kwa wanaomwamini Muhammad (s.a.w.w), kwa sababu maana yake yatakuwa ni waumini wanaamini, sawa na kusema waliosimama wamesimama na waliolala wamelala; na Qur'an imetakata na mifano hii, Sasa je, kuna tafsiri gani?

Jibu: Swali hili au mushkeli huu utakuwepo ikiwa tutafasiri waumini kuwa ni waumini katika sahaba wa Mtume na sio katika watu wa Kitabu; kama alivyofanya mwenye Majmaul-bayan na wala asizuiwe na Arrazi na mwenye Al-Manar na wafasiri wengi. Ama tukifasiri waumini kuwa ni Mayahudi wanaowafuata wenye kubobeaa katika elimu miiongoni mwao, basi swali hili halitakuwepo. Kwani maana yatakuwa ni wenye kubobeaa katika elimu miiongoni mwa Mayahudi na wenye kuchukua kauli zao katika watu wa mila zao, wanaamini Qur'an, Taurat na Injil. Wao wanaamini kwa dalili na hawa wanaamini kwa kufuata, Sisi tunapondokea kwenye tafsiri hii kuliko ya kwanza.

Na wenye kusimamisha Swala.

Maneno yamekuwa mengi kuhusu kunasibishwa (kusema Muqimini na sio Muqimun); mpaka ikapokewa kutoka kwa Athman na Aisha kuwa neno hili limekosewa, lakini Razi amebatilisha haya kwa kusema "Msahafu umenukuliwa kwa Mutawatir kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.w.t) itawezekana vipi kuthibiti kosa?"

Ilivyo sawa ni kwamba neno hili limenasibishwa na sifa; yaani ninawasifu wanaosimamisha Swala, kwa lengo la kuonyesha fadhila ya Swala na thamani yake; kama tulivyooleza katika kifungu cha Irabu.

Na wenye kutoa zaka, ni habari ya Mubtada (kianzio) kilichokadiria; yaani na hao ni wenye kutoa Zaka. Kwa maana ya kuwa wenye kuswali ambao wanastahiki sifa ni wale wanaoikutanisha Swala na kutoa Zaka. Na wenye kumwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Inaungana na

wenye kutoa Zaka. Ama malipo ya wote ameyaashiria Mwenyezi Mungu kwa kusema: Hao tutawapa ujira mkubwa.

﴿إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَىٰ نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِنْ بَعْدِهِ وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَطِ وَعِيسَى وَأَيُّوبَ وَيُونُسَ وَهَارُونَ وَسُلَيْمَانَ وَآتَيْنَا دَاوُدَ زُبُورًا﴾

163. Hakika sisi tumekuletea wahyi kama tulivyompelekea wahyi Nuh na Manabii baada yake. Na tukampelekea Wahyi Ibrahim na Ismail na Ishaq na Yaqub na wajukuu na Isa na Ayyub na Yunus na Harun na Suleiman; na Daud tukampa Zaburi.

﴿وَرُسُلًا قَدْ قَصَصْنَا هُمْ عَلَيْكَ مِنْ قَبْلِ وَرُسُلٍ وَكَلَمَ اللَّهُ مُوسَى تَكْلِيمًا﴾

164. Na mitume tuliokusimulia kabla na mitume ambao hatukukusimulia. Na Mwenyezi Mungu akanena na Musa maneno.

﴿رُسُلًا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لَعَلَّا يَكُونُ لِلنَّاسِ عَلَىٰ إِلَهٍ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا﴾

165. (Ni) Mitume wabashiri, waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya mitume; na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu mwenye hekima.

﴿لَكِنَّ اللَّهُ يَشْهُدُ بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ أَنَّهُ لَهُ بِعِلْمٍ وَالْمَلَائِكَةُ يَشْهُدُونَ وَكُفَّىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا﴾

166. Lakini Mwenyezi Mungu anayashuhudia aliyokuteremshia, Ameyateremsha kwa elimu yake na Malaika (pia) wanashuhudia; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.

TUMEKULETEAWAHYI

Aya 163 - 166

MAANA

Hakika sisi tumekuletea wahyi kama tulivyompelekea wahyi Nuh na manabii baada yake. Na tukampelekea wahyi Ibrahim na Ismail na Is-haq na Yaaqub na wajukuu na Isa na Ayyub na Yunus na Harun na Suleiman na Daud tukampa Zabur.

Makusudio ya wajukuu hapa ni wajukuu 12 katika watoto kumi na wawili wa Yaqub bin Is-haq bin Ibrahim. Makusudio ya wahyi kwa wajukuu ni mitume katika wao, sio wahyi kwa wao wote.

Aya hii na inayofuatia inaambatana na Aya zilizotangulia: Njia ya kuambatana kwake ni kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika Aya zilizotangulia ameelezea watu wa Kitabu kwamba wao wanaamini fikra ya utume na wanakubali kwamba Mwenyezi Mungu ana mitume, lakini wao hawawakubali wote, bali wanaamini baadhi na kukanusha baadhi. Muhammad ni mionganoni mwa wale wanaowakanusha. Pia amebainisha huko Mwenyezi Mungu kwamba mwenye kukanusha utume wa mmoja katika mitume yake basi ni kama aliyemkufuru Mwenyezi Mungu na kwamba imani sahihi ni kumwamini Mwenyezi Mungu, siku ya mwisho, Malaika wake, vitabu vyake vyote na mitume wake wote.

Kisha akathibitisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika Aya tunayoifasiri na iliyo baada yake, kwamba mwenye kukubali misingi ya utume, akaamini

utume wa mmoja wao, basi ni lazima aamini utume wa Muhammad (s.a.w.w), kwa sababu Mwenyezi Mungu amempelekea wahyi kama alivyowapelekea wengineo katika mitume na akadhihirisha mikononi mwake miujiza, kama alivyoidhihirisha kwa mitume wengine.

"Linalopatikana kwa maafikiano, haliwi ni sababu ya mafarikiano," na mwenye kufarikisha na kugawanya atakuwa amekifarikisha kitu na nafsi yake.

Na mitume tuliokusimulia kabla, na mitume ambao hatukukusimulia.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutaja majina ya mitume, katika Aya iliyotangulia, alisema kumwambia Mtume wake mtukufu kuwa kuna mitume wengine wasiokuwa hawa tumekusimulia kabla ya kushuka Sura hii na wako wengine hatukukusimulia.

Imeelezwa katika Al-manar kwamba Aya iliyokusanya zaidi majina ya mitume ni ile isemayo:

﴿وَوَهِبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ كُلُّا هَدَيْنَا وَتُوْحَادَ هَدَيْنَا مِنْ قَبْلٍ وَمِنْ ذُرْيَّ تِهِ دَأْوُدَ وَسُلَيْمَانَ وَأَيُّوبَ وَيُوسُفَ وَمُوسَى وَهَارُونَ وَكَذِيلَكَ تَجْزِي الْمُحْسِنِينَ ﴾ ٨٤﴿ وَرَّجَرِيَا وَيَحْيَى وَعِيسَى وَإِلَيْ أَسَاطِيرِ الْأَنْوَافِ كُلُّ مَنَ الصَّالِحِينَ ﴾ ٨٥﴾ وَإِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَيُونُسَ وَلُوطًا وَكُلُّا فَضَّلْنَا عَلَى الْعَالَمِينَ ﴾

"Na tukampa Is-haq na Yaqub, wote tukawaongoa. Na Nuh tulimwongoa kabla na katika kizazi chake, Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun, Na hivi ndivyo tuwalipavyo wafanyao mema. Na Zakaria na Yahya na Isa na Ilyas, wote ni mionganoni mwa watu wema. Na Ismail an Al-yasa na Yunus na Lut. Na wote tukafadhihisha juu ya walimwengu" (6:84.86)

Wengine ni Hud, Saleh na Shuaib nao ni katika waarabu.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema: "**Na mitume ambao hatukukuhadithia**" bila kuishiria idadi ya mitume ambao hakumtajia. Lakini watu wenye kuzidisha mambo wamekataa ila kutoa idadi, nao wakazidisha. Kuna mwenye kusema mia tatu na kumi na tatu (313).

Mwingine akasema ni, milioni moja laki nne na ishirini na nne elfu (1,424,000). Watatu akasema ni elfu nane (8,000), nusu yao wakiwa Waisrail. Na wanenaye akasema ni laki moja na ishirini na nne elfu (124,000). Kauli zote hizi na nyinginezo ni dhana za mbali. Ilivyo hasa ni kuwa Mwenyezi Mungu ndiye anayejua idadi yao na walivyo.

JE MITUME WOTE NI WA MASHARIKI?

Kuna swali linalomtokea kila mtu nalo ni je mitume wote ni wa Mashariki na wala hakuna aliyetokea Magharibi? Ikiwa wote ni kutoka Mashariki, je yuko Mchina, Mjapani au Mhindi? Au kutoka Mashariki ya mbali? Kisha je, ikichukuliwa kuwa wote ni wa Mashariki, tutaliwekaji hilo pamoja na misingi ya aliyesema:

Hakika Mwenyezi Mungu hawaachi watu bure bure; na kwamba hekima yake na rehema yake inahukumia kupelekea mitume kwa wote, "**watakaobashiria na kuonya**" (2:213)

Watakaowakumbusha na kuwaonyesha njia ili wasiwe na hoja yoyote kwa Mwenyezi Mungu. Na je, unakubalika msingi huu wa kuhusisha taifa kinyume na mataifa mingine na jinsi kinyume na jinsi nyingine?

Jibu: Hakika msingi huu usemao Mwenyezi Mungu hawaachi watu bure bure, na kwamba Mwenyezi Mungu hana budi kutoa hoja kabla ya hesabu na adhabu, ni msingi wa jumla usiokubali kuhusika na ardhi ya Mashariki au Magharibi, wala kwa jinsi nyeupe, ya njano au nyeusi.

Lakini hoja haifungamani tu na kupatikana Mtume kwa dhati yake katika kila mji na kila kizazi, bali msingi unakuwa kwa Mtume au kwa Kitabu kilichoteremshwa au kwa sharia ya Mwenyezi Mungu inayosimamiwa na manaibu wa mitume; hata pale Mwenyezi Mungu anapomfisha Mtume, bado hoja inakuwa imebaki kwa watu. Amirul-Mumin Ali ^(a.s) anasema katika hotuba ya kwanza, katika Nahjul-balagha "**Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakumwacha kiumbe wake asiwe na Nabii mwenye kutumwa au Kitabu chenye kuteremshwa au hoja yenyе kulazimiana au hoja iliyosimama.**"

Hoja yenyе kulazimiana ni naibu wa Mtume na hoja yenyе kusimama ni sharia iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu. kila moja ya hizi nne, iwe peke yake au pamoja na mwenzake inasimama kuwa ni hoja ya Mwenyezi Mungu kwa watu. Kwa hali hii basi ndio tunapata tafsir ya Aya isemayo:

﴿وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنْ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَبَيْوَا الطَّاغُوتَ﴾

"Na hakika tulipeleka Mtume katika kila umma ya kwamba muabuduni Mwenyezi Mungu na mijepushe na Taghut." (16:36)

Pia Aya isemayo: "Na hakuna uma wowote ila alipita humo muonyaji." (35:24) Vilevile tunapata tafsiri ya:

﴿فَكَيْفَ إِذَا جِئْنَا مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ بِشَهِيدٍ وَجَهَنَّمَ عَلَى هَؤُلَاءِ شَهِيدًا﴾

"Basi itakuwaje tutakopowaletea kila umma shahidi na tukakuleta wewe kuwa shahidi juu ya hawa." (4:41)

Makusudio ya Mtume katika Aya ya kwanza, mwonyaji katika Aya ya pili na shahidi katika Aya ya tatu, ni moja kati ya hoja nne: Mtume mwenyewe, naibu wake, Kitabu kilichoteremshwa na Mwenyezi Mungu au sharia. Inajulikana kuwa matatu ya mwisho, yanaishia kwa Mtume hivyo ikafaa kutegemeza shahada kwa Mtume.

Hapa kuna swalı linalojitokeza, nalo ni kuwa: kwa nini haikutajwa akili pamoja na hoja nyingine zilizotajwa pamoja na kuwa Mwenyezi Mungu anaitolea akili hoja kama amtoleavyo hoja Mtume?

Jibu: Akili ni hoja, hilo halina shaka, lakini hiyo ni hoja katika kujua kuweko Mwenyezi Mungu. Ama katika mengine, kama kujua Siku ya mwisho, halali ya Mwenyezi Mungu na haramu yake, hayo yanahitajia mwamshaji na mzinduzi atakayeongoza na kuweka njia sahihi ya kuyafikia. Kazi ya akili katika uwanja huu tulio nao ni kujua yale ayasemayo Mtume ya wajibu wa imani na dalili za uongofu wa heri ya dunia na akhera. Itakapofahamu akili ayasemayo Mtume, basi itakiri bila ya kusita.

Baada ya utangulizi huu ambaø hauna budi katika kufahamu maudhui yetu, tunarudi kwenye swalı, kuwa je, mitume wote ni wa Mashariki?

Tunajibu: Hapana! Ikiwa hatukupata habari ya mitume waliopelekwa kwa umma wa Magharibi na baadhi ya Mashariki, haina maana kuwa Mwenyezi Mungu hakupeleka Mtume yejote huko.

Pia sio dharura kwa kupeleka hoja kwa watu wa Magharibi kuwa Mtume lazima awe katika wao, bali anaweza kuwa ni wa Mashariki, lakini ujumbe wake ukaenea Mashariki na Magharibi, na kufikisha ujumbe huo kupita makhalifa wake na manaibu, kama alivyoambiwa Mtume Muhammad (**s.a.w.w**):

﴿وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا كَافَةً لِلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ﴾

"Na hatukutuma ila kwa watu wote, uwe mtoaji bishara na muonyaji, lakini watu wengi hawajui" (34:28)

Na akamwambia tena: "Na hatukutuma ila uwe rehma kwa walimwengu." (21:107).

Vitabu nya dini nya zamani vimeashiria kuwa risala ya Muhammad ni ya wote na kwamba ni rehema kwa viumbe vyote. Zaidi ya hayo, vimetaja jina la Abu Lahab kwa herufi na uadui wake kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (**s.a.w.w**) Abdul-haq Vidyarthi, amesema katika Kitabu Muhammad in World Scriptures (Muhammad katika vitabu nya dini za duniani): "Hakika jina la Mtume wa kiarabu limeandikwa kwa tamko lake la kiarabu, Ahmad, katika Sama Veda miongoni mwa vitabu nya Brahamanas¹.

kwenye sehemu ya sita na ya nane ya juzuu ya pili imeelezwa waziwazi kuwa Ahmad atapokea sharia kutoka kwa Mola wake nayo itakuwa imejazwa hekima, Na sifa za Al-Kaaba zimethibiti katika Kitabu Atharva Veda.

Na katika Kitabu Zand Avesta, ambacho ni mashuhuri kuwa ni Kitabu kitakatifu katika umajusi, imekuja habari ya Mtume akisifiwa kuwa yeze ni rehema kwa walimwengu, atakayelingania kwa Mwenyezi Mungu ambaye hakuwa yeote mfano wake, na atapingwa na adui anayeitwa Abu Lahab².

Haiwezekani habari hizi zitokee kwa asiyekuwa muumbwa. Hizo ni wahyi tu kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwenda kwa Mtume miongoni mwa mitume yake, hilo halina shaka. Kama si hivyo basi ni nani anayeweza kutoa habari ya utume wake kwamba baada ya maelfu mamia ya miaka atapatikana Mtume atakayeyitwa Ahmad, atakayelingania kwenye ibada ya Mungu mmoja tu aliye pekee, na atakayepingwa na adui aitwaye Abu Lahab?

Kwa hivyo basi katika habari hii kuna dalili ya wazi na ya kweli juu ya mambo mawili:

Kwanza: ukweli wa Muhammad katika utume wake na kuenea risala yake.

Pili: kwamba Mwenyezi Mungu alituma mitume hapo zamani ambao hatukuwasikia au visa vyao pia hatukuvisikia; kisha hatujui, pengine maji-

Baada ya yote hayo ni kwamba kutumwa Mtume Mashariki na Magharibi ni maudhui muhimu yanayotaka Kitabu mbali. Ama mnasaba huu, ambao ni tafsiri ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "na mitume

1 Vitabu nya wahindi

2 Kitabu Muhammad in World Scriptures, kimechapishwa kwa lugha ya Kingereza na kunukuliwa na Aqqad katika Kitabu chake Abqdrriyyatul-Islamiyya; na sisi tumenukuu kutoka kwa Aqqad na ya wenye hekima, tunayosikia au kuyasoma ni ya mitume na kwamba mafunzo yao yametoweka au yamefutika.

ambao hatukukusimulia." Hauwezi kuchukua zaidi ya tuliyoyataja; na huenda tukapetuka mpaka.

Tunamwomba Mwenyezi Mungu kumpa, kwa maudhui haya ya kielimu yenyenye kunufaisha, elimu na uvumilimivu kila mwenye kufanya utafiti na uchunguzi.

Na Mwenyezi Mungu akanena na Musa maneno.

Mwenyezi Mungu amemtaja Musa peke yake katika jumla hii, kwa sababu yeze ndiye aliyemhusu kusema naye, kinyume na wengine, ingawaje mitume wote walipokea maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini mazungumzo hayo yalikuwa kwa namna aliyoitaja Mwenyezi Mungu:

﴿وَمَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُكَلِّمَهُ اللَّهُ إِلَّا وَحْدَهُ أَوْ مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ أُوْرِسَلَ رَسُولًا فَيُوحِي بِإِذْنِنِهِ مَا يَشَاءُ﴾

"Na haikuwa kwa mtu kwamba Mwenyezi Mungu aseme naye ila kwa wahyi au kwa nyuma ya pazia au humtuma mjumbe naye humpa wahyi" (42:51)

Kwa hiyo mazungumzo ya Musa na Mwenyezi Mungu yalikuwa ni nyuma ya pazia. Hakuna yeyote anayejua hali ya pazia hii na ilikuwaje. Mwenyezi Mungu amelinyamazia hilo na sisi tunalinmyamazia, kama alivyolinyamazia Yeye Mwenyewe.

Kwa hali yoyote iwayo, kuhusishwa Musa na kuzungumza na Mwenyezi Mungu hakupunguzi kitu kwa mitume wengine, wala hakufahamishi kuwa yeze ni bora na mkamilifu zaidi ya wengine, hapana! Kwani kumtuma roho mwaminifu kwa wa mwisho wa mitume ni daraja ya juu na ya ukamilifu zaidi.

(Ni) Mitume wabashiri, waonyaji ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya mitume.

Desturi ya 'Hakuna adhabu bila ya ubainifu,' kama wanavyosema mafakihi au 'Hakuna adhabu bila ya kauli wazi,' kama wasemavyo watunga sheria, ni wazi kabisa, isiyohitaji dalili, bali hiyo yenye ni dalili. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakumwacha binadamu bure bure, bali alimwamrisha na akamkataza, na hapana budi kwake kumfikilizia amri na makatazo haya ili awe na hoja, hata kama atahalifu.

Na hoja zake hazifahamiki ila kwa wahyi; na kwa kuwa mitume ndio kiungo cha kati baina ya Mwenyezi Mungu na viumbe vyake katika kufikisha hukumu zake, na ahadi zake, ndipo Mwenyezi Mungu akawatuma mitume watoao habari njema na waonyaji. Ili kusiweko na nafasi ya kutoa udhuru na sababu. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَلَوْ أَنَّا أَهْلَكْنَاهُمْ بِعَذَابٍ مِّنْ قَبْلِهِ لَقَالُوا رَبَّنَا لَوْلَا أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا فَنَتَّبَعَ آيَاتِكَ مِنْ قَبْلِنَا أَنَّا نَنْدِلُ وَنَخْرُجُ﴾

"Na lau kama tungeliwangaamiza kwa adhabu kabla yake wangesema: Ewe Mola wetu! Kwa nini usituletee mtume tukazifuata ishara zako kabla hatujadhalilika na kufedheheka?" (20: 134)

Tumezunguzumzia kuhusu ubaya wa adhabu bila ya ubainifu katika kufasiri (2:159)

Lakini Mwenyezi Mungu anayashuhudia aliyokuteremshia. Ameyateremsha kwa elimu yake, na Malaika (pia) wanashuhudia; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.

Ushahidi unakuwa kwa kauli na au kwa vitendo, kama ushahidi wa ulimwengu kwa kuwepo muumbaji na uweza wake, au ushahidi wa kutoa kwa kuwepo mtoaji na ukarimu wake na ushahidi wa ujasiri kwa ushuja wa mjasiri na nguvu zake. Ushahidi wa vitendo ni dalili zaidi na una nguvu kuliko ushahidi wa kauli ambao unakuwa na shakashaka.

Miongoni mwa ushahidi wa vitendo ni ushahidi wa Mwenyezi Mungu kwa Muhammad (**s.a.w.w**) alipompa dalili na miujiza ya ukweli.

Mwingine ni Qur'an Tukufu aliyoteremsha kwa elimu yake. Maana ya 'kwa elimu yake' ni kwamba Qur'an inatokana na elimu ya Mwenyezi Mungu sio elimu ya viumbe ambayo inakuwa na makosa na mapendeleao.

Ama ushahidi wa Malaika, unafuatilia wa Mwenyezi Mungu ambao unatoshelezea ushahidi wote Ndipo Mwenyezi Mungu akasema: "**na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.**"

Baada ya hayo ni kwamba hakuna asiyependa kusadikiwa na watu katika anayoyasema, lakini mwenye akili huwa hajishughulishi na hilo kabisa hata akifanywa mwongo na kujibiwa maneno yake, maadamu ana yakini ya ukweli wake.

Hilo ndilo linalokusudiwa na Aya. Ni kama kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) anamwambia Mtume wake. "Usikushughulishe ukadhibishaji wa mwenye kukadhibisha utume wako na upinzani wa mwenye kupinga mwito wako, maadamu kwangu umkweli mwenye kusadikisha"

Aya hii ina makusudio kama yanayokusudiwa na Aya isemayo:

﴿فَلَا تَدْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسَرَاتٍ إِنَّ اللَّهَ عَلَيْمٌ بِمَا يَصْنَعُونَ﴾

"Basi roho yako isitoke kwa kuwasikitikia, **Hakiika Mwenyezi Mungu anayajua wanayoyafanya**" (35:8)

TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

﴿إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ قَدْ ضَلُّوا ضَلَالًا بَعِيدًا﴾

167. Hakika wale waliokufuru na kuzuilia (watu) na njia ya Mwenyezi Mungu, wamekwishapotea upotevu ulio mbali.

﴿إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَظَلَمُوا لَمْ يَكُنْ اللَّهُ لِيَغْفِرَ لَهُمْ وَلَا يَهْدِيهِمْ طَرِيقًا﴾

168. Hakika wale waliokufuru na kudhulumu, haitakuwa kwa Mwenyezi Mungu kuwasamehe wala kuwaongoza njia.

﴿إِلَّا طَرِيقٌ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ بَسِيرًا﴾

169. Isipokuwa njia ya Jahannam, humo watadumu milele. Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.

﴿يَا أَيُّهَا الرَّأْسُ قَدْ جَاءَكُمُ الرَّسُولُ بِالْحَقِّ مِنْ رَبِّكُمْ فَامْتُوْا حَيْرًا لَكُمْ وَإِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ اللَّهَ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا﴾

170. Enyi watu! Amekwishawafikia Mtume kwa haki kutoka kwa Mola wenu, basi aminini (itakuwa) kheri kwenu. Na kama mtakataa, basi hakika ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo mbinguni na ardhini, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi mwenye hekima.

WALIKUFURU NA KUZUILIA

Aya 167 – 170

MAANA

Hakika wale waliokufuru na kuzuilia (watu) na njia ya Mwenyezi Mungu wamekwishapotea upotofu ulio mbali.

Anasema Razi na wengineo katika wafasiri, kuwa sifa hizi ni za Mayahudi, kwa sababu wao waliukufuru Uislamu na kuwazuia wengine kwa kuingiza shaka kwenye nyoyo za wenye akili.

Hakika wale waliokufuru na wakadhulumu haitakuwa kwa Mwenyezi Mungu kuwasamehe wala kuwaongoza njia, isipokuwa njia ya Jahannam, humo watadumu milele.

Baadhi ya wafasiri wanaona kuwa Aya ya kwanza inahusika na Mayahudi, na hii inahusika na washirikina; na kwamba Mayahudi walizulia watu na uislamu kwa kuingizia shaka, na washirikina wakazuia kwa dhulma, ambapo walimtangazia vita Muhammad (s.a.w.w) na wakapigana naye mara nyingi.

Mwenyezi Mungu hatawasamehe wao wala wengine maadamu wako kwenye upotevu, wala hatawaongoza huko akhera isipokuwa kwenye njia ya Jahannam. Kwa sababu hapa duniani walifuata njia ya upotevu, wakaiacha njia ya uongofu ingawaje walionya.

Kauli yake Mwenyezi Mungu 'milele' ni dalili ya kubakia kwao motoni na kutokatikiwa na adhabu. Lau si tamko hilo (Milele) basi ingekuwa kuna uwezekano ama wa kudumu milele au kukaa sana katika Jahannaam.

Enyi watu! Amekwishawafikia Mtume kwa haki kutoka kwa Mola wenu. Basi aminini (itakuwa) kheri kwenu.

Makusudio ya Mtume ni Muhammad (**s.a.w.w**). Na mwito unawaenea watu wote, wakati wote na mahali popote. Kwa sababu kumwamini Muhammad (**s.a.w.w**) na mwito wake ni haki; na wajibu wa imani ya haki hauhusiki na mtu fulani wala wakati fulani.

Kauli yake Mwenyezi Mungu: kwa haki kutoka kwa Mola wenu, inajulisha kuwa; Uislamu haukubali utawala wowote isipokuwa utawala wa haki. Mwenye kutii, atakuwa mwenye kukurubishwa kwa Mwenyezi Mungu na mwenye kuasi basi hakika ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo mbinguni na ardhini; na Mwenyezi Mungu ni mjuzi mwenye hekima.

﴿يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَا تَغْلُبُوا فِي دِينِكُمْ وَلَا تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقُّ إِنَّمَا الْمُسِيحُ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ رَسُولُ اللَّهِ وَكَلِمَتُهُ الْقَاتِلَةُ إِلَى مَرْيَمَ وَرُوحٌ مِّنْهُ فَآمَنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَلَا تَقُولُوا ثَلَاثَةٌ انتَهُوا خَيْرًا لَّكُمْ إِنَّمَا اللَّهُ إِلَهُ وَاحِدٌ سُبْحَانَهُ أَن يَكُونَ لَهُ وَلَكُمْ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَكَفَى بِاللَّهِ وَكِيلًا﴾

171. Enyi watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo haki. Masih Isa bin Maryam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno lake tu alilompelekea Maryam, na ni roho iliyotoka kwake. Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na mitume wake; wala msiseme watatu. Komeni!, itakuwa kheri kwenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mungu mmoja tu. Ameepukana kuwa na mtoto. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi.

﴿لَن يَسْتَكِفَ الْمُسِيحُ أَن يَكُونَ عَبْدًا لِّلَّهِ وَلَا الْمَلَائِكَةُ الْمُقَرَّبُونَ وَمَن يَسْتَكِفُ عَنْ عِبَادَتِهِ وَيَسْتَكِبِرُ فَسَيَحْشُرُهُمْ إِلَيْهِ جَمِيعًا﴾

172. Masih hataona unyonge kuwa mtumwa wa Mwenyezi Mungu wala Malaika wenye kukurubishwa. Na watakaoona unyonge utumwa wa Mwenyezi Mungu na kutakabari, basi atawakusanya wote kwake.

﴿فَإِنَّمَا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَيُؤْفَيُهُمْ أُجُورُهُمْ هُمْ وَرِيزِيدُهُمْ مِّنْ فَضْلِهِ وَإِنَّمَا الَّذِينَ اسْتَنَكُفُوا وَاسْتَكَبَرُوا فَيُعَذَّبُهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا وَلَا يَجِدُونَ لَهُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا﴾

173. Ama wale ambao wameamini na wakatenda mema, atawalipa ujira wao sawa, na atawazidishia kwa fadhila yake. Na ama wale walioona utumwa na wakafanya kiburi, basi atawaadhibu adhabu iliyo chungu. Wala hawatopata mlinzi wala wa kuwasaidia.

MSIPETUKE MIPAKA KATIKA DINI YENU

Aya 171-173

MAANA

Enyi watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo haki. Masih Isa bin Maryam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno lake tu alilompelekea Maryam, na ni roho iliyotoka kwake. Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na mitume wake; wala

msiseme watatu. Komeni!, itakuwa kheri kwenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mungu mmoja tu. Ameepukana kuwa na mtoto. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi.

Haufichiki kwake utiifu wa mwenye kutii wala uasi wa mwenye kuasi, Na hekima yake imepitisha kumlipa kila mmoja anavyostahiki katika thawabu au adhabu.

Hatuju dini iliyositisiza na kutilia mkazo katika itikadi ya Tawhid (Umoja wa Mungu), kama Uislamu. Mwenyezi Mungu hana mfano wala kinyume chake, hana maingiliano wala mfungamano. "**Hakuna chochote kama mfano wake**"(42:11) Huu ndio msingi unaosimamia itikadi ya kiislamu.

Ajabu ni ya yule asemaye. "Ikiwa Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kuumba kila kitu, basi inatakiana kuweza kuumba Mwenyezi Mungu mfano wake." La ajabu katika kauli hii ni kuchanganya sifa za Muumbaji na aliyeumbwa, na mwenye kuabudu na mwenye kuabudiwa, katika dhati moja. Ni wazi kuwa mwenye kuumba hawesi kuwa mwenye kuumbwa isipokuwa kwa yule asemaye kuwa Masih ana hali mbili: Ya kimungu na ya kibinadamu.

Tumezungumzia yaliyosemwa kuhusu Bwana Masih katika kufasiri Sura (3:58), na kuhusu Tawhid na kukanusha ushirikina na utatu katika kufasiri (4:50), Vile vile tumezungumzia kupetuka mipaka katika kufasiri Sura (3:128). Na sasa tunarudia tena maudhui haya kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Enyi watu wa Kitabu, 'Msipite kiasi katika dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo haki.

Wote Mayahudi na Wakristo walisema kauli ya kupita kiasi. Mayahudi walimteremsha chini kabisa; na Wakristo wakampandisha juu mpaka kufikia uungu. Ama Waislamu wamesema yaliyosemwa na Qur'an; na hiyo ni kauli ya katikati baina ya kauli zote mbili.

Katika Aya iliyotangulia msemo ulielekezwa kwa Mayahudi na katika Aya hii unaelekezwa kwa Wakristo kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Wala msiseme watatu." Huku ndiko kupita kiasi katika dini na kauli ya batili. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ametakata na ushirika na maingiliano yoyote au mafungumano na kuwa na mwenzi.

QUR'AN NA WANAOHUBIRI UTATU

Masih Isa bin Maryam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno lake tu alilompelekea Maryam.

Hii ndiyo hakika ya Isa, na ndiyo waliyoizungumzia Waislamu. Ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, basi imetosha, kama Ibrahim, Musa na Mitume wengineo.

Tulikuwa pamoja na wahubiri wa kikristo katika sehemu zilizotangulia za tafsiri hii na sasa tuko nao katika tafsiri ya Aya hii; Kwa sababu wana kisa chao utakachokijua baadaye.

Kwanza tunaanza na swalii, kama desturi yetu, katika kutaka kufafanua, ili msomaji aendelee mpaka mwisho bila ya kuhisi kuchoka au kukimwa.

Swali ni: Vipi Isa awe kama mitume wengine na yeze amezaliwa bila baba, jambo ambalo si la kawaida, na wengine wote wamezaliwa na baba zao?

Mwenyezi Mungu Mwenyeze amelijibu swali hili na akalifupisha kwa mfupisho huu wa ajabu: "Na neno lake alilompeleke Maryam, na ni roho iliyotoka kwake."

Kwa ufanuzi zaidi, ni kuwa kauli ya Wakristo, kuzaliwa bila baba ni sahihi. Vilevile ni sahihi kuwa hili si jambo la kawaida, lakini kosa linakuwa pale wanaposema kuwa huku kutokuwa kawaida ndio daliili ya uungu wa Isa. Njia ya makosa ni kuwa kukosekana baba hakulazimiani na kupatikana uungu. Vinginevyo, basi inalazimika Adam awe Mungu, bali yeze ndiye anayestahiki zaidi kuwa Mungu kuliko Isa, kutokana na mantiki yao, kwa sababu ameumbwa bila ya baba na bila ya mama; na Isa amezaliwa na mama.

Zaidi ya hayo, ni kwamba kutokuwepo kawaida si hoja, kwani moto ulikuwa baridi na salama kwa Ibrahim; basi inatakitana awe Mungu, kwa vile hilo ni jambo lisilo la kawaida. Kisha je, kuna la zaidi gani kwa aliyeumba ulimwengu wa ajabu bila ya kitu chochote ila kwa neno moja tu, 'kuwa na ikawa' (36:82), na kuumba mtu bila ya baba? Je, kuumbwa Isa (a.s) ni jambo kubwa kuliko kuumbwa mbingu na ardhi?

﴿خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ﴾

"Kwa hakika umbo la mbingu na ardhi ni kubwa kuliko umbo la wanadamu, lakini watu wengi hawajui".(40:57)

Kwa hiyo neno 'kuwa na ikawa,' ndilo lile lile alilolitumia kwa mja wake Isa, katika kauli yake 'na neno lake alilompeleke Maryam.' Maana ya kumpeleke Maryam, ni kuwa Mwenyezi Mungu alimfahamisha Maryam kuzaliwa mtoto huyu kupitia Malaika. Kwa hiyo 'neno' hapa ndiyo 'neno' kama ilivyo hapo nyuma.

Ama roho aliyomsifu nayo Mwenyezi Mungu (swt) Isa katika Aya hii na nyinginezo makusudio yake ni uhai ambao hauna chimbuko isipokuwa kwake Yeye Mtukufu, na kwamba Mwenyezi Mungu (swt) alimpa uhai huo Isa na akaupa uhai udongo wa Adam:

﴿إِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي خَالِقٌ بَشَرًا مِنْ طِينٍ ﴾ ٧١ ﴿فَإِذَا سَوَّيْتُهُ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِنْ رُوحِي﴾

"Mola Wako alipowaambia Malaika: Hakika mimi nitaumba mtu kwa udongo. Na nitakapomkamilisha na kumpulizia roho yangu" (38:71-72) Kwa hiyo roho katika udongo wa Adam ndiyo roho katika tumbo la Maryam. Yasemwayo huko ndiyo yasemwayo hapa. Kutofautisha ni kuonea tu!

Wahubiri wa kanisa wamejaribu kuwababaisha wasiokuwa na ujuzi wa Kitabu na siri za lugha, kuwa kauli yake Mwenyezi Mungu 'na neno lake na roho iliyotoka kwake' ni hoja yao sio jibu la kuwarudishia wao baada ya kufasiri neno na roho, kwa maana ya mfano wa Mwenyezi Mungu na sifa zake, sio kwa maana ya athari mionganoni mwa athari za uwezo wake na ukuu wake, kama ilivyo sawa.

Lau lingekuja neno la Mwenyezi Mungu na roho yake katika mfumo mwingine, basi tungeichukulia tafsiri ya makosa kuwa si hadaa wala vitimbi. Lakini wahubri wameyageuza maana ya kukataza yaliyo katika matamko haya mawili, kwa niya mbaya. La kwanza linakataza kupita kiasi katika Bwana Masih ^(a.s). La pili linakataza kauli ya utatu na kumnasibishia mtoto. Kisha wakayafasiri matamko hayo kulingana na vile inavyoafikiana na matakwa yao na makusudio yao, sio vile ilivyo katika makamusi ya lugha. Maana ya haya yote ni kuhadaa na kutatiza.

Hebu turudie Aya yote ili msomaji asipotee.

Enyi watu wa Kitabu! Msipite kiasi katika dini yenu, wala msiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila yaliyo haki. Masih Isa bin Maryam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na neno lake tu alilompelekea Maryam, na ni roho iliyotoka kwake. Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na mitume yake; wala msiseme watatu. Komeni!, itakuwa kheri kwenu. Hakika Mungu ni mmoja tu. Ameepukana kuwa na mtoto. Ni vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi.

Je, baada ya maandishi haya yaliyo wazi kuna sababu za kufasiri Neno la Mungu na roho ya Mwenyezi Mungu kuwa ni dhati yake na sifa zake? Hakuna sababu yoyote, hata kama matamko haya yangekuja mbalimbali, haiwezi kufaa tafsiri hii kwa namna yoyote kwa Qur'an ambayo imesema kwa lugha iliyo wazi:

﴿لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ ثَلَاثَةٍ﴾

"Hakika wamekufuru wale waliosema kuwa Mwenyezi Mungu ni watatu wa utatu" (5:73)

Ni umbali ulioje wa kukufurisha huku kuliko wazi, kuwa Qur'an inawaunga mkono Wakristo katika kusema kwao kuwa Masih ni Mungu au ni mwana wa Mungu au kuwa ana sifa za uungu! Ikiwa Qur'an ni hoja katika Aya zake au matamko yake, basi ni wajibu vilevile kauli yake iwe ni hoja:

﴿يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَمْ تَلِمِسُونَ الْحُقْقَ بِالْبَاطِلِ وَلَا يَخْتَمُونَ الْحُقْقَ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ﴾

"Enyi watu wa Kitabu! Mbona mnachanganya haki na batil na mnaficha haki, hali mnajua"¹ (3:71)

Ikiwa Qur'an si hoja katika kauli yake hii, basi ni wajibu kutokuwa hoja pia mahali pengine. Ama kuamini yote au kukanusha yote, kutofautisha ni hadaa tu.

Wengi katika wahubiri wamemfanya uovu Bwana Masih na wakajifanyia uovu wao wenyewe, kwa kubadilisha na kugeuza ambako tumekutolea mfano katika yale matamko mawili. Hebu tukisie kwamba mtu wa kawaida amehadaika kwa sababu yao, je, hii itakuwa ni faida kwa Masih au Wakristo? Itakuwaje ukweli wa mambo ukifichuka?

¹ La kushangaza zaidi ni yale niliyoyasoma kuhusu kauli ya baadhi ya wahubiri na Wastashriq kwamba Muhammad amechukua mafunzo yake kutoka Injili na Ulama wa Kiyahudi. Nasi twauliza, je, Muhammad amechukua pia hizi Aya mbili na nyinezo na hadith ambazo wanazikana Wakristo? Je mafunzo yote hayo ameyachukua kutoka kwa watu wa kanisa waliokwa katika zama zake. Ikiwa ni hivyo basi huku ni kukubali wao wenyewe ukafiri wao.

Masih hataona unyonge kuwa mtumwa wa Mwenyezi Mungu wala Malaika wenye kukurubishwa.

Kwa sababu hana njia ya kupata thawabu na kuokoka na adhabu yake isipokuwa kwa kumwabudu yeye peke yake.

Na watakaoona unyonge utumwa wa Mwenyezi Mungu na kutakabari, basi atawakusanya wote kwake.

Huko watangojwa na adhabu kali. Hatuna la zaidi la kutafsiri kauli yake Mwenyezi Mungu:

Ama wale ambao wameamini na wakatenda mema.

Mpaka mwisho wa Aya. Kwa sababu ni wazi zaidi kuliko kufasiriwa. Hata pale niliposema "Huko watangojewa na adhabu kali" Ni kiasi cha kujaza nafasi tu kama ambavyo msomaji ataona, Namna hii wamefanya wengineo katika wafasiri. Sheikh wao mkubwa Tabari amesema:

"**Hataona unyonge** yaani hajitukuzi, **Na watakaoona unyonge** yaani watakaojituza: Na mwanafalsafa wao Arrazi akasema:" Hataona unyonge, Amesema Azzujaji yaani hajitukuzi, Na watakaoona unyonge yaani walio na unyonge"

Mifano ya hayo ni mingi. Ndio mshairi akajisemea: Wameyafasiri maji baada ya juhudu kuwa ni maji. Hilo walilifanya kwa kujua na kwa makusudi, si kwa lolote ila ni kwamba mfasiri wa Qur'an ni wajibu, kama wanavyodai, afasiri kila linalomjia, hata kama Aya iko wazi. Wameghafilika na yale waliyoyasema walipofasiri kauli yake Mwenyezi Mungu: "Ndani yake zimo Aya zilizo waziwazi, ambazo ndizo msingi wa Kitabu, na nyingine zenye kufichikana." Na kwamba kuzifafanua zilizo wazi, ni mushkeli zaidi ya mushkeli.

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمْ بُرْهَانٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَأَنَّا لَنَا إِلَيْكُمْ نُورًا مُّبِينًا﴾

174. Enyi watu! Imewafikia hoja kutoka kwa Mola wenu na tumewateremshia nuru iliyowazi.

﴿فَأَمَّا الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَاعْتَصَمُوا بِهِ فَسَيُدْخَلُوهُمْ فِي رَحْمَةٍ مَّنْهُ وَفَضْلٍ وَيَهْدِيهِمْ إِلَيْهِ صِرَاطًا مُّسْتَقِيمًا﴾

175. Ama wale waliomwamini Mwenyezi Mungu na wakashikamana naye, basi atawaingiza katika rehema itokayo kwake na fadhila na atawaongoza kwake kwa njia iliyonyooka.

IMEWAFIKIA HOJA KUTOKAKWA MOLA WENU

Aya ya 174 - 175

MAANA

Enyi watu! Imewafikia hoja kutoka kwa Mola wenu, na tumewateremshia nuru iliyowazi.

Aya zilizotangulia zimeelezea hoja ya Mayahudi na Wakristo. Baada ya Mwenyezi Mungu kusimamisha hoja kwa wote, amewatolea mwito wote kumwamini Muhammad (**s.a.w.w**) na Qur'an Tukufu.

Wameafikiana wafasiri kuwa makusudio ya hoja ni Muhammad, na nuru iliyowazi ni Qur'an na kila anayemfuata Muhammad. Kitabu cha Mwenyezi Mungu ni dalili ya mkato ya kuhakikisha haki na kubatilisha batili, na ni nuru iliyoneea inayoongoza kwenye usawa. Kwa sababu vyote viwili

vinazungumza kwa Wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu tu. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿قُلْ مَا كُنْتُ بِدُعَاءٍ مِّنَ الرُّسُلِ وَمَا أَذْرِي مَا يُفْعَلُ بِي وَلَا يَكُنْ إِنْ أَتَيْتُ إِلَّا مَا يُؤْخَذُ إِلَيَّ وَمَا أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ مُّسِينٌ﴾

"Sema: mimi si kioja katika mitume; wala sijui nitakavyofanywa mimi wala nyinyi, sifuati ila niliyopewa wahyi na mimi si lolote ila ni muonyaji mwenye kubainisha." (46:9)

Ama dalili ya kuwa Muhammad na Qur'an ni wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kwamba ni hoja, haiwezi kufupilizwa na yanayosemwa katika tafsiri ya Aya.

Wahakiki wametunga mamia ya vitabu kuhusu hizo dalili, Tumevitaja vingi kila inapohitajika katika Tafsir yetu hii, Ni juu ya mwenye kuitafuta haki kufanya utafiti na kufuutilia. Kuna kitu kimoja tunachomwomba huyo mtafutaji, asighafilike nacho - alinganishe baina ya mafunzo ya Qur'an na mafunzo ya vitabu vya dini nyingine.

Vilevile afanye utafiti wa idadi ya Injil, zilikuwa ngapi katika karne ya kwanza au ya pili baada ya kuzaliwa Isa (a.s)? Afanye utafiti, kwa nini walifanya mkutano wa Maaskofu huko Nicaea¹ mwaka 325 AD ambao uliwajumuisha Maaskofu elfu mbili na arobaini (2040) waliwakilisha makanisa yote ulimwenguni? Je, walifikiana nini katika kongamano hili? Je, walifikiana Maaskofu wote kuwa Isa ni Mungu, au kuna wengine waliosema ni kiumbe na wengine wakasema ni Mungu? Je, waliingilia suala la asili ya tatu - roho mtakatifu na kutaja uungu wake, au uliokubali uungu wa asili hii ni mkutano uliofanywa Constantine mwaka 381 AD na kwamba asili hii haikujulikana² kabla ya tarehe hii?

Tunamtaka yule anayetafuta haki kufanya utafiti kwa upande huu na sisi tuko pamoja naye katika natija yoyote atakayoishilia nayo.

Ama wale waliomwamini Mwenyezi Mungu na wakashikamana naye, basi atawaingiza katika rehema itokayo kwake na fadhila na atawaongoza kwake kwa njia iliyonyooka.

Baadhi ya wafasiri wametofautisha baina ya rehema na fadhila, kwamba rehema inakuwa duniani na fadhila itakuwa akhera. Mwingine akasema akimnukuu Ibn Abbas, kwamba rehema ni pepo na fadhila ni ile ambayo hakuna jicho lilioiona wala sikio lililoisikia, Lakini huyu inaonekana alitaka kutofautisha, akachanganya. Kwa sababu sifa hizi ni za pepo hasa.

Ama sisi hatuoni tofauti yoyote baina ya rehema na fadhila. Inafaa kuunganishwa kimatamko tu, jambo ambalo linaptikana sana katika lugha ya kiarabu na linapendeza, Nalo huitwa kuunganisha tafsiri.

Maana kwa ujumla ni kuwa mwenye kumwamini Mwenyezi Mungu na akamtegemea yeye tu, basi atakuwa katika rehema ya Mwenyezi Mungu na fadhila yake duniani na akhera. Duniani atapewa tawfiki na uongofu wa njia

1 Mji wa zamani ulioko Turkey uliojulikana kama Byzantain, Costantine wa kwanza alieujenga upya na kuita jina lake. Ulikuwa mji mkuu wa Ugiriki, ukawa wa Roma, hatimae ukawa mikononi mwa dola ya Uthmaniya na kuwa mji mkuu wake, ukaitwa Istanbul.

2 Mji wa zamani katika Asia , sasa ni sehemu katika Uturuki.

ya kuielekea haki, hataiacha kabisa. Ama huko akhera basi ni raha, manukato na mabustani yenyne neema.

Ufupisho wa tafsiri ya Aya hii ni kauli ya Amirul-Muminin (a.s): "**Mola mwenye kurehemu na dini iliyo sawa.**" Kila mtu na alichokichagua.

﴿يَسْتَفْتُونَكُلِّ الَّهُ يُفْتِيَكُمْ فِي الْكَلَالَةِ إِنْ أَمْرُوا هَلَكَ لَيْسَ لَهُ وَلَدٌ وَلَهُ أَخْتٌ فَلَهَا نِصْفٌ مَا تَرَكَ وَهُوَ يَرِثُهَا إِنْ لَمْ يَكُنْ لَّهَا وَلَدٌ فَإِنْ كَانَتَا اثْتَتَيْنِ فَلَهُمَا الشُّلُّانِ مِمَّا تَرَكَ وَإِنْ كَانُوا إِخْوَةً رِجَالًا وَنِسَاءً فَلِلَّهِ كُلُّ حَظٍ الْأُنْتَيْنِ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ أَنَّ تَضِلُّوا وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ﴾

176. Wanakuuliza fatwa; sema: Mwenyezi Mungu anawapa fatwa juu ya mkiwa. Iwapo mtu amekufa hali hana mtoto na anaye ndugu wa kike, basi (huyo dada) atapata nusu ya alichokiacha. Naye atamrithi nduguye wa kike akiwa hana mtoto. Wakiwa ni ndugu wa kike wawili basi watapata theluthi mbili za alichokiacha. Na wakiwa ni ndugu wa kiume na wa kike, basi fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili. Mwenyezi Mungu anawabainishia ili msipote; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

MWENYEZI MUNGU ANAWAPA FATWA JUU YA MKIWA

Aya 176

MAANA

Wanakuuliza fatwa; sema Mwenyezi Mungu anawapa fatwa juu ya mkiwa.

Mkiwa katika mrithi ni asiyekuwa mzazi au mtoto. Pia yule anayerithiwa na huyo anaitwa mkiwa, kwa vile hakurithiwa na mzazi au mtoto. Natija ni moja katika sifa zote mbili.

Neno hili limekuja katika Aya mbili katika Qur'an, katika Sura Annisa. Moja ni mwanzo wa Sura hii, ambapo makusudio yake huko ni ndugu wa marehemu wa upande wa mama tu, na Aya ya pili ni hii tulio nayo, ambapo makusudio yake hapa ni ndugu wa marehemu na dada zake wa upande wa baba na mama, au wa baba tu.

Iwapo mtu amekufa hali hana mtoto wa kiume au kike, kwa sababu neno Walad linatumiwa kwa aliyezaliwa (mtoto). Mwenyezi Mungu anasema katika kutumia neno walad: "**Mwenyezi Mungu hakujifanyia mtoto**" (23:91)

Na pia akiwa hana mmoja wa wazazi wawili, kama linavyofahamisha neno "ukiwa" kuongezea Hadith.

Na anaye ndugu wa kike, basi (dada huyo) atapata nusu ya alichokiacha. Makusudio ya ndugu wa kike ni ndugu baba mmoja mama mmoja, ikiwa hayuko basi ni wa baba mmoja tu. Ama ndugu wa kike wa upande wa mama tu, hukumu yake imekwisheshaezwa katika Aya 11 ya Sura hii.

Yaani, ikiwa yuko dada wa tumbo moja au wa upande baba tu hakuna mtoto wala mmoja wa wazazi wawili, basi dada atachukua nusu kama fungu lake na atachukua nusu ya pili kwa kurudishwa; yaani atachukua mali yote.

Hiyo ni kwa upande wa Shia. Ni sawa awe marehemu ana asaba (ami wa marehemu n.k) au la. Ama Sunni wanaitoa nusu iliyobaki kwa asaba akiwepo, kama hayupo basi atachukua mali yote. Tofauti baina ya Sunni na Shia ni kuwepo asaba tu. Maelezo zaidi yako kwenye vitabu vya Fiqh.

Naye atamrithi nduguye wa kike akiwa hana mtoto wa kike au wa kiume, wala mmoja wa wazazi wawili na atachukua mali yote kwa kurithi, kwa maafikiano ya madhehebu zote.

Wakiwa ni ndugu wa kike wawili basi watapata theluthi mbili za alichokiacha.

Yaani ndugu wa kike wa upande wa baba na mama au upande wa babatu. Yameafikiana madhehebu yote ya kiislamu kuwa hukumu ya dada wawili ndiyo ya wengi; Kwa hiyo maana hapa itakuwa wakiwa ni wawili na zaidi basi watapata theluthi mbili ya alichokiacha marehemu awe kaka au dada.

Na wakiwa ni ndugu wa kiume na wa kike, basi fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili.

Baada ya kubainisha fungu la ndugu wa kike peke yao, na fungu la dada wawili na zaidi wasiokuwa na kaka zao, amebainisha wakiwa pamoja ndugu wa kike na kiume kwamba wanaume watapa mara mbili zaidi ya wanawake.

Yamekwishatangulia maelezo kwa urefu na ufanuzi kuhusu mirathi ya binti na dada katika kufasiri Aya ya 11 ya Sura hii pamoja na kauli za Shia na Sunni na dalili zao.

TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

Sura Ya Tano: Al - Maidah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu
 ﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَوْفُوا بِالْعُهُودِ أُحِلَّتْ لَكُمْ بِهِمَةُ الْأَنْعَامِ إِلَّا مَا يُتَّلِّ عَلَيْكُمْ غَيْرُ مُحْلِّيٍ
 الصَّيْدُ وَأَنْتُمْ حُرُومٌ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا يُرِيدُ﴾

1. Enyi mliaoamini! Tekelezeni mapatano. Mmehalalishiwa wanyama wenye miguu mine, ila wale mnaotajiwa bila kuhalalishiwa mawindo mkiwa katika Ihramu. Hakika Mwenyezi Mungu anahukumu atakavyo.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُحْلِّو شَعَائِرَ اللَّهِ وَلَا الشَّهْرُ الْحُرَامُ وَلَا الْهَدْيَ وَلَا الْقَلَائِدَ وَلَا آمِنَ الْيَتَمَ حِلْمَرَامَ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِّنْ رَّبِّهِمْ وَرِضْوَانًا وَإِذَا حَلَّتُمْ فَاصْطَادُوا وَلَا يَجِدُونَكُمْ شَتَّانٌ قَوْمٌ أَنْ صَدُّوكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ أَنْ تَعْتَدُوا وَتَعَاوَذُوا عَلَى الْبَرِّ وَالثَّقَوْيِ وَلَا تَعَاوَذُوا عَلَى الْإِثْمِ وَالْعُدُوانِ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ﴾

2. Enyi mliaoamini! msivunje heshima ya alama za Mwenyezi Mungu wala ya mwezi mtakatifu, wala ya wanyama wa kuchinja, wala ya vigwe, wala ya wale wakusudiao kwenda kwenye nyumba tukufu kutafuta fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi.Na mkishatoka kwenye Ihramu, basi windeni. Wala kule kuwachukia watu waliowazulia kufika Msikiti mtukufu, kusiwapelekee kuwafanya jeuri, Na saidianeni katika wema na takua wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.

KWA JINA LA ALLAH MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU TEKELEZENI MAPATANO

Aya 1-2

MAANA

Aya za Qur'an huzungumzia itikadi, ibada, sharia, maadili, maongozi ya kidini na ya kidunia, hukumu na jihadi. Aya zizungumziazo sharia, ikiwamo ibada, huitwa Aya za hukumu. Nazo zinafikia kiasi cha 500.

Miongoni mwa Aya hizo ni hii isemayo: **Enyi mliaoamini! Tekelezeni mapatano.**

Jumla hii, pamoja na ufupi wake, ina manufaa makubwa. Kwani madhehebu yote yamekongamana kuwa ndio msingi na asili ya wajibu wa kutekeleza mapatano waliyopatana kwa kuridhiana, yakiwa masharti ya sharia yamekamilika, ambayo ni pamoja na kubaleghe na kuwa na akili kwa waliopatana.

Vile vile ustahiki wa kumiliki kilichofanyiwa mapatano na kutowajibisha ya halali kuwa haram na ya haram kuwa halali na mengineyo, ambayo yametajwa katika vitabu vya Fiqhi kama vile Fiqh Imam Jafar as-Sadiq J.3.

Mmehalalishiwa wanyama wenge miguu minne ambao ni ngamia, ng'ombe, kondoo na mbuzi, wa kufugwa au wa porini. Baada ya Mwenyezi Mungu kuhalalisha kuliwa wanyama hawa, amevua kwa kusema:

Ila wale mnaotajiw.

Na Mwenyezi Mungu Mtukufu ametutajia hapa aina mbili za wanyama:

Kwanza: ni ile aliyoashiria kwa kauli yake: Bila ya kuhalalisha mawindo mkiwa katika Hija.

Pili ni ile aliyoashiria katika Aya ya tatu: "Mheramishiwa mfu na damu." Ufafanuzi wake utakuja, inshallah.

Maana ya bila ya kuhalalisha mawindo mkiwa katika Hija, Ni kuwa wanyama ambao Mwenyezi Mungu ametuhalalishia kuwala ni wanyama wa kufugwa au wa porini ambao hatukuwawinda wakati wa Ihramu¹.

Ama wale tunaowawinda katika hali hii ni haramu kuliwa. Kwa sababu, kila akiwindacho mwenye kuhirimia haifai kukila; ni sawa awe ni katika wanyama wa kufuga au wa porini. Utakuja ufanuzi katika Tafsiri ya Aya 97 na ilio baada yake.

Enyi mliaoamini! Msivunje heshima ya alama za Mwenyezi Mungu.

Na alama zake Mwenyezi Mungu Mtukufu ni hukumu za dini yake, ambazo miongoni mwa zilizojitokeza zaidi ni ibada ya Hija. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ذَلِكَ وَمَنْ يُعَظِّمْ شَعَائِرَ اللَّهِ فَإِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ﴾

"Ndivyo hivyo! Na anayeziadhimisha alama za Mwenyezi Mungu, basi hilo ni katika takua ya moyo" (22:32)

Maana ya kukataza kuvunja miiko ya hukumu za dini ya Mwenyezi Mungu ni kutozipindua na kufanya kama tunavyotaka, **Wala ya mwezi mtakatifu.**

Yaani msipigane katika miezi mitukufu, Makusudio ya miezi mitukufu ni minne: Dhul-qaeda, Dhul-Hijja, Muhamram na Rajab².

Wala ya Wanyama wakuchinjwa kwenye nyumba ya Mwenyezi Mungu Mtukufu miongoni mwa Ngamia, Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo. Makusudio ni kuwa yejote asimtaaradhi mnyama kwa kumpora au kumzuia kufika kwenye nyumba tukufu.

Wala ya vigwe, yaani wala heshima ya wale waliofungwa vigwe. Walikuwa wakiwafunga wanyama vigwe ili wajulikane na wasitaaradhiwe na yejote. Wametajwa wenye vigwe baada ya kutaja wanyama wa kuchinja, pamoja na kuwa hao wanaofungwa vigwe ndio hao watakaochinjwa, kwa sababu ya kutilia umuhimu; kama vile kusema: "Angalieni sana Swala na Swala ya katikati" (2: 238)

Wala ya wale wakusudiao kwenda kwenye Nyumba tukufu kutafuta fadhila za Mwenyezi Mungu na radhi.

Yaani msimuuue yejote anayekusudia nyumba ya Mwenyezi Mungu; ni sawa awe amekusudia ibada au biashara.

Na mkishatoka kwenye Ihramu, basi windeni, kwani kuwinda ni haram katika hali ya Ihram na katika ardhi ya Al-Haram. Ikiwa mtu hayuko katika

1 Kuwa katika matendo ya Hija.

2 Mfungo pili, tatu, nne, na kumi.

Ihram wala hayuko katika ardhi ya Haram¹, basi kuwinda na kula windo ni halali. Neno basi windeni ni kuhalalisha sio kuamrisha, kwa sababu limeku baada ya makatazo.

Wala kule kuwachukia watu waliowazuilia kufika msikiti mtukufu, kusiwapelekee kupituka mipaka.

Katika mwaka wa sita Hijria, washirikina ndio waliokuwa wakitawala Makka na nyumba tukufu.

Mtume na sahaba zake wakataka kuzuru nyumba tukufu katika mwaka huo, lakini washirikina wakawazuia. Baadaye Makka na nyumba tukufu zikawa chini ya mamlaka ya Waislamu. Ikashuka Aya hii, zikiwa na maana kuwa haifai kwenu nyinyi Waislamu chuki ya washirikina kuwapelekea kuwazuia na nyumba tukufu, kwa kuwa waliwazuilia mwanzo. Hii ilikuwa kabla ya kushuka Aya:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنَّمَا الْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ احْرَامٍ هَذَا﴾

"Enyi mliaoamini! Hakika washirikina ni najisi kwa hivyo wasiukurubie Msikiti mtakatifu baada ya mwaka wao huu!!" (9:28)

Unaweza kuuliza: Mwenyezi Mungu si amesema kuwa:

﴿فَمَنْ اعْتَدَى عَلَيْكُمْ فَاعْتَدُوا عَلَيْهِ بِمِثْلِ مَا اعْتَدَى عَلَيْكُمْ﴾

"Wanaowachokoza nanyi pia wachokozeni kwa kadiri walivyowachokoza?" (2:194)

Jibu: Aya hii imeshuka kuhusu kisasi na kulipiziana katika mambo maalum; kama vile vita na kukatana viungo; yaani mwenye kupigana nanyi piganeni naye, na mwenye kumkata mkono wa mwingine naye akatwe, na mfano wa hayo. Ama mwenye kuzuia ibada ya Mwenyezi Mungu, biashara au kilimo, basi haijuzu kumlipizia hivyo bali atalipizwa kwa kitu kingine.

Kwa ufupi malipo ya mchokozi yanaweza kuwa ni kulipiza alivyofanya au kwa namna nyingine. Sehemu nyingi malipo yanakuwa ni ushindi wa haki sio kuadhibu.

MAPINDUZI NA KUPINGA MAPINDUZI

Na saidianeni katika wema na takua wala msisaidiane katika dhambi na uadui.

Miongoni mwa maneno yanayozunguka leo katika vinywa vya wasemaji na kalamu za waandishi ni mapinduzi na kupinga mapinduzi. Wakiwa na maana ya kuwa mapinduzi ni kuwasaidia wenye ikhlasi na kuwatetea dhidi ya ufisadi.

Na kupinga mapinduzi ni kuwasaidia wahaini na wasio wana mapinduzi katika kujaribu kuleta mageuzi. Dhahiri ya Aya inatupelekea kufuatishia kauli yake Mwenyezi Mungu: wala msisaidiane katika dhambi na uadui, kuwa ni kupinga mapinduzi ya kila heri na maendeleo.

﴿ حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ الْمَيْتَةُ وَالدَّمُ وَلَحْمُ الْخَنِزِيرِ وَمَا أَهَلَ لِغَيْرِ اللَّهِ بِهِ وَالْمُنْخَنِقَةُ وَالْمَوْقُوذَةُ وَالْمُنَّارِدَةُ وَالْتَّطِيحةُ وَمَا أَكَلَ السَّيْعُ إِلَّا مَا ذَكَرْتُمْ وَمَا ذِيَحَ عَلَى التُّصُّبِ وَأَنْ تَسْتَقْسِمُوا بِالْأَرَامِ ذُلِّكُمْ فِسْقُ الْيَوْمِ يَئِسَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ دِينِكُمْ فَلَا تَخْشُوْهُمْ وَأَخْشُوْنِ الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ مِّنْ﴾

1 Al-Kaaba na sehemu maalum inayoizunguka

دِينَكُمْ وَأَنْتَمْ عَلَيْكُمْ نِعْمَتٌ وَرَضِيَ اللَّهُ عَنْكُمْ لَكُمُ الْإِسْلَامُ دِينًا فَمَنِ اضْطُرَّ فِي تَحْمِصَةٍ غَيْرَ مُتَجَانِفٍ لِأَئُمُّ قَبَائِلَ اللَّهُ عَفُورٌ رَّحِيمٌ

3. Mmeharamishiwa nyamafu na damu na nyama ya nguruwe, na aliyechinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na aliyekufa kwa kunyongeka, na aliyekufa kwa kupigwa, na aliyeanguka, na aliyepigwa pembe, na aliyeliwa na mnyama ila mliowachinja, na aliyechinjiwa mizimu. Na kuagulia kwa mburuga. Hayo yote ni ufasiki. Leo waliokufuru wamekata tamaa katika dini yenu, basi msiwaogope na mniogope mimi. Leo nimewakamilishia dini yenu na kuwatimizia neema yangu na nimewapendelea Uislamu kuwa dini. Basi aliyefikwa na dharura bila kuelekea kwenye dhambi. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye maghfira mwenye kurehemu.

MMEHARAMISHIWA MFU

Aya ya 3

MAANA

Vyakula vyote na vinywaji vyote ni halali ila ambavyo imepatikana nukuu ya kuharamishiwa kwa umahususi; kama vile nyamafu na kadhalika, au kwa ujumla; kama vile vitu vinavyodhuru, vikiwemo vitu vichafu. Mwenyezi Mungu anasema:

"Enyi watu kulenii vilivyomo katika ardhi halali na vizuri" (2:168)

Yametangulia maelezo katika Aya ya kwanza katika kauli yake Mwenyezi Mungu ila wale mnaotajiwa. Na Mwenyezi Mungu anatutajia aina mbili, ambapo aina ya kwanza ametutajia katika Aya ya kwanza, aina ya pili ni hii anayotutajia katika Aya hii, navyo ni kumi:

1. **Nyamafu:** Ni kila mnyama au ndege aliyekufa bila ya kuchinjwa kisheria. Kuchinja huko kunatofautiana kulingana na wanyama: samaki kuchinjwa kwake ni kutolewa hai katika maji; kwa nzige ni kwa kumshika akiwa hai. Vilevile kwa aliye tumboni ni kwa kuchinjwa mama yake. Kwa windo kuchinja kwake ni kwa kutumia mbwa aliyefundishwa, upanga, mkuki, mshale au ala yoyote kali. Na kuchinja mnyama kwa kuelekezwa Qibla na kukata mishipa minne pamoja na kutaja jina la Mwenyezi Mungu. Ufafanuzi umo katika vitabu vya fiqh, kama vile Fiqhul Imam Jafar as-Sadiq.

2. **Damu:** inayotoka kwa nguvu na kupambanuka na nyama. Kwa sababu ile ilio katika nyama inasamehewa; vile vile inasamehewa damu iliyogeuka nyama ikawa ini, kwa madhehebu yote; na ni haramu ikiwa ni wengu kwa Shia.

3. **Nyama ya nguruwe:** Ni haramu kwa Waislamu wote.

4. **Aliyechinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.** Washirikina walikuwa wakichinja kwa ajili ya masanamu na kuyataja majina ya Lata na Uzza. Yamekwishatangulia maelezo kuhusu hayo katika Tasfiri (2:173).

5. **Aliyekufa kwa kunyongeka:** Ni yule anayekufa kwa kunyongwa kwa kamba, mkono au kuingizwa kwenye kitu cha kubana nk.

6. **Aliyekufa kwa kupigwa kwa fimbo au kitu chochote.**

7. **Aliyekufa kwa kuanguka:** Ni yule aliyeporomoka kutoka juu akafa.

8. **Aliyekufa kwa kupigwa pembe:** Ni yule aliyepigwa pembe na mwenzake mpaka akafa.

9. **Aliyeliwa na mnyama,** lakini Mwenyezi Mungu ametoa katika aina hii akiwa hai. Huyo atakuwa halali kuliwa kwa kuchinjwa kisharia. Hii ndio maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu ila mliowachinja. Katika Hadith imeelezwa kuwa kwa uchache wa kuwahi mchinjaji ni kumwahi akitingisha sikio lake, mkia wake au kupepesa jicho lake.

10. **Aliyechinjiwa mizimu.** Mwenye Kitabu Attashiu-lilumittanzil anasema: Mizimu ni mawe ambayo wakati wa ujahiliya walikuwa wakiyatkuza na kuyachinjia na wala sio masanamu. Kwa sababu masanamu ni yale yenze Sura, na mizimu haina Sura.

Ilivyo ni kwamba uharamu wa vyakula sio aina hizi kumi tu zilizotajwa na Aya tukufu, bali kuna aina nyingine za vyakula vilivyo haramu; kama vile mbwa, wanyama wanaoshambulia, ndege walao nyama; kama vile Kozi na Tai. Pia baadhi ya aina za samaki na vinginevyo viliivytajwa na Hadith na kukongamana mafakihi. Wala hakuna tofauti baina ya yaliyoelezwa na Qur'an na yale yaliyoelezwa na Hadith.

﴿وَمَا آتَيْتُ الرَّسُولَ فَخُدُودًا وَمَا نَهَا كُمْ عَنْهُ فَإِنْ تَهْوَى﴾

"Na anachowapa Mtume kichukueni na anachowakataza kiacheni" (59:7).

Sio mbali kuwa kuhusisha kutaja aina hizi kumi ni kwa kunasibiana na kauli yake Mwenyezi Mungu, "Mmehalalishiwa wanyama."

Baada ya Mwenyezi Mungu kutaja aina hizo, ameunganisha kwa kusema:

Na kuagulia kwa mburuga.

Wakati wa Ujahiliya mtu akitaka kufanya jambo muhimu huchukua mbao tatu: moja huiandika 'Ameniamuru Mola wangu'; Ya pili huiandika 'Amenikataza Mola Wangu'; na ya tatu haiandiki kitu. Kisha huzifunika na kitu na kuingiza mkono wake ili atoe mojawapo. Ikitokea amri hufanya, ikitokea katazo huacha na ikitokea tupu hurudia, mpaka itokee amri au katazo.

Hayo yote ni ufasiki.

Yaani yote hayo yaliyotajwa. Hakuna maana ya kutofautiana wafasiri kuhusu neno 'Hayo' kuwa je ni kuhusisha hayo ya mburuga au yote, maadamu hukumu ya yote ni moja - ufasiki, yaani dhambi kubwa.

Leo waliokufuru wamekata tamaa katika dini yenu, basi msiwaogope na mniogope mimi.

Wafasiri wengi wamesema kuwa makusudio ya leo katika Aya ni siku ile iliyoshuka Aya hiyo. Siku ya Hija ya kuaga (Hijjatul-Wadai) katika mwaka wa kumi Hijriya.

Mwenye Majmaul-bayan anasema: Leo hapa ina maana ya sasa, kama mtu akisema leo umekua, akiwa na maana ya sasa umekua.

Vyovoyote iwavyo maana ya Aya ni kuwa makafiri wamekata tamaa ya kuwa Uislamu utakwisha au kuharibika, baada ya kumakinika katika nyoyo za wafuasi wake na kuanza kuenea siku baada ya siku. Kwa hiyo enyi Waislamu msiwaogope makafiri bali muogopeni Mwenyezi Mungu peke yake. Amesema kweli Mwenyezi Mungu katika kila anayoyasema:

﴿يُرِيدُونَ أَن يُظْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَيَأْبَى اللَّهُ إِلَّا أَن يُمَّ تُورَةً وَلَوْ كَرَةً الْكَافِرُونَ ﴾٣٦
هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينُ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الَّذِينَ كُلَّهُ وَلَوْ كَرَةً الْمُشْرِكُونَ﴾

"Wanataka kuzima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, lakini Mwenyezi Mungu anakataa isipokuwa kuitimiza nuru yake, wajapochukia makafiri. Yeye ndiye aliyemleta Mtume wake kwa uongofu na dini ya haki ili ajalie kushinda dini zote ijapokuwa watachukia washirikina" (9:32-33).

Itakuwa ni jambo la faida kwa mnasaba huu tudokoze maneo kutoka Kitabu Al-Islam Fil-qarnil-Ishirin cha Aqad, amesema: "Uislamu hapo mwanzoni hakuwa na nguvu, lakini ukawa na nguvu imara, baada ya mamia ya miaka. Uimara huu na nguvu ya kiislamu katika hali ya udhaifu ni ya kustaajabisha, lakini uimara wake hivi sasa baada ya kupita karne ishirini ni wa kustaajabisha zaidi. Kwa sababu Uislamu hauna kinga yoyote wala mali, silaha, elimu au maarifa, Bali hata watu wake hawana maafikiano ya kujikinga.

Nguvu ya itikadi ya Kiislamu imeendelea katika pembe zote za ulimwengu ikiwa mbali na vita vya kidola na siasa zake au kuwa katika vyeo. Katika Afrika leo kuna mamilioni ya Waislamu, ambao hawana vyeo vyovoyote katika nchi au katika siasa. Hali kama hiyo iko huko Sumatra na Java, na inakurubia hali hiyo katika Pakistan na pengine China na sehemu inayopakana nayo"

KUKAMILISHWA DINI NA KUTIMIZWA NEEMA

Leo nimewakamilishia dini yenu na kuwatimizia neema yangu na nimewapendelea Uislamu kuwa ndiyo dini.

Shia na Sunni wengi wametofautiana kuhusu Aya hii: Tutaelezea kauli za pande zote mbili, kama wanakili tu, sio waungaji mkono wala wakanushaji na kumwachia msomaji na akili yake aamue mwenyewe. Sunni au wengi wao wamesema kuwa makusudio ya Aya ni kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewakamilishia Waislamu dini yao kwa kushinda kwake na kujitokeza kwake juu ya dini zote pamoja na kupigwa vita. Na ameitimiza neema yake kwa kubainisha itikadi yake na sharia yake kuanzia shina hadi matawi na kubainisha yote wanayoyahitaja katika dini yao na dunia yao.

﴿مَا فَرَظَنَا فِي الْكِتَابِ مِنْ شَيْءٍ﴾

"Hatukupunguza Kitabuni kitu chochote" (6:38)

Shia wamesema kuwa itawezekana kuifasiri Aya hii, kwa maana hayo, ikiwa hatutakukutanisha na tukio lake na kubainisha makusudio yake. Kwani Aya nyingi zinafasiriwa na tukio lililoambatana nalo na muda wa kushuka kwake. Kwa mfano kama ile Aya isemayo kumwambia Mtume wake mtukufu:

﴿وَتَحْشِي النَّاسَ وَاللَّهُ أَحَقُّ أَن تَحْشِيَهُ﴾

"Na ukachelea watu na hali Mwenyezi Mungu ndiye mwenye haki zaidi ya kumchelea." (33:37)

Lau kama Aya hii tutaiepusha na kisa cha Zaid bin Haritha na tukachukua dhahiri yake, basi maana yatakuwa ni kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) anaathirika na kuwaridhisha viumbe kuliko

muumba wake; jambao ambalo haliwezekani kwa yule ambaye Mwenyezi Mungu amemchagua kuchukua wahyi wake na ujumbe wake.

Kisha wakaendelea kusema Shia kuwa Aya hii imekutanishwa na tukio lake mahsusini linalofasiri na kubainisha makusudio yake. Hilo wameliTafsir tolea dalili kama ifuatavyo:-

Kwanza: Wameafikiana wanachuoni wa Kishia na Kisunni, wafasiri na wana historia, kuwa Aya za Sura ya Maida zote zimeshuka Madina lakini Aya hii: (Leo nimewakamilishia dini yenu), imeshuka Makka mnamo mwaka wa 10H, mwaka ambao Mtume Muhammad (**s.a.w.w**) alihiji Hijja ya mwisho. Kwani alielekea kwenye rehema ya Mola (kufariki) katika mwezi wa Rabiul-Awwal (mfungo sita) mwaka wa 11 H.

Pili: Baada ya Mtume kumaliza Hijja yake hii, alielekea Madina. Alipofika Ghadir Khum - sehemu katika Juhfa penye njia nyingi - aliamrisha mnadi Swala anadi, watu wakakusanyika; na kabla ya kutawanyika kushika njia zao, akawahutubia, na mionganini mwa maneno aliyosema ni: "Hakika Mwenyezi Mungu ni mtawala wangu na mimi ni mtawala wa waumini na mimi ni bora kwao kuliko nafsi zao. Basi ambaye mimi ni mtawala wake na Ali ni mtawala wake. "Akasema hivyo mara tatu; riwaya nyingine zinasema ni mara nne, Kisha akaendelea kusema "Ewe Mola wangu! Mpende anayempenda na mhasimu anayemhasimu, mdhalilishe anayemdhalilisha, ipeleke haki pamoja naye popote atakapokuwa. Haya basi aliyepo na amwambie asiyekuwepo"

Sunni hawaikanushi Hadith hii baada ya kuzidi kiwango cha Mutawatir¹, na wengi katika Maimamu wao na wanavyuoni wao wameinukuu akiwamo Imam Ahmad Ibn Hanbal katika Musnadi yake, Nasai katika Khasais, Hakim katika Mustadrak, Khawarizami katika Manaqib, Ibn Abdu Rabbih katika Istia'b na Asqalani katika Iswaba. Vilevile Tirmidhi, Dhahabi, Ibn Hajar na wengineo. Lakini wengi wao wamefasiri neno Wilaya kwa maana ya mapenzi badala ya utawala na kwamba makusudio ya kauli ya Mtume (**s.a.w.w**) ambaye mimi ni mtawala wake, ni ambaye ananipenda na ampende Ali.

Shia wamejibu tafsiri hii, kuwa kauli ya Mtume inafahamisha waziwazi kwamba utawala ulithibiti kwa Mtume juu ya waumini ndio huo ulithibiti kwa Ali ^(a.s) bila ya kuzidi au kupungua. Na utawala huu ndio utawala wa kidini, hata kama neno Wilaya lina maana elfu.

Kwa hiyo basi maana ya Aya ni kwamba Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameikamilisha dini hii leo kwa kutoa kauli wazi kuwa Ali ni Khalifa.

Unaweza kuuliza: Kukamilisha dini kwa huidhirisha juu ya dini nyingine na kubainisha hukumu yake kwa ukamilifu, kama wasemavyo Sunni, ni kauli wazi isiyohitaji tafsiri. Ama kukamilisha dini kwa kumweka

1 Shia wameinukuu Hadith hii kutoka katika rejea kadha za Sunni, Wanavyuoni wao wametunga vitabu mahsusini, wa mwisho wao ni Sheikh Amini katika wanachuoni wa mji mtukufu wa Najaf wakati huu. Ametunga Kitabu alichokiita Al- Ghadir, kikiwa na Juzu 12 chenye kurasa karibu elfu tano (5000) ametaja wapokezi wa Hadiith: Sahaba 120, Taabin 84, Maimamu na wahifadhi wa Hadith 360, akiwemo Hanafi, Shafi na wengineo. Yote hayo ameyanukuu kutoka vitabu vyta kisunni vinavyouzwa madukani Iraq, Iran, Lebanon na kwingineko.

Ali kuwa Khalifa ni kauli ambayo hapana budi kuweko na tafsiri na ufanuzi, basi Shia wanaifasiri kwa namna gani?

Katika kufasiri hilo, Shia wamesema: Kukamilika haki hakutimii ila kwa kupatikana utawala wa sharia na utawala wa utekelezaji kwa pamoja, mmoja peke yake hautoshi ikiwa haukuungwa na mwingine.

Utekelezaji ulikuwa mikononi mwa Mtume Mtukufu (**s.a.w.w**), Hapo maadui wa Uislamu wakadhani kwamba utawala wa utekelezaji utakwisha kwa kuondoka Mtume.

Na ukiondoka ndio Uislamu umeondoka. Ndipo Mtume akamweka Ali ahifadhi sharia baada yake na aisimamishe dini, kama alivyoisimamisha yeye. Kwa hiyo ikawa makafiri hawana tumaini lolote la kwisha Uislamu au kudhoofika.

Basi aliyefikwa na dharura bila kuelekea kwenye dhambi. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye kusameha mwenye kurehemu.

Imekwishapita tafsiri ya Aya hii katika (2:173) kifungu mwenye dharura na hukumu yake.

﴿يَسْأَلُونَكَ مَاذَا أَحِلَّ لَهُمْ قُلْ أَحِلَّ لَكُمُ الظَّبَابُ وَمَا عَلِمْتُمْ مِنَ الْجَوَارِحِ مُكَلِّبِينَ تَعْلَمُونَهُنَّ مِمَّا عَلِمَكُمُ اللَّهُ فَكَلُّوا مِمَّا أَمْسَكْنَ عَلَيْكُمْ وَإِذْ كُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهِ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ﴾

4. Wanakuuliza wamehalalishiwa nini. Sema mmehalalishiwa vilivyo vizuri. Na mllichowafunza mbwa mionganini mwa wanyama wa kuwinda, mnawafunza kama alivyowafunza Mwenyezi Mungu. Basi kuleni walichowakamatia na mkisomee jina la Mwenyezi Mungu. Na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ni mwepesi wa kuhisabu.

NA MLICHOWAFUNZA WANYAMAWA MAWINDO

Aya 4

MAANA

Wanakuuliza wamehalalishiwa nini. Sema mmehalalishiwa vilivyo vizuri.

Kizuri ni kinyume cha kibaya. Vibaya ni vilivyoelezwa waziwazi na kuhuishwa na sharia kuhusu uharamu wake, kama vile nyamafu, nyama ya nguruwe; au vilivyoelezwa kiujumla, ambavyo kwa namna moja au nyingine vina madhara na ufisadi.

Jumla hii Mwenyezi Mungu ameitaja kwa tamko au kwa maana katika sehemu 15 kwenye Kitabu chake kitukufu.

Na mllichowafunza mbwa mionganini mwa wanyama wa kuwinda, mnaowafunza kama alivyowafunza Mwenyezi Mungu. Basi kuleni walichowakamatia na mkisomee jina la Mwenyezi Mungu.

Madhehebu yote yameafikiana kwa kauli moja kwamba windo la mbwa ni halali kuliwa, likifa bila ya kuchinjwa, kwa masharti yafuatayo:

1. Kuwa mbwa amefundishwa - akiamrishwa na bwana wake anashika amri na akikatazwa anakatazika. Hiyo ndiyo maana ya kauli yake Mwenyezi Mungu: "**Mnawafunza kama alivyowafunza Mwenyezi Mungu**".

2. Mwindaji awe amemshakiza mbwa kuwinda. Lau atakwenda mwenyewe na akaja na windo, si halali kuliwa.

3. Mwindaji awe Mwislamu, kwa upande wa Shia.
4. Asome Bismillah wakati wa kumshakiza mbwa, aseme: Nenda kwa jina la Mwenyezi Mungu na mfano wa hayo.
5. Mbwa alikute windo liko hai, na life kwa kujeruhiwa naye. Lau akilikuta limekufa basi si halali, au akilikuta hai, lakini likafa sio kwa kujeruhiwa basi si halali.

Hata hivyo wametofautiana kuhusu kuwinda kwa kutumia mnyama mwagine, asiyekuwa mbwa, kama vile: Chui, Kipanga nk. Shia wamesema, si halali na wengineo wamesema ni halali. Shia wametoa dalili kuwa neno 'mbwa mionganoni mwa wanyama wa kuwinda' katika Aya, linahusika na mbwa tu.

﴿الْيَوْمَ أُحِلَّ لَكُمُ الطَّيَّبَاتُ وَطَعَامُ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حَلٌّ لَكُمْ وَطَعَامُكُمْ حَلٌّ لَهُمْ وَالْمُحْسَنَاتُ مِنَ الْمُؤْمِنَاتِ وَالْمُحْسَنَاتُ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ إِذَا آتَيْتُمُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ مُخْصِسِينَ غَيْرَ مُسَافِحِينَ وَلَا مُتَّخِذِي أَخْدَاءِ إِنِّي وَمَنْ يَكْفُرُ بِالْإِيمَانِ فَقَدْ حَبَطَ عَمَلُهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الظَّالِمِينَ﴾

5. Leo mmehalalishiwa vilivyo vizuri na chakula cha wale waliopewa Kitabu ni halali kwenu, na chakula chenu ni halali kwao; na wanawake wenye kujichunga katika waumini na wanawake wenye kujichunga katika wale waliopewa Kitabu kabla yenu mtakapowapa mahari yao mkafunga ndoa bila ya kufanya uzinzi wala kuwafanya mahawara. Na mwenye kukataa kuamini hakika amali zake zimepomoka na yeze huko Akhera atakuwa mionganoni mwa wenye kupata hasara.

UTWAHARAWAWATU WA KITABU

Aya ya 5

LUGHA

Neno ihswan lina maana nne: Uislamu, kuolewa, uhuru na kujichunga na zina ambako ndiko kulikokusudiwa.

MAANA

Leo mmehalalishiwa vilivyo vizuri na chakula cha wale waliopewa Kitabu ni halali kwenu na chakula chao ni halali kwao.

Wametofautiana Sunni na Shia katika maana ya makusudio ya chakula cha watu wa Kitabu ambao ni Mayahudi na Manaswara (Wakristo). Sunni wamesema makusudio ni walichokichinja. Haya yamenukuliwa kwao kutoka kwa mwenye Tafsir Al-Manar ninamnukuu:

"Wamefasiri kundi kubwa kuwa chakula hapa ni kwa maana ya walichokichinja, kwa sababu vyakula vinginevyo tayari ni halali kwa asili yake."

Mafakihi wengi wa Kishia wamesema kuwa watu wa Kitabu ni najisi wakaharamisha chakula chao, kinywaji chao na hata mkate na maji waliyo yagusa; na wakafasiri chakula katika Aya kwa maana ya nafaka (vyakula nya tembe tembe).

Ama sisi tunaona kuwa watu wa Kitabu ni twahara¹. Tumeyafafanua haya pamoja na dalili katika Kitabu Fiqhul Imam Jafar as-Sadiq J.1. Na Marja'a wakubwa wengi wamekwenda na rai hii; akiwemo Sayyid Hakim na Sayyid Khui.

Ama kauli ya mwenye kusema kuwa mtu wa Kitabu ni mwenye kunajisika na wala si najisi, hiyo ni kucheza na maneno. Kwa sababu katika sharia vitu viko mafungu mawili Twahara na Najisi, hakuna cha tatu. Ni kweli kuwa kitu twahara kinaweza kuzukiwa na najisi kisha ikaondoka kwa kutwaharishwa; lau najisi inakuwa nacho basi kitakuwa ni najisi, sio chenye kunajisika.

Ama kufasiri chakula kwa kuhusisha nafaka ni umbali wa mbali kabisa na fasihi ya Qur'an na balagha yake. Imetumia neno chakula kwa windo la baharini wala hakuna nafaka baharini. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿أَحَلَّ لَكُمْ صَيْدُ الْبَحْرِ وَطَعَامُهُ﴾

"Mmehalalishiwa kuvua baharini na chakula chake," (5:96)

Pia ametumia neno hilo katika maji, ambapo maji na nafaka ni tofauti. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿فَمَنْ شَرِبَ مِنْهُ فَلَيْسَ مِنِّي وَمَنْ لَمْ يَطْعَمْهُ فَإِنَّهُ مِنِّي﴾

"Basi atakayekunyuwa humo si pamoja nami, na asiyekunyuwa atakuwa pamoja nami" (2:249)

Neno asiyekunyuwa hapo limetokana na twaam chakula. Vilevile amelitumia katika vyakula mbalimbali, Mwenyezi Mungu anasema: ".Na mmapokwisha kula tawanyikeni" (33:53)

Je, kuna yejote atakayeweza kuitisha tafsiri yake kwa maana ya mkila shairi tawanyikeni? Kama atapitisha mfano wa tafisiri hii, basi itakuwa ni tafsir ya aina gani hiyo? Bali hata Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametumia chakula kuhusu nyama; akasema:

﴿قُلْ لَا أَجِدُ فِي مَا أُوحِيَ إِلَيَّ مُحَرَّماً عَلَىٰ طَاعِمٍ يَطْعَمُهُ إِلَّا أَنْ يَكُونَ مَيْتَةً أَوْ ذَمَّاً مَسْفُوحًا أَوْ لَحْمَ حَنَزِيرٍ﴾

"Sema: Sioni katika yale niliyopewa wahyi kitu kilichoharamishwa kwa mlaji kukila isipokuwa nyamafu au damu inayomwagika au nyama ya nguruwe". (6:145)

Kwa ajili hiyo basi tunasema kuwa chinjo la watu wa Kitabu ni halali ikiwa itajulikana kuwa masharti yamekamilika - kuelekea Qibla, kusoma Bismillahi na kukata mishipa minne. Hii ndiyo tofauti baina ya chinjo la mtu wa Kitabu na Mwislam, ambapo kwa mtu wa Kitabu haliwi halali mpaka ijulikane kuwa masharti yalikamilika.

Lakini kwa Mwislamu litakuwa halali bila ya kuweko haja ya kujuu kukamilika masharti, isipokuwa kama itajulikana kuwa masharti hayakukamilika.

Tumeyafafanua haya pamoja na dalili katika Kitabu Fiqhul Imam Jafar as- Sadiq J 4.

1 Hatimaye mwanachuoni mkubwa wa tifa la Kiislamu la Kishia Sayyid Al-Hakim ametoa fatua kuwa ni twahara.

Kuna riwaya sahihi kutoka kwa Ahlul Bait kuhusu jambo hili, akazitumia shahidi wa pili, Saduq, Ibn Abu Aqil na Ibn Al-Junaid. Mwenye Majmaulbayan amesema katika kufasiri Aya hii: "Wafasiri wengi na mafakihi wengi wamesema kuwa makusudio ya chakula katika Aya ni chinjo la watu wa Kitabu na ni kauli waliyokwenda nayo jamaa katika watu wetu" yaani wanachuoni wa Kishia wanaotegemewa kwa kauli zao.

Na wanawake wanaojichunga katika waumini na wanawake wanaojichunga katika wale waliopewa Kitabu kabla yenu mtakapowapa mahari yao mkafunga ndoa, bila ya kufanya uzinzi wala kuwafanya mahawara.

Makusudio ya uzinzi ni zina ya dhahiri na kufanya uhawara ni zina ya siri siri. Imeshartiwa mahari kwa kutokuzini kwa kutambulisha kwamba anachotoa mwanamume kumpa mwanamke ni lazima iwe ni mahari ya ndoa ya sharia sio hongo ya zina. Maana ni kwamba Mwenyezi Mungu amehalalisha kuwaoa wanawake wanaojistahi katika Waislamu na katika watu wa Kitabu. Na kwamba mwenye kuwaoa ni lazima awape mahari ya sharia kiasi cha mali iliyoafikianwa, sio malipo ya uzinzi.

Wameafikiana mafakihi wa madhehebu yote kwamba si halali kwa Mwislamu kumuoa asiyekuwa na dini kabisa wala wanaoabudu mizimu na moto. Wametofautiana katika ndoa ya mwenye Kitabu, yaani Wakristo na Mayahudi. Madhehebu mane ya Kisunni wamesema; Inajuzu kumuoa na wakatolea dalili kwa Aya hii. Wametofautiana mafakihi wa Kishia baina ya kujuzu na kutojuzu na kutofautisha baina ya ndoa ya daima na ya muda; baadhi wakajuzisha ya muda na kuzuia ya daima.

Sisi tuko pamoja na wasemao kujuzu bila ya chochote kwa kutegemea haya yafuatayo:-

Kwanza: Dalili zihalalishazo ndoa kwa ujumla.

Pili: Kauli yake Mwenyezi Mungu: "Na wanawake wanaojichunga katika wale waliopewa Kitabu." Tatu: Riwaya nyingi kutoka kwa Ahlu bait ^(a.s) na kutajwa na mwenye Wasail na Jawahir na kuzisifu kwa Mustafidha, yaani zilizofikilia wingi wa kukurubia kuwa Mutawatir, Tumezinukuu baadhi yake katika Fiqh Imam Jafar as-Sadiq.

Unaweza kuuliza: utasema nini kuhusu kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Wala msiwaoe washirikina mpaka waamini" (2:221)

na vile vile kauli yake Mwenyezi Mungu: "**Wala msifungamane na makafiri katika mshikamano.**" (60:10)

Jibu: washirikina sio watu wa Kitabu kwa dalili ya kuunganishwa katika Aya isemayo:

﴿لَمْ يَكُنِ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ وَالْمُشْرِكِينَ مُنْفَكِّينَ حَتَّىٰ تَأْتِيهِمُ الْبِيِّنَةُ﴾

"Hawakuwa wale ambao wamekufuru katika watu wa Kitabu na washirikina ni wenyewe kuachana na waliyonayo mpaka iwjajie hoja." (98:1)

Ama kauli yake "msifungamane na makafiri katika mshikamano" haiko wazi kuwa inahu ndoa; Kwa sababu mshikamano, kama unavyofumbiwa, ndoa vile vite hufumbiwa isiyokuwa ndoa. Mwenye Masalik anasema: "Aya haiko wazi katika makusudio ya ndoa wala katika makusudio yaliyo kijumla zaidi ya hayo."

Na mwenye kukataa kuamini hakika amali zake zimepomoka na yeze huko Akhera atakuwa mionganoni mwa wenyewe hasara.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutaja sehemu ndogo ya hukumu zake, halali yake na haramu yake anasema: Mwenye kusikia akatii basi yeye ni Mumin wa kweli, amali yake itakuwa yenyε kukubaliwa na malipo yake na thawabu zake ni juu yangu.

Na atakayezikanusha hukumu zangu na sharia basi yeye ni kafiri mwenye kupata hasara Kwa hiyo makusudio ya imani hapa ni zile zile hukumu ambazo ni wajibu kuziamini.

Hiyo ni katika mlango wa kufanya tendo kuwa ndio linatendwa; kama kusema kula kwa maana ya chakula. Kuhusu kupomoka tumekuzungumzia kwa ufanuzi zaidi katika (2:217)

TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا قُمْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ فَاغْسِلُوا وُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ إِلَى الْمَرَافِقِ وَامْسَحُوا بِرُءُوسَكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ إِلَى الْكَعْبَيْنِ وَإِنْ كُنْتُمْ جُبَابًا فَأَطْهِرُوهَا وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَى أَوْ عَلَى سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِنْكُمْ مِنَ الْغَائِطِ أَوْ لَا مَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجْدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيْبًا فَامْسَحُوا بِوُجُوهَكُمْ وَأَيْدِيَكُمْ مِنْهُ مَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيَجْعَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ حَرَجٍ وَلَا كِنْ يُرِيدُ لِيَطْهِرُكُمْ وَلَيَتَمَّ نِعْمَتُهُ عَلَيْكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ﴾

6. Enyi mliaoamini! Mnaposimama kwa ajili ya Swala, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka vifundoni, na mpake vichwa vyenu na miguu yenu mpaka vifundoni. Na mkiwa na janaba basi ogeni, na mkiwa wagonjwa au mumo safarini au akawa mmoja wenu ametoka chooni au mkagusana na wanawake, kisha msipate maji, basi tayamamuni na mchanga ulio twahara, mpake nyuso zenu na mikono yenu. Mwenyezi Mungu hapendi kuwatia katika taabu lakini anataka kuwatakasa na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru.

﴿وَإِذْ كُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَمِنَّا فَلَمْ سَمِعُنَا وَأَطْعَنُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِدَارِ الصُّدُورِ﴾

7. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu na ahadi yake aliyoifungamanisha nanyi mliposema: Tumesikia na tumetii Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa yaliyomo vifuani.

UDHU NA TAYAMMAM

Aya 6 - 7

IRABU

Herufi Ba katika neno Biruu, usikum imesemekana ni ya kuzidi, ikasemekana ni ya kuambatana na ikasemekana ni ya kufanya baadhi. Ufanuzi utakuja katika kifungu cha maana.

MAANA

Enyi mliaoamini! Mnaposimama kwa ajili ya Swala, yaani mkitaka kuswali.

Basi osheni nyuso zenu

Hakuna tofauti katika hilo, isipokuwa kwamba Shia wamesema ni wajibu kuanzia juu na haifai kufanya kinyume. Wengine wamesema inafaa namna yoyote ingawaje kuanzia juu ni bora.

Na mikono yenu mpaka vifundoni

Vilevile hakuna tofauti isipokuwa Shia wamejibisha kuanza vifundoni na kutanguliza mkono wa kulia. Sunni wakasema kuwa inafaa kuosha namna yoyote, ingawaje kuanzia vifundoni na kutanguliza kuume ni bora.

Unaweza kuuliza: Sunni na Shia wote wamekhaliwu dhahiri ya Aya, kwa sababu vifundo inapasa iwe ni mwishilio wa kuosha kwa sababu ya herufi ilaa (mpaka) ambapo Sunni hawaliwajibishi hilo na Shia hawaliruhusu hilo. Je kuna Taawil gani?

Wengi wamejibu kuwa herufi ilaa hapa ina maana ya mfano wa kauli yake Mwenyezi Mungu: "**Na awazidishie nguvu mpaka kwenye nguvu zenu.**" (11:52)

Yaani pamoja na nguvu zenu. Tuonavyo sisi ni kuwa kuwekea mpaka katika Aya ni kuelezea sehemu za kiungo kinachooshwa ambacho ni mkono bila ya kuangalia namna ya kuosha - kuanzia na kuishilia, sawa na mtu anavyosema: Nimekuuzia ardhi kuanzia hapa mpaka huko. Au kata mawaridi ya bustani kuanzia hapa mpaka huko.

Akiwa na maana ya kuelezea kiwango na kiasi sio kubainisha namna na hali.

Na mpake vichwa vyenu.

Hanbal wamesema ni wajibu kupaka kichwa na masikio mawili, na kupaka kunaweza kutoshelezwa na kuosha kwa sharti ya kuitisha mkono kichwani. Malik wakasema ni wajibu kupaka kichwa chote isipokuwa masikio.

Hanafi wakasema ni wajibu kupaka robo ya kichwa; na inatosheleza kukivika kichwa majini au kukimiminia maji. Shafi wakasema ni wajibu kupaka baadhi ya kichwa ijapokuwa ni kidogo; Inatosha kuosha au kunyunyiza.

Shia Imamia wakasema ni wajibu kupaka sehemu ya mbele ya kichwa. Inatosheleza kwa uchache inavyokubalika jina la kupaka; wala haijuzu kuosha au kunyunyiza. Kwa hiyo, maana ya kuwa 'ba' ni kuambatana, ni ya kauli mbili za mwanzo; na kuwa 'ba' ni ya kufanya baadhi, ni ya kauli za mwisho.

Na miguu yenu mpaka vifundoni.

Kisomo (qiraa) cha miguu, kimekuja mara mbili: Kwa Nasb (Arjula) na kingine kwa Khafdh (Arjuli). Sunni wamesema ni wajibu kuosha miguu kwa vile imeungana na mikono kutokana na visomo vyote viwili cha kwanza kiko wazi kwamba inaungana kitamko na mahali. Ama kwa kisomo cha (Khafdh) ni kwa ujirani na kufuata; yaani kwa vile neno Ruusi (Vichwa) lina khafdh basi na jirani yake naye akapata khafdh; sawa na wasemavyo waarabu 'Juhru Dhwabbin Kharibin' ingawaje Kharibin ni wajibu isomewe kwa (raf_u) kwa sababu ni sifa ya Juhr, na wala sio sifa ya dhabbin, lakini imesomwa kwa Khafdh kwa sababu ya ujirani.

Shia wamesema ni wajibu kupaka miguu na wala sio kuosha kwa sababu neno miguu linaungana na vichwa. Kwa kisomo cha Khafdh ni wazi. Ama kwa kisomo cha Nasb¹ ni kuungana na mahali pa neno ruus (vichwa) ambapo ni pa Nasb. Kwa sababu kila kilicho majruri kitamko ni mansub ki mahali.

Kisha Shia wakaendelea kusema: Kuunganisha miguu kwenye mikono hakujuzu kutokana na mambo mawili: Kwanza ni kinyume cha ufasaha kwa sababu ya kuwako kitenganishi baina ya mikono na miguu. Kitenganishi chenyewe ni "**na mpake vichwa vyenu.**" Lau kama miguu ingeunganishwa mikono, basi angelisema Mwenyezi Mungu. "Na mikono yenu mpaka vifundoni na miguu yenu mpaka vifundoni".

1 Istilahi ya kinahw: Mansub na nasb, ni kusomwa kwa fatha na khafdh, makhfudh, jarr na majrur ni kusomwa kwa kasra.

Pili: Kuunganisha kwenye mikono kunafanya maana ya kila kisomo kibadilishe maana nyingine. Kwani maana ya kisomo cha Nasb, ni kuosha na kwa kisomo cha jarri ni kwa kupaka. Na hii ni kinyume na kuunganishwa kwenye vichwa ambapo maana inakuwa moja kwa visomo vyote viwili. Zaidi ya hayo kufanya khafdh kwa ujirani si ufasaha wala hajatokea katika maneno ya Mwenyezi Mungu kabisa.

Mkiwa na janaba basiogeni.

Ni wajibu kuoga janaba kwa mojawapo ya mambo mawili:

Kwanza: kushusha manii, iwe katika usingizini au kuwa macho.

Pili: Kuingiza kichwa cha dhakari katika tupu hasa kuitia yote kamili. Sunni hawakuwajibisha aina maalum ya kuoga, isipokuwa wamewajibisha kuenezwa maji kiwiliwili chochote kwa namna yoyote itakayokuwa.

Shia wameligawanya josho la janaba kwenye aina mbili: Tartib (kimpangilio) na Irtimasi (kujivika). Tartib, ni kujimiminia maji kwa kuanzia kichwa, kisha upande wa kuume wa mwili kisha wa kushoto. Lau ataharibu mpango huo, akatanguliza linalokuja baadae, basi josho litabatilika. Ama Irtimasi ni kukivika kiwiliwili chote katika maji kwa mara moja, lau sehemu itakuwa nje ya maji, basi haitoshi.

Na mkiwa wagonjwa au mko safarini au akawa mmoja wenu ametoka chooni, au mkagusana na wanawake, kisha msipate maji, basi tayamamuni na mchanga ulio twahara, mpake nyuso zenu na mikono yenu.

Imetangulia tafsiri yake katika (4:43)

Mwenyezi Mungu hapendi kuwatia katika tabu; lakini anataka kuwatakasa na kutimiza neema Yake juu yenu ili mpate kushukuru.

Tabu ni dhiki na mashaka; na madhara ni tabu na zaidi; kama vile adha, maradhi na kufilisika. Uislamu hauweki hukumu itakayoleta aina yoyote ya dhiki na mashaka, sikwambii madhara. Haukuamrisha jambo ila litakuwa na kheri na masilahi na haukukataza jambo ila ndani yake mtakuwa na shari na uharibifu.

Iwapo jambo lina yote mawili (manufaa na madhara) itaangaliwa, ikiwa manufaa ni makubwa zaidi basi hutakiwa kufanywa, na ikiwa madhara ni makubwa basi hukatazwa. Daima liangaliwalo ni wingi. Ikiwa yote ni sawa, basi kunakuwa na hiyari. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِبُو لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحِبِّيْكُمْ﴾

"Enyi mlionamini! Mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume wake anapowaitia katika yale yatakayowapa uhai" (8:24)

Na akasema tena:

﴿بِرِيدُ اللَّهِ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ﴾

"Mwenyezi Mungu anawatachia yaliyo mepesi wala hawataki yaliyo mazito" (2:185)

Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu na ahadi yake aliyofungamanisha nanyi.

Kila mwenye kuingia dini au chama basi anakuwa amejiwekea mkataba wa kukubali misingi yake na mafunzo yake, na afanye hivyo kwa radhi yake, Na hii ndiyo ahadi ambayo tumemfungia Mwenyezi Mungu sisi Waislamu tulipoukubali Uislamu kuwa ndio dini.

Mwenye kuitekeleza ahadi hii kama alivyoamrisha Mwenyezi Mungu atakuwa amemtekelezea Mwenyezi Mungu, Na mwenye kuasi atakuwa amemfanyia hiyana Mwenyezi Mungu.

Maana yaliyo dhahiri zaidi ya kutekeleza ahadi ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) ni kuwafanyia ikhlasi waja wake na kuamiliana nao kwa ukweli, Na wala sijui alama ya ukweli katika dini zaidi ya kutekeleza ahadi. Namuuusia kila binadamu asimwamini yejote kwa elimu yake au ibada zake au cheo chake na umashuhuri wake, bali amwamini na amtegemee baada ya kuwa na yakini ya ukweli wake na utekelezaje wake wa ahadi.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُوئُنَا قَوَامِينَ لِلَّهِ شُهَدَاءٍ بِالْقِسْطِ وَلَا يَجِدُونَ مَنْكُمْ شَنَآنٌ قَوْمٌ عَلَى أَلَّا تَعْدِلُوا اعْدِلُوا هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ خَيْرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ﴾

8. Enyi mlionamini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mtoao ushahidi kwa uadilifu. Wala kuchukiana na watu kusiwapelekee kutofanya uadilifu, Fanyeni uadilifu ndiko kunakokurubisha kwenye takua, Na Mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu ana habari za mnayoyatenda.

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ﴾

9. Mwenyezi Mungu amewaaahidi wale walioamini na wakafanya mema kuwa watapata maghfira na malipo makubwa.

﴿وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ﴾

10. Na wale waliokufuru na kuzikadhibisha ishara zetu, hao ndio watu wa motoni.

UADILIFU NDIO UNAOKURUBISHA KWENYE TAKUA

Aya 8 - 10

MAANA

Enyi mlionamini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mtoao ushahidi kwa uadilifu.

Imani sahihi inayo mambo ya dhahiri yanayohisiwa. Mwenyezi Mungu ameyapanga na kuyafafanua kwa mifuno mbali mbali katika Aya kadhaa. Mengi yamepita na yanayokuja ni mengi zaidi. Aya tuliyonayo inasema kwa lugha ya wazi wazi kuwa ikiwa nyinyi ni waumini basi muwe wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na mshuhudie uadilifu.

Maana ya kumsimamia Mwenyezi Mungu Mtukufu ni ukweli na ikhlasi katika kauli na vitendo. Ama kushuhudia kwa uadilifu sio makusudio ya kuwatolea ushahidi maadui zetu na walio dhidi yetu kutokana na haki yetu au ya wengine, ingawaje mfumo wa Aya unafahamisha hivyo. Isipokuwa makusudio ni kufanya uadilifu mtu katika mambo yake yote bila ya kuonea.

Akiwa ni mtaalamu wa mambo ya kidunia, elimu yake ataifanya ni nyenzo ya kumaliza sababu za udhaifu, unyonge na kurudi nyuma, na kuleta sababu za kuwa na nguvu na maendeleo. Akiwa ni ulama wa mambo ya dini atalingania neno la Mwenyezi Mungu kufanya uzuri mtu ukhalifa wa Mwenyezi Mungu katika ardhi yake na kumsimamisha kila anayeipeleka kombo njia hii. Na akiwa hajui (sio ulama), basi atawaitikia wenye elimu na dini na kuwa upande wao akiwasaidia na kuwaunga mkono maadamu wako pamoja na haki.

Huu ndio uadilifu aliouamrisha Mwenyezi Mungu katika Aya hii na nyinginezo. Uadilifu ambao ndio matumaini ya ubinadamu na lengo lake, na ambao maisha hayawezi kuwa bila ya huo. Jamii inaweza kuishi bila ya elimu, lakini kuishi bila ya uadilifu katika upande wowote ule ni muhali, hata kama watu wake ni magwiji na wagunduzi. Elimu bila ya uadilifu madhara yake ni mengi kuliko manufaa yake. Ama uadilifu wote ni manTafsir ufaa, na ni muhali kuweko aina ya madhara ndani yake. Na kama ukiyapata, basi itakuwa ni njia ya kuzuia madhara makubwa zaidi na yenye hatari kubwa.

Wala kuchukiana na watu kusiwapeleke kutofanya uadilifu.

Fanyeni uadilifu Makusudio ya watu katika Aya hii ni maadui wa kheri na uadilifu ambao wanakwamisha kila jaribio la kumkomboa binadamu na minyororo ya udhaifu na kutoendelea. Mwenyezi Mungu (s.w.t) anatuamrisha kufanya uadilifu na kufanya mambo kwa ajili ya maisha ya binadamu bila ya kujali chuki ya wanaokwenda kombo na vitimbi vyao. Kwa maneno mengine, inatakikana tufanye mambo kwa kutumia mfano unaosema: "mbwa anabweka na safari yaendelea"

Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini na wakafanya mema kuwa watapata maghfira na malipo makubwa.

Katika (2:25) Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewapa bishara waumini wa vitendo kwamba wao wana Pepo ambazo hupita mito chini yake, katika (3:57) akawabashiria kuwa Yeye atawalipa ujira, akaongeza katika (4:56) kwamba wao Peponi watapata Wake watakatifu. Na katika Sura nyingine akatoa ahadi kwa mifumo mingine. Lengo katika Sura zote ni moja tu - kuhimiza imani na matendo.

Na wale waliokufuru na kuzikadhibusha ishara zetu, hao ndio watu wa motoni.

Baada ya kuwaahidi neema waumini wa kimatendo, anawapa kiaga cha moto makafiri, kama kawaida yake Mwenyezi Mungu Mtukufu ya kufuatisha kuhimiza na kuhofisha.

Aya hii ni dalili wazi kuwa mwenye kumkanusha Mwenyezi Mungu ni katika watu wa motoni, hata kama hakuambiwa na Mtume au wasii wa Mtume. Kwa sababu dalili zake Mwenyezi Mungu ambazo zinakuwa ni hoja ya kuweko kwake hazihusiki na aliyowateremshia mitume Wake. Ameisimamisha dalili ya kutosha juu ya umoja Wake na ukuu Wake katika nafsi na katika mbingu na ardhini; atakayezikanusha, hoja iko juu yake.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿أَوَلَمْ يَتَعَكَّرُوا فِي أَنفُسِهِمْ مَا خَلَقَ اللَّهُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا إِلَّا بِالْحَقِّ﴾

"Je hawafikirii katika nafsi zao (wakaona kuwa) hakuumba Mwenyezi Mungu mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake ila kwa haki?". (30:8)

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ هُمْ قَوْمٌ أَنْ يَبْسُطُوا إِلَيْكُمْ أَيْدِيهِمْ فَكَفَّ أَيْدِيهِمْ عَنْكُمْ وَأَثْقِلُوا اللَّهَ وَعَلَى اللَّهِ فَلِيَوْكِنِ الْمُؤْمِنُونَ﴾

11. Enyi mliaoamini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu juu yenu, walipoazimia watu kuwanyooshea mikono yao, akaizua mikono yao kuwafikia. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu.

KUMBUKENI NEEMA YA MWENYEZI MUNGU

Aya 11

MAANA

Enyi milioamini! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu juu yenu, walipoazimia watu kuwanyooshea mikono yao, akaizua mikono yao kuwafikia.

Ikisemwa amemnyooshea ulimi ni kumtukana, na amemnyooshea mkono ni kumshambulia.

Makusudio ya watu hapa ni washirikina wa Makka ambao walitaka kuumaliza Uislamu ulipoanza, kwa njia ya kuwashambulia wafuasi wake kwa kuwaua, kuwaadhibu na kuwafukuza kisha kutangaza vita na kuandaa majeshi. Lakini Mwenyezi Mungu hatimaye aliwapa ushindi Waislamu kwa maadui zake na wakawa watukufu baada ya kuwa dhalili na watawala badala ya kutawaliwa. Wala hakuna neema kubwa kuliko uhuru na kuwashinda maadui.

Baada ya Mwenyezi Mungu (swt) kuwakumbusha Waislamu neema hii tukufu, aliaaambia;

Na mcheni Mwenyezi Mungu, na waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu.

Yaani, tumewapa nguvu hizi ili mztumie katika kuithibitisha haki na wala sio kuonyesha ushujaa; na katika kueneza amani na uadilifu, sio kuwakandamiza wanyonge kuwakalia na kuwatawala, kama walivyowafanya washirikina hapo mwanzo na kama wafanyavyo watu wengi.

Wanatafuta uadilifu wawapo wanyonge na wanaukanusha mara tu wawapo na nguvu. Mumin wa kweli humwogopa Mwenyezi Mungu na kumshukuru akiwa na nguvu zaidi kuliko akiwa dhaifu; au angalau sawa katika hali zote mbili. Ama yule anayeamini kwa ulimi bila moyo, basi ni kinyume:

﴿فَإِذَا رَكِبُوا فِي الْفُلْكِ دَعَوْا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ التَّيْنَ فَلَمَّا تَجَاهُمْ إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ﴾

"Na wanapopanda katika Jahazi humuomba Mwenyezi Mungu hali ya kuwa wanamtakasia utii, lakini anapowafikisha salama nchi kavu, mara wanamshirikisha" (29:65)

﴿وَلَقَدْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَبَعْثَنَا مِنْهُمُ الْتَّيْنَ عَشَرَ نَقِيبًا وَقَالَ اللَّهُ إِنِّي مَعَكُمْ لَئِنْ أَقْمُمُ الصَّلَاةَ وَآتَيْتُمُ الرِّزْكَةَ وَآمِنْتُمُ بِرُسُلِي وَغَرَّرْتُمُوهُمْ وَأَقْرَضْتُمُ اللَّهَ قُرْضًا حَسَنًا لَا كُفَّارٌ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَلَا دُخْلَنَّكُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ فَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ مِنْكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيلُ﴾

12. Na hakika Mwenyezi Mungu alifanya agano na wana wa Israil na tukaweka mionganini mwao wakuu kumi na wawili. Na Mwenyezi Mungu akasema: Kwa hakika mimi niko pamoja nanyi, kama mkisimamisha Swala na mkatoa Zaka na mkaamini mitume yangu na mkawasadidua na mkamkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mzuri; hakika nitawafutia maovu yenu na nitawaingiza katika mabustani yapitayo mito chini yake, Basi atakayekufuru baada ya hayo hakika amepotea njia iliyo sawa.

﴿فِيمَا نَقْضَيْهِمْ مِّيقَاتُهُمْ وَجَعَلْنَا قُلُوبَهُمْ قَاسِيَةً يُحِرِّقُونَ الْكَلْمَ عَنْ مَوَاضِعِهِ وَنَسُوا حَطَّا
مِمَّا ذُكِرُوا بِهِ وَلَا تَرَأْلُ تَظْلِعُ عَلَىٰ حَائِنَتِهِمْ نَهْمٌ إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاصْفُحْ إِنَّ اللَّهَ
يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ﴾

13. Basi kwa sababu ya kuvunja kwao agano, tuliwalaani na tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu. Wanageuza maneno na mahali mwake na wakaacha sehemu ya yale waliyokumbushwa. Na hutaacha kugundua khiyana yao, isipokuwa wachache mionganini mwao. Basi wasamehe na uwaache, Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.

﴿وَمَنِ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّا نَصَارَىٰ أَخْذَنَا مِيقَاتُهُمْ فَنَسُوا حَطَّا مِمَّا ذُكِرُوا بِهِ فَأَغْرَيْنَا بَيْنَهُمُ الْعَدَاؤُ
وَالْبَعْضَاءِ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَسَوْقَ يُبَيِّنُهُمُ اللَّهُ بِمَا كَانُوا يَصْنَعُونَ﴾

14. Na kwa wale waliosema: "Sisi ni Wanaswara", tulifanya agano nao, lakini wakaacha sehemu ya yale waliyokumbushwa, kwa hiyo tukaweka baina yao uadui na chuki mpaka siku ya Kiyama, Na Mwenyezi Mungu atawaambia waliyokuwa wakiyafanya.

KUFANYAAGANO NAWAISRAIL

Aya 12 - 14

MAANA

Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika Kitabu chake kitukufu amezungumzia makafiri na washirikina kwa ujumla, na akazungumzia washirikina wa Kiquraish kwa Sura mahsus, kutokana na aliyo yapata Mtume kutoka kwao. Vilevile amewazungumzia wanafiki, ambao walidhihirisha Uislamu na kuuficha ukafiri, na Mayahudi na Wakristo, lakini Mayahudi amewazungumzia zaidi kuliko wote. Kwa sababu wao ndio waliokuwa na inadi zaidi na chuki juu ya ubinadamu. Yamepita mengi kuwahu su wao katika Sura ya Baqara, Al-Imran na Annisa. Sehemu kubwa ya Sura tuliyonayo (Al-Maida), inawahu su wao na Wakristo.

Na hakika Mwenyezi Mungu alifanya agano na wana wa Israel na tukaweka mionganini mwao wakuuu kumi na wawili.

Mwenyezi Mungu ametaja kuwa amewaweka viongozi kumi na wawili katika wana wa Israel, na wala hakubainisha kuwa je, hawa ni viongozi wa vizazi vyao ambao wanawakilisha matawi kumi na mawili ya Yakub, ambaye ndiye Israel, au ni Mitume au Mawasii? Hakutaja chochote, na sisi tunanyamaza aliyoyanyamizia Mwenyezi Mungu.

Aya inaelezea wazi kuwa Mwenyezi Mungu alikuwa na ahadi na waisrail, inayowataka watekeleze mambo matano na Mwenyezi Mungu atawalipa mambo mawili wakitekeleza, na wasipotekeleza watastahili adhabu. Mambo yenyewe ni haya yafuatayo:-

1. Kusimamisha Swala (**Mkisimamisha Swala**)
2. Kutoa Zaka (**na mkatoa Zaka**)
3. Kuamini Mitume ya Mwenyezi Mungu (**Na mkaamini Mitume yangu**)
4. Kusaidia Mitume (**na mkawasaidia**)
5. Kutoa mali Sabili (**Na mkamkopeshwa Mwenyezi Mungu mkopo mzuri**). Kuunganishwa kukopeshwa na Zaka kunafahamisha kuwa ilikuwa ni wajibu katika mali yao mambo mawili: Zaka na kutoa mali sabili.

Wakitekeleza mambo haya matano ambayo ni masharti katika agano lao, basi Mwenyezi Mungu atawalipa mambo mawili yakiwa ni malipo ya masharti hayo. Mambo yenye ni:-

1. Kufutiwa maovu (**hakika nitawafutia maovu yenu**).

2. Pepo (**na nitawaingiza katika mabustani yapitayo mito chini yake**). Hili ndilo agano la Mwenyezi Mungu na waisrail pamoja na masharti yake na malipo, Baada ya kubainisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwaambia: Basi atakayekufuru baada ya hayo hakika amepotea njia iliyo sawa.

Basi kwa sababu ya kuvunja kwao agano, tuliwalaani.

Hakika wao wanavunja kila ahadi isipokuwa ahadi ya kuvunja ahadi, Hii ni nembo isiyowabanduka milele, kama ambavyo laana haiwabanduki, kwa vile kuvunja ahadi kunalazimiana na laana.

Na tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu

Kila asiyeogopa shari na maasi basi moyo wake umekufa. Amesema Imam Ali ^(a.s). "**Ambaye imekuwa chache staha yake basi moyo wake umekufa."**"

Unaweza kuuliza: Vipi Mwenyezi Mungu amenasabisha kwake ugumu wa nyoyo zao? Je, hii haimanishi kuwa wao hawana jukumu lolote na ugumu huu, kwa sababu unatoka kwa Mungu na sio kwao?

Jibu: Mwenyezi Mungu amewabainshia njia ya heri na akawaamrisha kuifuata hiyo njia; na akawabainshia njia ya sharii, akawakataza kuifuatia; na akachukua kwao ahadi ya kusikiliza na kutii, kisha wakahaini, wakavunja ahadi na wakaendelea kuasi. Kwa hiyo akawaachilia mbali; na asiwaelekeze kwenye amali ya kheri; na kwa kuwa Mwenyezi Mungu hakuwaelekeza ndio ikasihi kunasibishiwa kwake ugumu. Mwenye kutaka zaidi, na arudie tuliyoyaeleza katika kufasiri Sura (4:88).

Wanageuza maneno na mahala mwake.

Imetangulia tafsiri yake katika Sura (4:46)

Na wakaacha sehemu ya yale waliyokumbushwa.

Wamekumbushwa Taurat wakabadilisha yale yanayopingana na matakwa yao na kubakisha wanayoyatamani. Ikiwa wameweza kuvunja ahadi ya Mwenyezi Mungu, na wakakibadilisha Kitabu chake alichowateremshia basi watashindwaje kuvunja ahadi na waarabu na wengineo na kugeuza maaazimio ya Umoja wa Mataifa na Baraza la usalama.

Na hutaacha kugundua khiyana yao, isipokuwa wachache mionganini mwao.

Mayahudi wa Bara arabu wakati huo hawakutosheka na kuukanusha utume wa Muhammad (**s.a.w.w**) bali walikula njama pamoja na maadui zake, ndipo Mwenyezi Mungu akamwambia hivyo; yaani wewe Muhammad umekutana na mengi kutoka kwao na utaendelea kukutana na mengi, hata kama utawafanya wema, kwa sababu mwema na mbaya kwao ni sawa, isipokuwa wachache tu katika wao waliosilimu na wakasadikisha Uislamu wao, kama Abdullah bin Salam na waliokuwa pamoja naye. Pamoja na yote hayo, Mwenyezi Mungu amemwamrisha Mtume wake kuukabili uovu wao kwa wema.

Basi wasamehe na uwaache.

Unaweza kuuliza: kuwa ni umbali sana kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) kuwasifu kwa sifa mbaya na kwamba haitarajiwi kheri kutoka kwao, kisha amwamrishe Mtume wake awasamehe na kuachana nao. Je Mayahudi wanajua maana ya msamaha? Na je, inafaa kumsamehe nyoka na nge.

Swali hilo limejibiwa kwa majibu kadha; kama vile kuwa dhamiri ya 'wasamehe' inawarudia wachache waliosilimu na kufanya ikhlas. Jengine ni kuwa Aya hii imefutwa hukmu yake na Aya ya upanga.

Majibu yote haya yanawezekana. Ama la kwanza ni kwamba dhamiri kwa dhahiri yake inamrudia aliye karibu. Ama la pili ni kupatikana 'kufuta hukumu' katika Qur'an.

Inawezekana kuwa amri ya kuwasamehe ilishuka baada ya Uislamu kuwa na nguvu ukawa katika ngome madhubuti isiyodhurika na vitimbi nya Mayahudi na wengineo katika makafiri.

Na kwa wale walisema: Sisi ni manaswara, tulifanya agano nao.

Baada ya kubainisha Mwenyezi Mungu (s.w.t) hali ya Mayahudi ya kuvunja ahadi na kubadilisha, amebainisha hali ya Wakristo, na kwamba wao na Mayahudi hali yao ni moja tu, lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Aya iliyotangulia ametaja aina ya ahadi waliyoivunja Mayahudi, na hapa hakutaja ya Wakristo. Sio mbali kuwa Mwenyezi Mungu ametumia maneno ya kiujumla kwa Wakristo kwa kufafanua ahadi aliyochukua kutoka kwao ambayo ni Tawhid.

Na wakaacha sehemu ya yale walivokumbushwa.

Walivokumbushwa ni Injil aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu kwa Isa (a.s) inayoeleza wazi wazi Umoja wa Mwenyezi Mungu na utume wa Muhammad (s.a.w.w) kwa jina la Ahmad, lakini wakabdalisha, sawa na Mayahudi walivyobadilisha Taurat.

Dalili ya nguvu zaidi kuwa Injil imebdilishwa ni kwamba viongozi wa kanisa na Maulama wa historia katika Injil nne ambao Wakristo waliwategemea katika karne ya nne, walitofautiana kuhusu nani aliyeandika Injil, imeandikwa lini, kwa lugha gani na vipi imekosekana kopi yake ya asili? Tofauti hizi zinapatikana katika Encylopedias kubwa ya Kifaransa. Haya na mengine mengi ameyataja mwenye Tafsiri Al-manar.

Kwa hiyo tukaweka baina yao uadui na chuki mpaka siku ya Kiyama.

Hakuna maneno bora yaliyosemwa, katika kufasiri jumla hii, kama yale yalisemwa na Sheikh Abu Zahra katika Kitabu Muhadharat fi Annasraniyya. Kwa hiyo ninamnukuu: "Kumetokea kutolewana na uadui baina ya wale walosema: Sisi ni Manaswara, tangu zamani na hivi sasa, kusadikisha yale aliyyasema Mwenyezi Mungu (s.w.t) katika Kitabu chake kikweli na kitukufu.

Damu zimemwagika baina yao wenywewe, kiasi ambacho hakijawahi katika kupigana kwao na watu wengine katika historia yote. Ni sawa iwe hilo ni kwa sababu ya tofauti za kidini au uongozi wa kidini au hata tofauti za kisisasi, kiuchumi na kijamii. Uadui huu umeendelea muda mrefu na wala hautazimika mpaka siku ya Kiyama, kama alivyosema Mkweli wa wasemaji."

﴿يَا أَهْلَ الْكِتَابِ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ كَثِيرًا مِمَّا كُنْتُمْ تُحْقِنُونَ مِنَ الْكِتَابِ وَيَعْلَمُونَ عَنْ كَثِيرٍ قَدْ جَاءَكُمْ مِنَ اللَّهِ نُورٌ وَكِتَابٌ مُبِينٌ﴾

15. Enyi watu wa Kitabu! Amekwishawafikia Mtume wetu, anayewafichulia mengi mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anayesamehe mengi. Hakika imekwisha wafikia nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Kitabu kinachobainisha.

﴿يَهْدِي بِهِ اللَّهُ مَنِ اتَّبَعَ رِضْوَانَهُ سُبُّلُ السَّلَامِ وَيُخْرِجُهُمْ مِنَ الظُّلْمَاتِ إِلَى الْفُورِ يَأْذِنُهُ وَيَهْدِيهِمْ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ﴾

16. Mwenyezi Mungu huwaongoza kwacho wenyewe kufuata radhi yake katika njia za amani na huwatoa katika giza kuwapeleka kwenya nuru kwa amri yake, na huwaongoza katika njia iliyonyooka.

IMEKWISHAWAFIKIA NURU

Aya 15 - 16

MAANA

Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimwamrisha Mtume wake (s.a.w.w) na Waislamu wote kujadiliana na watu wa Kitabu kwa uzuri; kisha akatoa mfano wa mjadala huu ili wawe na ubainifu wa maana yake. Miogoni mwa mifano hiyo ni kusema Waislamu kuwaambia watu wa Kitabu:

﴿آمَّا بِالَّذِي أَنْزَلَ إِلَيْنَا وَأَنْزَلَ إِلَيْكُمْ وَإِلَيْهُمَا وَإِلَهُكُمْ وَاحِدٌ وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ﴾

"Tunaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu na Mungu wetu na Mungu wenu ni mmoja, nasi ni wenyewe kusilimu kwake" (29:46)

﴿قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْ إِلَى گَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَا تَعْبُدُ إِلَّا اللَّهُ وَلَا تُشْرِكُ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا أَرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ﴾

"Sema enyi watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno la usawa baina yetu na baina yenu. Kwamba tusimwabudu yejote ila Mwenyezi Mungu wala tusimshirikishe na chochote, wala baadhi yetu wasiwafanye baadhi kuwa ni miungu, zaidi ya Mwenyezi Mungu." (3:64)

Na kuna Aya zinazoeleza baadhi ya madhambi ya watu wa Kitabu, kama vile Aya hii tuliyo nayo. Imetaja kugeuza kwao Taurat na Injil na kumfanyia inadi Muhammad aliywajia na uongofu.

Enyi watu wa Kitabu! Amekwisha wafikia Mtume wetu, anayewafichulia mengi mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anayesamehe mengi.

Makusudio ya Mtume ni Muhammad (s.a.w.w) kwa sababu yeze amewabainishia Mayahudi na Wakristo, baadhi ya waliyoyaficha katika Kitabu walichonacho. Wakristo walificha Tawhid ambayo ni msingi wa dini na Mayahudi katika itikadi wakaficha habari ya Hisabu na adhabu siku ya Kiyama, na katika sharia wakaficha uharamu wa riba na kurujumiwa mzinifu; kama ambavyo Mayahudi na Wakristo kwa pamoja walificha Utume wa Muhammad:

"Ambaye wanamkuta ameandikwa kwao katika Taurat na Injil." (7:157) Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimfichulia Muhammad (s.a.w.w) yote waliyoyaficha na kuyabdalisha Mayahudi katika Taurat na Wakristo katika Injil, kisha Muhammad (s.a.w.w) akawaambia mengi waliyokuwa wakiyaficha na akayanyamazia mengi aliyyojua. Hii ndio maana ya:

Anayewafichulia mengi mliyokuwa mkiyaficha katika Kitabu, na anayesamehe mengi.

Ufichuaji huu kutoka kwa Muhammad umekuwa ni dalili ya mkato ya utume wake na miujiza mionganoni mwa miujiza ya Qur'an ambao haifai kwa mwenye akili kuutilia shaka. Kwa sababu Mtume (**s.a.w.w**) alikuwa ni Ummiy (asiyesoma Kitabu) wala hakuambiwa na yeote yaliyo katika vitabu vya Mayahudi na Wakristo.

Unaweza kuuliza: Kwa nini Mtume aliwaambia baadhi tu na asiwaambie yote.

Jibu: Lengo ni kuwafahamisha kuwa Mtume anayajua wanayoyaficha; na lengo hilo linafikiwa kwa kuyasema baadhi; kama ambavyo linafikiwa kwa kueleza yote. Zaidi ya hayo ni kwamba walijua kuwa yeze Mtume (**s.a.w.w**) anajua baadhi ya waliyoyaficha basi ndio wamejua kuwa yeze anayajua yote.

UISLAMU NAWAPIGANIAAMANI

Hakika imekwishawafikia nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Kitabu kinachobainisha.

Imesemwa kuwa **Nuru** ni Muhammad na **Kitabu** ni Qur'an; na ikasemwa kuwa hizo ni sifa za Uislamu, wala hakuna tofauti baina ya kauli mbili ila katika ibara tu, kwa sababu Muhammad, Uislamu, na Kitabu ni maana yanayolazimiana hayaachani.

Mwenyezi Mungu huwaongoza kwacho wenyewe kufuata radhi yake.

Yaani mwenye kupendelea radhi ya Mwenyezi Mungu peke yake, na akaitafuta haki kwa njia ya haki, atapata katika Uislamu matakwa yake na makusudio yake, Kwa sababu ndani yake kuna faida tatu.

1. **Njia za amani:** Makusudio ya amani sio ile wanayoishisha wapigania amani, ya kutaka amani kwenye roho na mali za raia, isipokuwa makusudio ni amani kamili inayowachanganya watu wote, amani ya nyumba na familia kutokana na malezi mabaya. Vilevile Usalama wa akili kutokana na ujinga na imani potofu, na kusalimika nafsi na tamaa, chuki, uongo na hadaa.

2. **Na huwatoa katika giza kuwapeleka kwenye Nuru kwa amri yake:** Yaani anawatoa Mwenyezi Mungu kwa amri yake kutoka katika giza la kuabudu masanamu kwenye Nuru ya Tawhid ambayo itawakomboa na vifungo vyote isipokuwa kumwabudu Mwenyezi Mungu mwenye nguvu.

3. **Na huwaongoza katika njia iliyonyoka:** Njia iliyonyoka kwa Mwenyezi Mungu ni ile inayoyafanya maisha haya kuwa ni raha na wema, sio mashaka na uovu. Baada ya yote hayo je, watetezi wa amani wanaopiga kelele za kuongeza mapato yatosheleze watu wote, wanayo njia bora na yenye kufaa zaidi ya ile ya Uislamu? Je, wao wanawapenda waja wa Mwenyezi Mungu zaidi au wao wanajua zaidi masilahi yao kuliko Yeye Mwenyezi Mungu anavyojua kwa viumbwe vyake? Au je, katika itikadi ya kiislamu, sharia ya kiislamu na maadili ya Uislamu au katika hukumu za kiislamu, kuna hata moja inayopingana na kuongeza kipato na kukigawanya kwa haki?

Qur'an ndiyo ya kwanza kulingania kwenye maisha bora. Mwenyezi Mungu (**s.w.t**) anasema: "Hakika hii Qur'an inaongoza katika njia iliyonyooka kabisa." (17:9)

Wafasiri wanasema kuwa njia iliyonyooka ni hali nzuri. Vyovyyote nitakavyotia shaka, lakini nina yakini kwamba hakuna yeyote anayeusoma Uislamu kwa usahihi, yaani kwa uwezo na kutokuwa na kitu kingine, ila atauamini, atake asitake.

﴿لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ قُلْ فَمَنْ يَمْلِكُ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا إِنْ أَرَادَ أَنْ يُهْلِكَ الْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَأُمَّهُ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾

17. Hakika wamekufuru wale waliosema: Mwenyezi Mungu ni Masih bin Maryam! Sema: Ni nani anayemiliki chochote mbele ya Mwenyezi Mungu kama akitaka kumwangamiza Masih bin Maryam na mama yake na waliomo ardhini wote? Na ni wa Mwenyezi Mungu ufalme wa mbingu na vilivyomo baina yake. Huumba atakavyo; na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.

﴿وَقَالَتِ الْيَهُودُ وَالنَّصَارَىٰ تَحْنُّ أَبْنَاءَ اللَّهِ وَأَجْبَأُوهُ قُلْ فَإِمَّا يُعَذِّبُكُمْ بِذُنُوبِكُمْ بَلْ أَنْتُمْ بَشَرٌ مِّمَّنْ خَلَقَ يَعْفُرُ لِمَنْ يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَإِلَيْهِ الْمَصِيرُ﴾

18. Na Mayahudi na Manaswara wanasema: Sisi ni watoto wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake. Sema: Basi kwanini anawaadhibu kwa ajili ya dhambi zenu? Bali nyinyi ni watu (tu) katika aliowaumba. Humghufiria amtakaye na humwadhibu amtakaye. Na ni wa Mwenyezi Mungu ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake; na marejeo ni kwake.

﴿يَا أَهْلَ الْكِتَابِ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمْ عَلَىٰ فَتْرَةٍ مِّنَ الرُّسُلِ أَنْ تَقُولُوا مَا جَاءَنَا مِنْ بَشِيرٍ وَلَا نَذِيرٍ فَقَدْ جَاءَكُمْ بَشِيرٌ وَنَذِيرٌ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾

19. Enyi watu wa Kitabu! Hakika amewafikia Mtume wetu anayebainishia, katika wakati usio na Mitume, msije mkasema: Hakutufikia mtoaji bishara wala mwonyaji; basi amekwishawafikia mtoaji bishara na mwonyaji na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu.

WALISEMA MWENYEZI MUNGU NI MASIH

Aya 17 - 19

MAANA

Hakika wamekufuru wale waliosema: Mwenyezi Mungu ni Masih bin Maryam. Tumefahamu kuwa hukumu za sheria za kutungwa zinabadilika kulingana na wakati. Ama kubadilika misingi ya itikadi ya kidini, kulingana na hali na wakati, ni jambo lisiloingilika akili, Lakini yametokea haya katika itikadi ya Kimasihi (Kikristo).

Itikadi ya Kimasih ilianzia na Tawhid (Umoja wa Mungu) safi; na baadhi ya vikundi vikaenedelea kubaki kwenye Tawhid kwa mda mrefu. Miongoni mwa vikundi hivyo ni kikundi cha Paul, Arius na Apico; kama inavyoeleza Aya 116-117 katika sura hii (Al-Maida), Na Qur'an imeelezea wazi kuwa Isa ^(a.s) alileta itikadi ya Tawhid (Mungu Mmoja). Kama inavyoeleza Aya 116-117

Ikaendelea itikadi ya Tawhid kwa Wakristo wengi na wala haikutangazwa itikadi ya utatu na kuungwa mkono kwa nguvu hadi mwaka 325 AD, ambapo baraza kuu la Nicaea lilipitisha uamuzi wa kuthibitisha uungu wa Masih na kumkufurisha mwenye kusema kuwa yeye ni mtu; wakachoma vitabu vyote vinavyomsifu kuwa si Mungu, na akautekeleza uamuzi huo, Costantine, Mfalme wa Roma. Akawa Masih ni Mungu kwao baada ya kuwa ni mtu.¹ Amesema kweli mwanafalsafa wa Kichina Lin Yu Tang: "Hakika Wagiriki wamewafanya miungu yao mfano wa watu. Ama Wakristo waliwafanya watu mfano wa Mungu"

Abu Hanifa naye anasema kuwa Mwenyezi Mungu hana hukumu hasa, ispukuwa hukumu yake ni vile anavyoona Mujtahid; yaani hukumu ya Mwenyezi Mungu hasa ni ile aliyoihukumu mtu pekee; si kwambii kundi au baraza kuu.

Kwa hali hiyo, inatubainikia kuwa itikadi ya Uungu wa Isa ^(a.s) ilikuwa kabla ya kushuka Qur'an kwa kiasi cha karne tatu. Kwa hiyo makusudio ya kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu;

Hakika wamekufuru wale waliosema Mwenyezi Mungu ni Masih bin Maryam.

Maana yanakuwa yako wazi yasiyohitajia taawili ya kuingiliana na umoja; kama walivyofanya wafasiri wengi waliotangulia, wakidai kwamba Wakristo wengi hawasemi kuwa Isa ni Mungu, bali wanasesma Mungu ameingia kwake au ameungana naye kwa hiyo hapana idadi. Mwenye Tafsir Al-manar anasema: "Mfano wa Zamakhshari, Baidhawi na Arrazi, hawakuangalia kwa undani kuhusu Ukristo; Kwa sababu hawakuvisoma vitabu vyao wala kuvipitia" Amesema kweli mwenye Al-Manar; kwani mwenye kuviangalia vitabu vyao, atakuta maelezo ya utatu waziwazi.

Amenkuu Sheikh Abu Zahra maelezo mengi kutoka katika vitabu hivyo, katika Kitabu Muhadharat Fi Annasraniyya na akaweka mlango maalum, katika Kitabu hiki, kwa anuani: "Ukristo kama ulivyo kwa Wakristo na katika vitabu vyao!" Miogoni mwa yaliyomo ni kwamba; Kasisi Butar alitunga risala aliyoita Al-usul wal-furuu akisema: "Katika Ungu kuna asili tatu, na kila mmoja ina kazi yake mahsus kwa mtu." Yamekwishatangulia maelezo kuhusu asili tatu, katika kufasiri Sura (4:50)

ASHAIRA NAWAKRISTO

Unaweza kuuliza: Wakristo wanaamini utatu na umoja wakati mmoja, kwa sababu wao wanasesma: Kwa jina la baba na la mwana na la roho mtakatifu Mungu Mmoja. Sasa inawezekanaje kuchanganya umoja na utatu? Vipi moja iwe tatu na tatu iwe moja?

Wakristo wenyewe wamejibu hilo, kuwa: itikadi iko juu ya akili na wao wanakuza watoto wao kwenye hilo na kuwaambia: Kama hamkufahamu hakika hii mtaifahamu Siku ya Kiyama.

Kwa mnasaba huu tunaashiria kuwa Ashaira katika Waislamu wanasesma: Mwenyezi Mungu anamtakia mja ukafiri, kisha anamwadhibu. Ikiwa kauli

1 Mabaraza kwa Wakristo yako sehemu tatu: Kuna baraza kuu, linalokusanya wawakilishi wa Makanisa yote ulimwenguni. Hili uamuzi wake haupingwi. Na kuna lile la mila ambalo linahusika na mambo ya mila fulani. Na jingine ni lile la majimbo linahusika na jimbo.

ya Wakristo, ya tatu moja haingiliki akilini, basi kauli ya Ashaira, kuwa Mwenyezi Mungu anafanya kitu kisha ana mwaadhibu mja wake haingiliki akilini vile vile.

Ama Waislamu wanaamini kwa imani ya mkato kwamba kila linalothibitishwa na akili, linathibitishwa na dini, na linalokataliwa na akili, linakataliwa na dini. Na wamepokea kutokana na Mtume wao kuwa ye ye amesema: "Asili ya dini yangu ni akili." Na kwamba mtu mmoja alimuuliza kuhusu maana ya wema na dhambi; akamwambia: "Utake fatwa moyo wako. Wema ni ule uliotuliza nafsi, na ukatulizana moyo. Na dhambi ni ile iliyotia wasiwasi nafsi na kusitasita moyoni, hata kama watu watakutolea fat-wa.

Sema: Ni nani anayemiliki chochote mbele ya Mwenyezi Mungu kama akitaka kumwamngamiza Masih bin Maryam, na mama yake na waliomo ardhini wote?

Aya hii ni dalili kubwa ya kuwajibu Wakristo kuwa Masih si Mungu, Kwa sababu ikiwa Mwenyezi Mungu anaweza kumwamngamiza Masih, basi Masih si Mungu. Na kama hawezi kumwangamiza, basi Yeye sio Mwenyezi Mungu.

Huenda mtu akasema kuwa: Aya hii haifai kuwa ni jibu kwa Wakristo, pia si dalili ya ukweli. Kwa sababu ni madai yasiyokuwa na dalili. Wakristo wanaweza kusema kuwa Mwenyezi Mungu hawezi kumwangamiza Masih wala Masih hawezi kumwangamiza Mwenyezi Mungu, kwa vile kila mmoja ni Mungu?

Jibu: Wakristo wameafikiana kwa kauli moja kwamba Mayahudi walimsulubu Masih, wakamwuudhi na kumwua na kumzika kaburini chini ya ardhi. Vile vile Injil yao imesema: "Naye Yesu akiisha kupaza sauti tena kwa nguvu, akaitoa roho yake." (Mat; 27:50). "Yesu akalia kwa sauti kuu, akasema, Ee Baba, Mikononi mwako naiweka roho yangu. Alipokwisha kusema hayo akakata roho" (Luka 23:46)

Lakini walipomjia Yesu na kuona kuwa amekwisha kufa, hawakumvunja miguu; Lakini askari mmoja wapo alimchoma ubavu kwa mkuki; na mara ikatoka damu na maji (Yohana 19: 33-34)

Na Mayahudi na Manaswara wanasema: Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake. Kauli yao hii ni sawa na kauli ya waliyozungumziwa na Mwenyezi Mungu aliposema: "Na walisema: Hataingia peponi ila aliye Myahudi au Mnaswara."(2:111) Kwa hakika itikadi ya Kiislamu inasema kuwa hakuna ubora wa binadamu kwa mwanadamu mwingine ila kwa takua, na kwamba kutamka neno Uislamu tu si chochote ila iwe pamoja na matendo mema. Sema: Basi kwanini anawaadhibu kwa ajili ya dhambi zenu?

Unaweza kusema: kuwa hili halitoshi kuwa ni jibu la Mayahudi, kwa sababu wanaweza kusema: Mwenyezi Mungu hatatuadhibu akhera! Ikiwa hawana dalili ya kutoadhibiwa kwao huko Akhera, vile vile hakuna dalili ya kuadhibiwa kwao siku hiyo?.

Jibu: Makusudio ya adhabu ni adhabu ya duniani na akhera. Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewaadhibu Mayahudi duniani kwa Fir'aun, Nebukadnezzar, Roma na wengineo. Angalia tafsiri ya Sura (2:40).

Ama adhabu ya Wakristo duniani hiyo ni chungu zaidi. Kwa sababu walikuwa wakipigana wenyewe kwa wenyewe na kuadhibiana wenyewe kwa wenyewe. Iilivyo hasa, baba hawezi kuwaadhibu wanawe, na mpenzi hawadhibu wapenzi wake.

Ama dalili ya kuadhibiwa kwao huko akhera ameiasiria Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa kauli yake, bali nyinyi ni watu (tu). Hamtofautiana na wengine katika chochote. Watu wote wanatokana na Adam, na Adam ameTafsir tokana na mchanga! Kama alivyosema Mtume wa Mwenyezi Mungu (**s.a.w.w**).

Humghufiria amtakaye, ambaye anamwona anastahiki maghufira yake. **Na humwadhibu amtakaye**, ambaye anamwona kuwa anastahiki adhabu yake.

Hakuna yeote atakayemlazimisha msamaha au kumzuia kuadhibu. Na ni wa Mwenyezi Mungu ufalme wa mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake. Kwa sababu yeye ni muumba wa ulimwengu, Na mwenye kuwa hivyo hahitajii watoto wala wapenzi.

Na marejeo ni Kwake.

Huko watajua Mayahudi na Wakristo kwamba wao ndio waja wa Mwenyezi Mungu waliochukiwa zaidi na Mwenyezi Mungu na watakuwa na adhabu zaidi kwa kumzulia kwao uongo kuwa wao ni watoto wa Mwenyezi Mungu na wapenzi wake.

Enyi watu wa Kitabu! Hakika amewafikia Mtume wetu, anayewabainishia, katika wakati usio na mitume.

Yaani; baada ya kukatika wahyi kwa muda mrefu na kuhitaji watu mitume na mwongozi. Imam Ali (^(a.s)) anasema: "**Alimtuma Mtume na watu wamepotea wamedangana, wanakusanya fitina, wamechotwa na matamanio, wameingiwa na Kibr, wamechanganyikiwa na ujinga, wamedangana katika mgongano wa mambo na balaa la ujinga, Akafikisha Mtume (s.a.w.w) nasiha na kulingania kwa hekima na mawaidha mazuri.**"

Msije mkasema: Hakutufikia mtoaji bishara wala mwonyaji. Basi amekwshawafikia mtoaji bishara na mwonyaji. Mwenyezi Mungu hakuwaachia hoja wala udhuru. Aya hii iko katika maana ya (4:165)

Na Mwenyezi Mungu ni Muweza juu ya kila kitu Anaweza kumnusuru Muhammad (**s.a.w.w**) na kuliweka juu neno la Uislamu, hata kama Mayahudi na Wakristo watapinga.

TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

﴿وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِقَوْمِهِ يَا قَوْمَ اذْكُرُوا نِعْمَةَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ جَعَلَ فِي كُمْ أَنْبِيَاءَ وَجَعَلَكُمْ مُّلُوّگاً وَآتَكُمْ مَا لَمْ يُؤْتِ أَحَدًا مِّنَ الْعَالَمِينَ﴾

20. Na pale Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, alipowafanya manabii kati yenu, na akawafanya watawala, na akawapa ambayo hakuwapa wowote katika walimwengu.

﴿يَا قَوْمَ ادْخُلُوا الْأَرْضَ الْمُقَدَّسَةَ الَّتِي كَتَبَ اللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَرْتَدُوا عَلَى أَذْبَارِكُمْ فَتَنَقَّلُوا بِرِّ الْخَاسِرِينَ﴾

21. Enyi watu wangu ingieni katika ardhi takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amewaandikia, Wala msirudi nyuma msije mkawa wenyewe kuhasirika.

﴿قَالُوا يَا مُوسَى إِنَّ فِيهَا قَوْمًا جَبَارِينَ وَإِنَّا لَنْ نَدْخُلَهَا حَتَّىٰ يَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِنْ يَخْرُجُوا مِنْهَا فَإِنَّا ذَاهِلُونَ﴾

22. Wakasema: Ewe Musa huko kuna watu majabari, Nasi hatutaingia huko mpaka watoke, Wakitoka huko basi tutaingia.

﴿قَالَ رَجُلَانِ مِنَ الَّذِينَ يَخَافُونَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمَا ادْخُلُوا عَلَيْهِمُ الْبَابَ إِذَا دَخَلْتُمُوهُ فَإِنَّكُمْ غَالِبُونَ وَعَلَى اللَّهِ فَتَوَكَّلُوا إِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِينَ﴾

23. Wakasema watu wawili, mionganini mwao wale wanaomwogopa (Mwenyezi Mungu), ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha: Waingilieni kwa mlangoni; mtakapowaingilia hapo, kwa hakika mtashinda. Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni waumini.

﴿قَالُوا يَا مُوسَى إِنَّا لَنْ نَدْخُلَهَا أَبَدًّا إِمَّا ذَامُوا فِيهَا فَادْهَبْ أَنَّتَ وَرَبُّكَ فَقَاتِلَا إِنَّا هَاهُنَا قَاعِدُونَ﴾

24. Wakasema: Ewe Musa! Sisi hatutaingia kabisa maadamu hao wamo humo, Basi nenda wewe na Mola wako mkapigane, sisi tutakaa hapa.

﴿قَالَ رَبِّي لَا أَمْلِكُ إِلَّا نَفْسِي وَأَنْجِي فَأُفْرُقُ بَيْنَنَا وَبَيْنَ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ﴾

25. Akasema: Ewe Mola wangu! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu; basi tutenge na watu hawa mafasiki

﴿قَالَ فَإِنَّهَا مُحَرَّمَةٌ عَلَيْهِمْ أَرْبَعِينَ سَنَةً يَتَبَعُونَ فِي الْأَرْضِ فَلَا تَأْسَ عَلَى الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ﴾

26. Akasema: Basi wameharamishiwa (ardhi) hiyo kwa miaka arubaini, watatangatanga ardhini, Basi usiwasikitikie watu mafasiki.

MUSA NAWATU WAKE

Aya 20 - 26

MAANA

Aya hizi ni sehemu ya mfululizo wa kisa cha wana wa Israil ambacho Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekitaja sehemu mbali mbali katika Sura za

Qur'an, Baadhi ya sehemu za kisa hicho amezirudia. Nazo, kama unavyoziona, maana yake yako dhahiri.

Na pale Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, alipowafanya manabii katyenu, na akawafanya watawala na akawapa ambayo hakuwapa wowote katika walimwengu.

Musa aliwakumbusha neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yao, kama utangulizi wa atakayowaamrisha - Jihadi. Alizihesabu neema hizo kuwa ni tatu:

Kwanza: kuwa Mwenyezi Mungu amewafanya mitume katika wao.

Pili: amewafanya wajitawale, wako huru wanajitawala wenyewe; hakuna neema kubwa kama uhuru.

Tatu: kuwa aliwafanya mambo ambayo hakumfanya mtu yejote: Aliwaangamiza adui yao bila jihadi wala kupigana; akawateremshia Manna na Salwa bila ya kulima wala kuvuna; akawatolea maji safi kutoka kwenye jiwe bila ya kufukua wala kuchimba; na akawafunika na kiwingu bila ya kujenga wala tabu yoyote.

Neema hizo tatu, zatupa tafsir ya kauli yake Mwenyezi Mungu:

﴿يَا بَنِي إِسْرَائِيلَ اذْكُرُوا نِعْمَتِ اللَّهِ الَّتِي أَنْعَمْتُ عَلَيْكُمْ وَأَنِّي فَضَّلَّتُكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ﴾

"Enyi wana wa Israil! Kumbukeni neema zangu nilizowaneemesha na nikawatukuza kuliko viumbe wengine" (2:47)

Kutukuzwa kwa watu wa wakati wao kulikuwa ni kwa kutumwa mitume kutokana na wao, kuwa huru, kuteremshiwa Manna na Salwa na mengineyo. Kwa maneno mengine kufadhilishwa kulikuwa hakukuwa ni kwa hulka na sifa, bali kulikuwa ni kwa namna walivyofanyiwa.

Enyi watu wangu! Ingieni katika hiyo ardhi takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amewaandikia, wala msirudi nyuma msije mkawa wenye kuhasirika.

Baada ya Musa kuwakumbusha neema ya Mwenyezi Mungu juu yao, aliwaamrisha kuipigania Palestina, na humo walikuwa na Waithi na Wakanaani, akawaamrisha kuwa na uvumiliivu na uthabiti katika vita; Mwenyezi Mungu alikuwa amewaahidi kukaa hapo wakati huo. Kwa hiyo kauli ya Musa: "Ambayo Mwenyezi Mungu amewaandikia," ni kuashiria ahadi hiyo, na wala sio maana yake kuwa Palestina ni milki yao kabisa kama wanavyodai Mayahudi.

Hata hivyo watu wake walimwambia kwa woga na udhaifu: "Ewe Musa! Huko kuna watu majabari, Nasi hatutaingia huko mpaka watoke, Wakitoka huko basi tutaingia" Wanataka ushindi rahisi na wa raha, usiowalazimisha kuuliwa wala kujeruhija; sawa na alivyoangamizwa adui yao Firaun.

Lakini kulikuwa na watu wawili katika wao waliosimama kuwaongoza wakiwahimiza kusikiliza na kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Ndio aliowaashiria Mwenyezi Mungu kwa kauli yake:

Wakasema watu wawili, mionganoni mwao wale wanaomwogopa (Mwenyezi Mungu), ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha: Waingilieni kwa mlangoni; mtakapowaingilia hapo, kwa hakika mtashinda. Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni waumini.

Yaani washambulieni ndani ya majumba yao watadhalilika na kuvunjika nguvu, huku mkiwa mnamatgeemea Mungu kikweli kweli, kama ilivyo kwa

waumini wenyе ikhlasi. Lakini wao walirudia kwenye umbile lao la inadi na jeuri za kujiona, wakasema:

Ewe Musa! Sisi hatutaingia humo kabisa maadam wao wamo humo, Basi nenda wewe na Mola wako mkapigane, sisi tutakaa hapa.

Je, umeuona ufidhuli wao kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake? Ni Mola wao pale palipo na masilahi yao ya kiutu, ikiwa hatawakalifisha na jambo litakalo wahangaisha na ikiwa atawaua maadui zao huku wenyewe wamekaa wakiwa salama.

Ama akiwaambia litakalowahangaisha hata kwa taklifa ndogo tu, basi huyo ni Mola wa Musa, na wala si Mola wao. Maana yake nikuwa matamanio yao peke yake ndiyo Mungu wao na Mola wao anayestahiki kuabudiwa na kutakaswa. Kwa kweli hali hii haihusiki na Mayahudi tu peke yao, bali inamchanganya kila anayemwabudu Mwenyezi Mungu nchani; na ni wengi katika Waislamu na Wakristo.

Akasema: Ewe Mola Wangu! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu.

Huu ni mwelekeo kutoka kwa Musa kwa Mola wake akieleza masikitiko kwa kutengwa kwake na watu wake baada ya juhudhi kubwa na taabu nyingi kwa ajili yao. Mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu; hakuna milki wala amri kwa asiyetiiwa.

Basi tutenge na hawa watu mafasiki.

Musa akawa hana budi kumwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu awatenge yeeye na watu wake baada ya kuvunja kwao ahadi ya Mwenyezi Mungu.

Akasema: Basi wameharamishiwa (ardhi) hiyo kwa miaka arubaini, watatangatanga ardhini, Basi usiwasikitikie watu mafasiki.

Hayo ndiyo malipo yao: Kutangatanga katika jangwa la Sinai lisilo kuwa na chochote, watembea humo bila ya kujua njia ya kutokea na wapi pa kwenda. Watakuwa hivi miaka arubaini mpaka wakubwa wao waishe na kinyanyukie kizazi kingine kipyा.

﴿وَأَنْلَى عَلَيْهِمْ نَبَأً أَبْيَهُ آدَمٌ إِلَّا لَحْقِي إِذْ قَرَبَا قُرْبًا فَتَقْبَلَ مِنْ أَحَدِهِ مَا وَلَمْ يُتَقْبَلْ مِنَ الْآخَرِ قَالَ لَأَقْتُلَنَّكَ قَالَ إِنَّمَا يَتَقْبَلُ اللَّهُ مِنَ الْمُتَقْبِلِينَ﴾

27. Na wasomee habari za watoto wawili wa Adam kwa ukweli, walipotoa Sadaka, ikakuba liwa ya mmoja wao, na ya mwingine haikukubaliwa. Akasema: Nitakuua! Akasema: Mwenyezi Mungu huwapokelea wamchao tu.

﴿لَئِنْ بَسَطَ إِلَيَّ يَدَكَ لِتَقْتُلَنِي مَا أَنَا بِبَاسِطٍ يَدِي إِلَيْكَ لِأُقْتَلُ ثُلَكَ إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ رَبَّ الْعَالَمِينَ﴾

28. Kama utaninyoshea mkono kuniua, mimi sitakunyoshea mkono wangu kukuua. Hakika mimi namwogopa Mola wa walimwengu.

﴿إِنِّي أُرِيدُ أَنْ تَبُوءَ بِإِثْمِي وَإِثْمِكَ فَتَكُونُ مِنْ أَصْحَابِ النَّارِ وَذَلِكَ جَزَاءُ الظَّالِمِينَ﴾

29. Mimi nataka ubebe dhambi zangu na dhambi zako; na kwa hivyo uwе mionganı mwa watu wa motoni, Na hayo ndio malipo ya madhalimu.

﴿فَظَوَّعْتُ لَهُ نَفْسُهُ قَتْلُ أَخِيهِ فَقَتَلَهُ فَأَصْبَحَ مِنَ الْخَاسِرِينَ﴾

30. Basi nafsi yake ikamfanya kumwua ndugu yake, akamwua; na akawa mionganoni mwa wenyewe kuhasirika.

﴿قَبَعَ اللَّهُ عَزَّلَهُ يَنْحُثُ فِي الْأَرْضِ لِيُرِيهُ كَيْفَ يُوَارِي سَوْءَةَ أَخْيَهُ قَالَ يَا وَيْلَكَ أَعْجَزْتُ أَنْ أَكُونَ مِثْلَ هَذَا الْغُرَابِ فَأُوَارِي سَوْءَةَ أَخِي فَأَصْبَحَ مِنَ النَّادِمِينَ﴾

31. Hapo Mwenyezi Mungu akamleta kunguru anayefukua katika ardhi, ili amwonyeshe jinsi ya kuisitiri maiti ya ndugu yake. Akasema: Ole wangu! Nimeshindwa kuwa sawa na kunguru huyu na kuficha maiti ya ndugu yangu? Basi akawa mionganoni mwa wenyewe kujuta.

QABIL NA HABIL

Aya 27 - 31

MAANA

Wasimulizi wa visa na wafasiri wengi wamesimulia ngano za kisa cha watoto wawili hawa wa Adam. Lakini hakuna rejea zozote za visa hivyo ila ngano za Kiisrail.

Sisi tutafupiliza yale yanayofahamika kutokana na Aya, kama ifuatayo:- Watoto wawili kutoka katika mgongo wa Adam moja kwa moja, kama inavyoonyesha, walizozana. Mwenyezi Mungu (s.w.t) hakutaja wazi majina yao, lakini wafasiri na wanahistoria walisema kuwa jina la muuaji ni Qabil na la aliyeuawa ni Habil.

Sababu ya mzozo ni kuwa kila mmoja wao alitoa sadaka. Mwenyezi Mungu Mtukufu akakubali sadaka ya Habil na kuikataa ya Qabil. Qur'an haikutaja aina ya sadaka wala aina ya kuikubali na kuikataa.

Qabil akamwonea kijicho nduguye na akatishia kumuua. Habil akamwambia wewe mwenyewe ndiwe mwenye kosa mimi sio wa kulaumiwa, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu anakubali wanaomcha na wewe si katika wao. Na kama unataka kuniua basi mimi sitakukabili kukuua; dhambi za kuniua na za kuacha kukubaliwa sadaka yako zitakutosha.

Hata hivyo maneno haya hayakuathiri nafsi ya Qabil, bali yalizidisha kijicho chake; na akatekeleza makusudio yake, Baada ya ndugu yake kuwa mfu, hakujua namna ya kumsitiri. Ndipo Mwenyezi Mungu akampelekea kunguru akachimbua shimo kwa miguu yake na mdomo wake. Baada ya muuaji kuona vile, Mushkeli wake ukaondoka, akapata mwongozo wa kumzika ndugu yake, kutokana na kazi ya kunguru. Naye akauma vidole kwa majuto ya kufanya dhulma kama ambavyo alijiona yeeye anashindwa na kunguru kwa maarifa.

Huu ndio ufupi wa kisa kama kilivyofahamika kutokana na Aya. Kwa mnasaba huu ni vizuri kuelezea kuhitalifiana kuliko maarufu sana baina ya maulama wa maadili, tangu zamani, kuwa je, mtu ni mshari kwa asili na ni mwenye heri kwa asili? Wafasiri wamejaribu kukitolea dalili kisa hiki kuwa ni mshari kwa asili.

Ilivyo hasa ni kuwa kila mtu ana mwelekeo wa heri na shari kwa maumbile yake; hata yule mbora wa wabora na mshari wa washari. Tofauti ni kuwa baadhi ya watu wana akili thabiti iliyo imara au dini yenye nguvu itakayowafunga kupupia shari. Na wengine wanasukumwa na matamanio kwa udhaifu katika dini yao au akili yao.

﴿مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ كَتَبْنَا عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنَّهُ مَنْ قَتَلَ نَفْسًا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِي الْأَرْضِ فَكَانَتْنَا قَاتِلَ النَّاسَ جِمِيعًا وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَانَ مَا أَحْيَا النَّاسَ جِمِيعًا وَلَقَدْ جَاءَهُمْ رُسُلُنَا بِالْبَيِّنَاتِ ثُمَّ إِنَّ كَثِيرًا مِّنْهُمْ بَعْدَ ذَلِكَ فِي الْأَرْضِ لَمُسْرِفُونَ﴾

32. Kwa ajili ya hayo tukawaandikia wana wa Israil ya kwamba atakayeua nafsi isiyoua nafsi au kufanya ujisadi katika ardhi, basi ni kama amewaua watu wote. Na mwenye kuiacha hai ni kama amewaaacha hai watu wote. Hakika waliwafikia mitume wetu kwa hoja zilizo wazi; kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika ardhi.

MMOJA NA WENGI

Aya 32

MAANA

Kwa ajili ya hayo tukawaandikia wana wa Israil

Kisa cha watoto wawili wa Adam kimefichua kuwa watu ni aina mbili; mkosa na mwenye kukosewa. Kwa sababu ya kuhami mwenye kukosea, na kuchunga maisha na nidhamu yake, Mwenyezi Mungu amejaalia kila mkosa na adhabu yake anayostahili; akazingatia kuuwa wasio na hatia ni kosa ya makosa yote.

Kauli yake Mwenyezi Mungu: **Kwa ajili ya hayo**, ni ishara ya kosa la kuuwa kama liliivo na wala sio ishara ya kisa cha Qabil na Habil; ingawaje hicho ndiyo sababu ya sharia hiyo; sawa na inavyotunga sharia serikali kwa sababu ya tukio fulani.

Unaweza kuuliza: Adhabu ya kuua inawaenea watu wote, sasa kuna makusudio gani ya kuwalhusu wana wa Israil?

Jibu: Ni kweli kuwa adhabu hii inawalusu watu wote, lakini Mwenyezi Mungu (s.w.t) amehusisha kuwataja Mayahudi, kwa sababu wao ndio wanaouwa zaidi waja wake na kumwaga damu zao. Taurat yao inashuhudia hilo kwa kuwalalishia kuua wanawake na watoto, na historia yao inashuhudia kuua kwao mitume hapo zamani na pia historia yao ya sasa huko Palestina.

Ya kwamba atakayeua nafsi isiyoua nafsi au kufanya ujisadi katika ardhi.

Yaani inajuzu kisheria kumwua aliyeua mtu kwa uadui; vile vile inajuzu kumwua mwenye kufanya ujisadi katika nchi. Ni malipo yenyе kulingana na ni kuchunga maisha ya watu na usalama wao.

Ama mwenye kumuua mtu asiyekuwa na hatia **basi ni kama amewaua watu wote.**

Wametofautiana wafasiri na wasiokua wafasiri katika wajihii wa kufananisha kuuwa mtu mmoja na watu wote, na kumwacha hai ni kama kuwaacha hai watu wote. Kuna mwenye kusema hilo ni sisitizo la kukanya kosa la kuua na kuhimiza kuiokoa nafsi na kuiepusha na maangamizo, kama vile moto n.k.

Mwingine naye akasema, hiyo ni kubainisha hakika ya muuaji, kwamba mwenye kuweza kuua mtu mmoja basi anaweza kuua watu wengi; sawa na kusema: "Anayeiba yai ataiba ngamia."

Na kwamba mwenye kumfanyia hisani mtu mmoja basi anaweza kuwfanyia wote, Wengine wamesema, hiyo ni kubainisha tabia ya watu

kwamba tabia inakuwa sawa tu, haizidi kwa wingi wa watu wala haipungui kwa uchache wao.

Tulivyofahamu sisi kutokana na Aya ni kuwa mtu mmoja katika mtazamo wa Kiislamu ndio lengo na wala sio nyenzo ya kumfikia mwagine; na kwamba yeze ndio dhahiri ya ubinadamu. Anastahiki yanayostahiki ubinadamu - heshima na karama. Kumfanyia makosa yeze ni kuufanyia makosa ubinadamu ambao unakuwa kutokana naye na watu wote; na kumfanyia wema yeze ni kuwafanyia wema watu wote.

Unaweza kuuliza: Huku si kukazia mawazo kwa mtu mmoja na kujitolea mhanga watu wengi kwa ajili ya mtu mmoja; ambapo sawa ni kuwa kinyume cha hivyo?

Jibu: Makusudio sio masilahi ya mtu mmoja ambayo yanaingilia masilahi ya wengi wala si ya mtu ambaye anajaribu kuishi kwa gharama ya wengine. Huyu haisabiwi kua ni mtu kwa maana yake sahih; bali yeze ndiye adui zaidi wa utu katika mtazamo wa Kiislamu.

Ndipo Mwenyezi Mungu akaashiria kwa kusema: "**au ufisadi katika nchi.**" Makusudio hasa ni mtu mmoja ambaye anayatengeneza masilahi yake na masilahi ya wengi, na anayeona kuwa maisha yake ndiyo maisha ya wote na heshima yake ni ya wote.

Kama ambavyo masilahi ya wote ni masilahi ya mtu mmoja mmoja, kwa sababu wote sio ndege bali wote ni mtu mmoja mmoja. Kundi lolote likiwa na mnyonge asiye na haki basi lote litakuwa ni nyonge, na limeharibika; sawa ulivyo mwili, kama kiungo chake kimoja kikiharibika, au nyumba ikivunjika moja ya nguzo zake. Kwa hali hii ndipo masilahi ya mmoja na wote, yatakuwa yamekamilika.

Hakika waliwafikia mitume wetu kwa hoja zilizo wazi; kisha wengi katika wao baada ya haya wakawa waharibifu katika ardhi.

Yaani mitume waliwafikishia Mayahudi hukumu ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) na kuwazungumzia kwa wahyi utakao kwake Mungu, kuwa kuua mtu asiye na hatia ni kama kuua watu wote, lakini Mayahudi hawakujali tahadhari hii, na wakaendelea kufanya ufisadi wa kumwaga damu na kuwavunjia watu heshima.

Kauli yake Mwenyezi Mungu baada ya haya ni ishara kuwa waliyafanya waliyoyafanya baada ya kusimamisha hoja na kuondoka nyudhuru zote za kuweza kusamehewa. Huu ndio msimamo wa Qur'an kwa kila mpinzani, inahojiana naye kwa mantiki ya haki na kumlingania kwa hekima, hata kama atang'ang'ania upinzani wake. Utakuwa ni wa kuipinga haki tu, sio kumpinga mwenye kulingania.

TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

﴿إِنَّمَا جَزَاءُ الَّذِينَ يُحَارِبُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَسْعَوْنَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا أَن يُقَتَّلُوا أَوْ يُصَلَّ بُوَا أَوْ تُفْعَلَ أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُمْ مِنْ خَلَافٍ أَوْ يُنْفَوْ مِنَ الْأَرْضِ ذَلِكَ لَهُمْ حِزْبٌ فِي الدُّنْيَا وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ﴾

33. Hakika malipo ya wale wanaopigana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kufanya ujisadi katika ardhi, ni kuuawa au kusulubiwa au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho au kuhamishwa katika nchi. Hii ndiyo fedheha yao katika dunia, na Akhera watapata adhabu kubwa.

﴿إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِنْ قَبْلِ أَن تَقْدِرُوا عَلَيْهِمْ فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

34. Ila wale waliotubia kabla hamjawatia nguvuni. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni mwangi wa maghfira, mwenye kurehemu.

MALIPO YA UFISADI

Aya 33 - 34

MAANA

Hakika malipo ya wale wanaopigana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kufanya ujisadi katika ardhi.

Makusudio ya kupigana vita na Mwenyezi Mungu na Mtume wake, ni kuwafanya uadui watu. Kwani kuwafanya uadui watu ndiko kumfanya uadui Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Kwa sababu hii, ndipo ikawa adhabu yake ni haddi¹ katika haddi za Mwenyezi Mungu.

Makusudio ya mwenye kufanya ujisadi, ni kila mwenye kuchomoa silaha kwa ajili ya kuwashofisha watu kwa kupiga, kuuwa, kunyan'ganya au kuvunja heshima. Iwe kwa Mwislamu au asiyekuwa Mwislamu, bara au baharini, usiku au mchana na mjini au porini. Iwe ni kwa upanga, bastola, fimbo au jiwe, mradi tu ikiwa ni kuchafua amani ya watu wenye, mali zao au heshima yao.

Kosa hili linazalisha makosa mengi; kama kuvuruga amani, kudharau sharia, kumwaga damu, kunyakua mali na hata kuvunjia heshima. Kwa ajili hiyo ndio Mwenyezi Mungu akafanya malipo yake, ni yale aliyoeleza kwa kusema kwake:

Ni kuuawa au kusulubiwa au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho au kuhamishwa katika nchi. Hii ndiyo fedheha yao katika dunia na Akhera watapata adhabu kubwa.

Aya imeeleza adhabu nne.

1. Kuua. Kumeelezwa kwa tamko la kusisitiza, kwa maana ya kuwa ni lazima. Lau kama jambazi ataua mtu; kisha wasimamizi wa aliyeuawa wakasamehe, basi msamaha huo hauzingatiwi. Aliulizwa Imam Jafar as-Sadiq ^(a.s) unaonaje, ikiwa wasimamizi wa aliyeuawa wakichukua fidia na kumwaacha, itafaa? Akasema: **La, ni lazima auawe.**

1 Ni kiwango fulani cha adhabu kilichowekwa na sharia

2. Kusulubiwa msititizo wake ni kama katika kuuliwa. Namna yake ni maarufu kwa watu.

3. Kukatwa mikono na miguu kwa mabadilisho; yaani ukikatwa mkono wa kushoto, utakatwa mguu wa kulia. Usisitizo wake ni zaidi kuliko usisitizo wa kuuwa na kusulubu, Kwa sababu ya kukaririka kukata.

4. Kuhamishwa mji ulio mbali na mji wake, ambapo atahisi ugeni na kufukuzwa. Abu Hanifa anasema makusudio ya kuhamishwa ni kutiwa jela. Mwenye Al-Manar ameeleza juu ya kauli hii kwa kusema: "Hii ni kauli ya kustaajabisha sana."

Madhehebu yametofautiana katika utekelezaji wa hukumu hizi. Je zitatekelezwa kwa hiyari (kuchagua yoyote) au ni kuangalia kiasi cha kosa na adhabu yake inayolingana.

Shia Imamiya wamesema kuwa neno au kwa dhahiri linafahamisha hiyari. Kwa hiyo ataachiwa hakimu kutekeleza lile litakaloondoa ujisadi na litakalo kuwa na masilahi katika kuuwa, kusulubu, kukata au kuhamisha. Kauli hii iko karibu na ya Malik.

Shafii amesema kuwa: adhabu hii itatofautiana kulingana na kosa. Mwenye kuua tu atauawa, mwenye kuuwa na kuchukua mali atauliwa na kusulubiwa baada ya kuuwa kwa siku tatu. Mwenye kuchukua mali tu bila ya kuua, atakatwa kwa mabadilisho, mwenye kuwatisha wapita njia tu, bila ya kuua au kuchukua mali, atahamishwa.

Hanafi amesema kuwa akichukua mali na kuua, basi hakimu atakuwa na hiyari, akitaka atamkata kwa mabadilisho au amuuwe bila ya kumsulubu, na akitaka anaweza kumuwa na kumsulubu. Namna ya kusulubu, ni kusulubiwa akiwa hai na tumbo lake litatobolewa kwa mkuki mpaka afe; na hatasulubiwa zaidi ya siku tatu.

Ila wale waliotubia kabla hamjawatia nguvuni. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghfira mwenye kurehemu.

Akitubia mkabaji watu njiani yeye mwenyewe kabla ya kushikwa, basi adhabu imemwondokea; kwa sababu hekima ya adhabu ni funzo la kutofanya tena, Kwa hiyo, akijizua itakuwa hakuna wajibu uliobakia. Na huu ni ukweli wa mfano wa ubinadamu ulioko katika sharia za kiislamu.

Kwa hakika ni kuwa toba kabla ya kutiwa nguvuni mwenye hatia, inamwondolea adhabu tu, lakini haki ya watu ni lazima ailipe. Akinyanganya mali, basi ni lazima airejeshe au thamani yake au mfano wake akiwa ameiharibu. Na kama akiuwa, basi ni juu ya wasimamizi wa aliyeuawa kumuua wakitaka.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَابْتَغُوا إِلَيْهِ الْوَسِيلَةَ وَجَاهُدُوا فِي سَبِيلِهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ﴾

35. Enyi mlionamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kumfikia mfanye juhudhi katika njia yake ili mpate kufaulu.

﴿إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْأَنَّ لَهُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَيِّعاً وَمَثْلَهُ مَعَهُ لَيَفْتَدُوا بِهِ مِنْ عَذَابٍ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مَا تُقْبِلُ مِنْهُمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ﴾

36. Hakika wale waliokufuru lau wangkuwa na yote yaliyomo duniani, na mengine kama hayo, ili watoe fidia ya kuepukana na adhabu ya siku ya Kiyama, yasingelipokelewa kwao; na wana wao adhabu iumizayo

﴿يُرِيدُونَ أَنْ يَخْرُجُوا مِنَ النَّارِ وَمَا هُمْ بِخَارِجِينَ مِنْهَا وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيمٌ﴾

37. Watataka watoke motoni, lakini hawatatoka humo, na wana wao adhabu inayodumu.

TAFUTENI NJIA YA KUMFIKIA

Aya 35-37

MAANA

Enyi mliaoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na tafuteni njia ya kumfikia na mfanye juhudhi katika njia Yake ili mpate kufaulu.

Kumcha Mwenyezi Mungu, kutafuta njia ya kumfikia (wasila) na kufanya juhudhi katika njia Yake yote haya ni ibara yenye maana moja au ni maana yanayooana, kwa sababu kumcha Mwenyezi Mungu ni kuacha machukivu yake na kutafuta njia ya kumfikia ni kupata radhi zake.

Na juhudhi inakusanya yote mambo mawili, Njia bora ya kumfikia Mwenyezi Mungu ni kuwapenda watu na kuwahudumia.

Niliwahi kusoma maneno kwenye Kitabu kimoja kikubwa yanayosema: "Ni muhali kwa asiyependa watu kujua hakika ya watu." Nasi tunaongezea: "Ni muhali kumpenda Mungu kwa asiyependa watu"

Hakika wale waliokufuru lau wangkuwa na yote yaliyomo duniani, na mengine kama hayo, ili watoe fidia ya kuepukana na adhabu ya siku ya Kiyama.

Mtu anajitolea milki yake yote ili apone ugonjwa na maumivu katika maisha haya; je kwa moto wa Jahannam itakuwaje.

Yasingelipokelewa kwao; na wana wao adhabu iumizayo.

Anakubali fidia yule anayehitajia, Na ni vya Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na ardhini, sasa anahitajia nini.

Watataka watoke motoni, lakini hawatatoka humo, na wana wao adhabu inayodumu.

Hii ni kauli wazi ya mkato kuwa mwenye kumpinga Muumba au akamwabudu mwininge, atakaa milele motoni. Aya nyingine inasema:

﴿كُلَّمَا أَرَادُوا أَن يَخْرُجُوا مِنْهَا أُعِيدُوا فِيهَا وَقِيلَ لَهُمْ دُوْقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّذِي كُنْتُمْ بِهِ تُكَدِّبُونَ﴾

"Kila watakapotaka kutoka humo watarudishwa mumo humo na wataambiwa: Onjeni adhabu ya moto ambayo mlikuwa mkiikadhibisha" (32:20)

Kuna makosa mengine ambayo hayatofautiani na kumkufuru Mwenyezi Mungu kwa dhambi na adhabu; kama vile kunyan'ganya vyakula vya umma na nyenzo za maisha na kuua.

﴿وَالسَّارِقُ وَالسَّارِقَةُ فَاقْطُعُوا أَيْدِيهِمَا جَزَاءً بِمَا كَسَبُا نَكَالًا مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ﴾

38. Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao; ni malipo ya yale waliyoyachuma. Ndiyo adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu mwenye hekima.

﴿فَمَنْ تَابَ مِنْ بَعْدِ ظُلْمِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّ اللَّهَ يَتُوبُ عَلَيْهِ إِنَّ اللَّهَ عَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

39. Mwenye kutubia baada ya dhuluma yake na akatengenea, basi hakika Mwenyezi Mungu atapokea toba yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwangi wa maghfira mwenye kurehemu.

﴿أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ يُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ وَيَغْفِرُ لِمَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ﴾

40. Je, hujui kuwa Mwenyezi Mungu ana ufalme wa mbingu na ardhi? Humwaadhibu amtakaye na humsamehe amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni muweza juu ya kila kitu.

MWIZI MWANAMUME NAMWANAMKE IRABU

Aya 38 – 40

IRABU

Dhahiri ya neno 'Mikono yao' ni kuwa mikono yote miwili ikatwe, lakini dhahiri hii inaachwa kutokana na Hadith na Ijmai, kama ambavyo ujumla wa mwizi mwanamume na mwizi mwanamke unaachwa.

MAANA

Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao ; ni malipo ya yale waliyoyachuma. Ndiyo adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu.

Makusudio ya adhabu, ni adhabu ya duniani. Kadiri zitakavyotofautiana sharia za Mwenyezi Mungu na za duniani katika kupinga aina ya kosa na adhabu na sharti za kuitekeleza, lakini zitaafikiana kuwa lengo ni kumkanya mkosaji kwa kuchunga amani na masilahi.

Imam Ali ^(a.s) anasema: "**Watawala ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu, wa kukingga aliyyaharamisha katika ardhi yake**" Wala haitiliwi manani kauli ya baadhi ya mafakihii kuwa lengo la adhabu, ni kuondoa adhabu ya akhera tu. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu ni mwangi wa rehema na mwadilifu wa kukuchanganya adhabu mbili kwa kosa moja.

Kukatwa mkono kuna masharti yafuatayo:-

1. Chenye kuibwa kiwe katika hifadhi na mwizi akitoe humo. Kwa mfano; mtu akiiba gari iliyofungwa ndani ya gereji, atakatwa na kilichoibwa kitarudiswa kwa mwenyewe. Na mwenye kuiba njiani au isiyofungwa ndani ya gereji, basi hakatwi mkono, bali ataaziriwa kwa namna atakayoona hakimu (kadhi) na kilichoibwa kitarudi kwa mwenyewe, wala hakuna kinyume cha hivyo.

2. Wameafikiana kuwa hakuna kukatwa mkono ila kitakachozidi robo dinari. Abu Hanifa amesema, ni dinari kamili.

3. Mwizi awe ni baleghe; kutokana na Hadith: "**Imeondolewa kalamu kwa mtoto mpaka abaleghe, na kwa mwenda wazimu mpaka apone, na kwa aliylala mpaka aamke.**" Malik anasema: "Hakuna tofauti baina ya mtoto na mkubwa."

4. Mwizi awe na akili; kutokona na Hadith hiyo iliyotangulia.

5. Wameafikiana kuwa baba hakatwi mkono kwa kuiba mali ya mwanawee; kwa Hadith: "**Wewe na mali yako ni wa baba yako.**" Madhehebu manne na baadhi ya Shia wamesema kuwa: mama ni kama baba.

Hanafi, Shafi na Hambal, wamesema: hakatwi mkono mume au mke kwa kuiba mali ya mwenzake.

Malik amesema: hakatwi ikiwa ameiba ndani ya nyumba wanayoishi; vinginevyo atakatwa.

Shia wamesema: atakatwa kwa hali yoyote ile, ila akiiba posho yake na ya watoto wake.

6. Wizi usiwe katika mwaka wa njaa. Akiiba mwenye njaa chakula kwa namna ambayo amekosa budi ila kuiba, hatakatwa.

Ama namna ya kukatwa mkono, yameafikiana madhehebu manne kuwa: atakatwa kiganja kuanzia sehemu ya kiwiko.

Shia wamesema: vitakatwa vidole nya kiganja cha kulia, na kitaachwa kiganja na dole gumba. Kuna maelezo mengi yanayoambatana na utafiti huu, tunayaachia vitabu nya Fiqhi, kama vile Fiqhul imam Jafar as-Sadiq J.6.

Mwenye kutubia baada ya dhuluma yake na akatengenea, basi hakika Mwenyezi Mungu atapokea toba yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwangi wa maghfira mwenye kurehemu.

Sunni wamesema: toba ya mwizi haimuondelei haddi (adhabu).

Shia Imamiya wamesema: akitubia kabla ya kuthibiti wizi kwa hakimu, basi hana haddi. Wameafikiwa juu ya hilo.

Mwenye Tafsir Al-Manar aliyesema: "Ikiwa wizi utafananishwa na ukabaji watu njiani, basi kauli ya kuwa haddi haipo, ni dhahiri, ikiwa mwizi atatubia kabla yakufika kwa hakimu"

Wameafikiana wote kwamba toba, haiondoi haki ya mwenye kuibiwa; Kwa hiyo ni lazima mali irudishwe ikiwa ipo na irudishwe badali ikiwa haipo.

Je, hujui kuwa Mwenyezi Mungu ana ufalme wa mbingu na ardhi? Humwadhibu amtakaye na humsamehe amtakaye.

Msemo huu unaelekezwa kwa kila mwenye kuisikia Qur'an, sio kwa Mtume peke yake. Ndani yake mna ubainifu kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) ndiye aliyeumba ulimwengu na binadamu, na kwamba yeze hafanyi ila lililo na heri na masilahi kwa waja wake.

Akimwaadhibu amtakaye katika wakosaji basi amefanya hivyo kwa kumpa malezi na kuwasalimisha watu na shari yake, Na, akimsamehe amtakaye katika waja wake waliotubia, basi anafanya hivyo kumhimiza kujitengeza.

﴿يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ لَا يَجْزِنَكَ الَّذِينَ يُسَارِعُونَ فِي الْكُفْرِ مِنَ الَّذِينَ قَالُوا آمَنَّا بِأَفْوَاهِهِمْ وَلَمْ تُؤْمِنْ قُلُوبُهُمْ وَمِنَ الَّذِينَ هَادُوا سَمَاعُونَ لِلْكَذِبِ سَمَاعُونَ لِقَوْمٍ آخَرِينَ لَمْ يَأْتُوكَ يُحَرِّفُونَ الْكِلَمَ مِنْ بَعْدِ مَوَاضِعِهِ يَقُولُونَ إِنَّ أُوْتِيْتُمْ هَذَا فَخُدُوهُ وَإِنَّ لَمْ تُؤْتَهُ فَاقْحَدُوهُ وَمَنْ يُرِدِ اللَّهُ فِتْنَتَهُ فَلَنْ تَمْلِكَ لَهُ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا أُولَئِكَ الَّذِينَ لَمْ يُرِدِ اللَّهُ أَنْ يُظْهِرَ قُلُوبَهُمْ لَهُمْ فِي الدُّنْيَا خَزْيٌ وَلَهُمْ فِي الْآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ﴾

41. Ewe Mtume! Wasikuuzunishe wanaofanya haraka kukufuru mionganoni mwa wale wasemao kwa vinywa vyao, tumeamini, hali nyoyo zao hazikuamini.

Na mionganoni mwa Mayahudi kuna wasikiao sana uwongo wasikiao kwa ajili ya watu wengine wasiokufikia, wanayageuza maneno kutoka mahali mwake; wanasema: Mkipewa haya basi yashikeni, na msipopewa haya basi tahahadharini.

Na ambaye Mwenyezi Mungu anamtakia fitna huwezi kumpatia chochote mbele ya Mwenyezi Mungu

Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu hataki kuzitakasa nyoyo zao; wana fedheha duniani na Akhera watakuwa na adhabu kubwa.

﴿سَاعُونَ لِلْكَذِبِ أَكَالُونَ لِلسُّخْتِ فَإِنْ جَاءُوكَ فَاحْكُمْ بَيْنَهُمْ أَوْ أَعْرِضْ عَنْهُمْ وَإِنْ تُعِرِّضْ عَنْهُمْ فَلَنْ يَضُرُّوكَ شَيْئًا وَإِنْ حَكَمْتَ فَاحْكُمْ بَيْنَهُمْ بِالْقِسْطِ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ﴾

42. Wasikilizao sana uwongo walao sana haram. Basi wakujia, hukumu baina yao au achana nao, na ukiachana nao, hawatakudhuru na chochote. Na ukiwahukumu basi hukumu baina yao kwa uadilifu; hakika Mwenyezi Mungu anapenda wadilifu.

﴿وَكَيْفَ يُحَكِّمُونَكَ وَعِنْدَهُمُ التَّوْرَاةُ فِيهَا حُكْمُ اللَّهِ ثُمَّ يَتَوَلَّنَ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَمَا أُولَئِكَ بِالْمُؤْمِنِينَ﴾

43. Watakfanya je hakimu nao wanayo Taurat yenyehukumu za Mwenyezi Mungu? Kisha baada ya hayo wanakataa; na hao si wenye kuamini.

WASIKILIZAO SANA UWONGO

Aya 41 – 43

MAANA

Ewe Mtume! Wasikuhuzunishe wanaofanya haraka kukufuru, mionganini mwa wale wasemao kwa vinywa vyao, Tumeamini, hali nyoyo zao hazikuamini.

Huu ni msemo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake (**s.a.w.w**) akimpoza moyo na mambo ya wanafiki na Mayahudi, Kwa sababu mwisho hautakuwa wao.

Jumla hii inahusika na wanafiki. Kwa sababu kuamini kwa mdomo bila ya moyo ndiyo hakika ya hali yao.

Kukatazwa kuhuzunika ni kukatazwa na kulazimiana nako na kutoathirika nalo; Kwa sababu binadamu hana hiyari nalo, Ni nani mwenye akili anaye hiyari kujihuzunika? Lakini inabaki kutawala akilini na kwa ajili ya dini.

Mtume Mtukufu (**s.a.w.w**) anasema: "**Jicho linalia na moyo unahuzunika, wala hatusemi yanayomchukiza Mola.**"

Baada ya Mwenyezi Mungu (**s.w.t**) kutaja wanafiki aliashiria kwa Mayahudi, kwa kusema:

Na mionganini mwa Mayahudi kuna wasikiao sana uwongo, wasikiao kwa ajili ya watu wengine wasiokufikia.

Tena yamerudi mazungumzo kwa Mayahudi. Katika Aya hii kuna habari walizozitegemea wafasiri, ambazo ufupi wake ni kuwa, Taurat ilieleza wazi wajibu wa kurujumu¹ mzinifu. Ikasadifu wakati wa Mtume (**s.a.w.w**) mwanamume na mwanamke, katika mamwinyi wao, akazini.

1 Adhabu ya kupigwa mawe hadi kufa.

Baadhi ya Mayahudi wakaona uzito kumrujumu. Wakatuma ujumbe kwa Mtume kumwuliza hukumu ya mzinifu. Wakawaambia wale wajumbe, akitoa fatwa kurujumu kataeni, na akifutu vinginevyo basi kubalini.

Mtume akawapa fat-wa ya kurujumu. Wakakataa wakidai kuwa Taurat haina hukumu ya kurujumu. Alipowatolea hoja, mmoja wa maulama wao, alikiri kuwa hukumu ya Taurat ni kurujumu; sawa na alivyosema Muhammad; na kwamba Mayahudi wameihuisha hukumu ya kurujumu kwa walalahoi tu na kutandikwa viboko kwa mamwinyi.

Kwa hiyo makusudio ya 'wasikiao uwongo' ni kwamba Mayahudi wanakubali uwongo kutoka kwa wanafiki na kutoka kwa baadhi yao.

Na, makusudio ya 'wengine wasiokufikia' ni wale waliotuma ujumbe kwa Mtume na wala wasije wao wenyewe.

Wanayageuza maneno kutoka mahali mwake kwa kuweka viboko mahali pa kurujumiwa.

Maana ya jumla hii yametangulia katika kufasiri (2:75).

Na vile vile imetangulia kwa herufi katika (4:45).

Wanasema: Mkipewa haya basi yashikeni na msipopewa haya basi tahadharini.

Yaani walisema wale waliotuma ujumbe, kuwa Muhammad akifutu isivyokuwa kurujumu kubalini na akifutu kurujumu basi kataeni.

Na ambaye Mwenyezi Mungu anamtakia fitina, huwezi kumpatia chochote mbele ya Mwenyezi Mungu.

Wametofautiana wafasiri kuhusu makusudio ya fitna. Ashaira, yaani Sunni, wamesema ni ukafiri; na maana yake ni kuwa: mja ye yeyote ambaye Mwenyezi Mungu amemjaalia kuwa kafiri na mpotevu, basi hakuna yeyote awezaye kumzuia. Ashaira wamepondokea kwenye tafsiri hii, wakiongozwa na Arrazi, kwa vile wao wanajuzisha kwa Mwenyezi Mungu kumtakia mtu ukafiri na kumfanya awe kafiri, kisha amwadhibu.

Shia na Mu'tazila wamesema, makusudio ya fitna katika Aya hii ni adhabu; na maana yanakuwa ni kwamba ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumwaadhibu, basi hakuna yeyote atakayeweza kuzuwiya adhabu. Wamesema hivyo, kwa vile wao hawaoni kwa Mwenyezi Mungu amfanyie mtu jambo kisha amwadhibu nalo.

Tuonavyo sisi kuhusu tafsiri ya Aya hii ni kuwa: Mwenyezi Mungu (s.w.t) aliwakataza Mayahudi uongo, kugeuza, vitimbi na hadaa, na akawaahidi adhabu wakihalifu, lakini wao waliendelea kuwa na inadi wala hawakujali makatazo wala kinga. Ndipo Mwenyezi Mungu akaachana nao na wala asiwazuiye na fitna.

Kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu anatoa mwongozo na nasaha kwa watu, katika mambo yanayohusiana na vitendo vyao, na wala sio kuwalazimisha kwa nguvu. Hilo amelisisitiza Mwenyezi Mungu kwa kusema kwake.

Hao ndio amba Mwenyezi Mungu hataki kuzitakasa nyoyo zao.

Yaani hakutaka kuwategemezea utoharifu wa nyoyo na utakatifu wa nafsi. Bali amewahiyarisha katika hilo. Kwa kuzingatia haya, ndio imesihi kunasibisha fitna kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tumeyafafanua hayo katika kufasiri (4:88)

Wasikiao sana uwongo, walao sana haram.

Amelikariri hilo Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa kushutumu sana na kukanya sana hayo. Haramu ni mali ya haramu, kama riba na mfano wake. Kosa zaidi ya riba ni mali zinazochukuliwa na wakoloni na vibaraka wao, ili wananchi wabakie masikini na kuomba chakula kwa wale waliowanyang'anya vyakula vyao na mali zao.

Basi wakikujia, hukumu baina yao au achana nao, Na ukiachana nao, hawatakudhuru chochote. Na ukiwahukumu basi toa hukumu baina yao kwa uadilifu, Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda waadilifu.

Huu ni ubainifu wa wadhifa wa hakimu Mwislamu, akiwahukumu watesi wasiokuwa Waislamu. Wameafikiana mafakihi kuwa ikiwa si katika walio katika dhima (chini ya himaya ya Kiislamu), basi hakimu atakuwa na hiyari akitaka atawahukumu na asipotaka atakataa; ataangalia masilahi.

Na wametofautiana mafakihi, ikiwa ni katika watu walio katika dhima. Mwenye Al-Manar katika upande wa Sunni, amesema ni wajibu kwa hakimu kuwahukumu. Na wamesema mafakihi wa Kishia, bali atakuwa na hiyari akitaka atuhukumu akitaka hatawahukumu.

Na kama akiamua basi ni wajibu juu yake kuhukumu kwa hukumu ya kiislamu, si kwa hukumu ya dini yao; kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: '**Na ukiwahukumu basi hukumu baina yao kwa uadilifu.**'

Ikiwa mmoja wa mahasimu wawili ni Mwislam na mwininge si Mwislam, basi ni wajibu kwa hakimu kukubali madai na kuhukumu kama vile alivyosema Mwenyezi Mungu, kwa maafikiano ya Waislamu wote.

Watakuwayaje hakimu, nao wanayo Tawrat yenyehukumu za Mwenyezi Mungu? Kisha baada ya hayo wanakataa.

Mayahudi walitaka kuhukumiwa kwa Mtume (**s.a.w.w**) kuhusu mzinifu; alipowahukumu walikataa hukumu yake baada ya kumteua kuwa hakimu. Bora wasingemfanya hakimu tangu mwanzo.

Lakini kumkubali kuwa hakimu, kisha wakatae hukumu yake ni jambo la kushangaza. Hii ni pamoja na kuwa wao wanajua kwa yakini kuwa Mtume (**s.a.w.w**) atuhukumu kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu iliyo katika Tawrat.

Na hao si wenye kuamini.

Yaani hakuna la kushangaza katika kuikataa hukumu ya Mtume baada ya kumridhia kuwa hakimu na baada ya kuhukumu kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu.

Kwa sababu wao hawamwamini Mwenyezi Mungu wala Tawrat kwa imani ya kweli; isipokuwa wanaamini hawaa yao na matakwa yao. Na kila asiyeridhia haki na hukumu yake, basi hayuko katika imani ya kweli awe Yahudi au Mwislam.

Mwenyezi Mungu anasema:

﴿فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مَّا قَضَيْتَ وَإِنَّمُوا تَسْلِيمًا﴾

"Naapa kwa Mola wako! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye hakimu katika yale wanayohitalifiana baina yao. Kisha wasione dhiki katika nyoyo zao kwa uliyohukumu na wanyeyekee kabisa kabisa" (4:65)

﴿إِنَّا أَنْزَلْنَا السُّورَةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ يَحْكُمُ بِهَا النَّبِيُّونَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا لِلَّذِينَ هَادُوا وَالرَّبَّانِيُّونَ وَالْأَحْجَارُ بِمَا اسْتُحْفِظُوا مِنْ كِتَابِ اللَّهِ وَكَانُوا عَلَيْهِ شُهَدَاءَ فَلَا تَخْشُوَ النَّاسَ وَاحْشُوْنَ وَلَا تَشْرُوْا بِآيَاتِي شَمَنًا قَلِيلًا وَمَنْ لَمْ يَحْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَلُولَيْكَ هُمُ الْكَافِرُونَ﴾

44. Hakika tuliteremsha Tawrat yenyeye uongozi na nuru, ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha na watawa na wanazuoni, waliwahukumu mayahudi; kwani walitakiwa kukihifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi msiwaogope watu bali niogopeni mimi. Wala msiuze Aya zangu kwa thamani chache. Na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio Makafiri.

USIWAOGOPE DATU

Aya 44

MAANA

Hakika tuliteremsha Tawrat yenyeye uongozi na nuru.

Kila Kitabu alichokiteremsha Mwenyezi Mungu kwa Mitume yake, basi ni mwangaza unaoongoza kwenye haki na kheri. Tawrat ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu alichomteremshia Musa ^(a.s), ni mwongozo na nuru.

Ama Tawrat ya sasa haikutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu iko mbali na kuwa ni mwangaza na nuru na kuwa ni haki na heri.

Mafunzo yake yanasmamia ubaguzi na kugawa watu; yanawafanya Mayahudi kuwa ni taifa teule la Mwenyezi Mungu; inawahalalishia kuyapiga vita mataifa mingine, kuuwa watu, kuwachinja wanawake na watoto, kunyakuwa mali zao na kuikalia mijji yao.

Angalia Kitabu cha Waamuzi 20: 13 – 14.

Ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha na watawa na wanazuoni waliwahukumu Mayahudi; kwani walitakiwa kukihifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu.

Yaani mitume waliokuja baada ya Musa, kama vile Daud, Suleiman, Zakariya na Yahya walikuwa wakiwaongoza Mayahudi kwa hukumu ya Tawrat ambayo ni uongozi na nuru; wakiwashalalishia halali na kuwasharamishia haramu.

Kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu; 'Manabii waliojisalimisha maana yake ni kuwa mitume wa Mwenyezi Mungu walijisalimisha kwa Mwenyezi Mungu, wakawahukumu Mayahudi kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu si kwa matakwa yao wala kwa ijtihami yao au mapenzi yao; kama walivyofanya Mayahudi wakati wa Mtume, Muhammad (s.a.w.w) kumtaka awahakumie mzinifu vile watakavyo wao.

Vilevile watawa wa kiyahudi, maulama wao na makadhi wao, waumini wenyewe ikhlasi walikuwa wakihukumu yale waliyoyajua na kuyahifadhi kutoka katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu.

Nao walikuwa mashahidi juu yake.

Maana ni kuwa watawa na maulama walikuwa wakikitumia Kitabu cha Mwenyezi Mungu wala hawakipangi. Hapana mwenye shaka kuwa mwenye kuitkuza kauli na akaitumia, anakuwa ameitolea ushahidi kwa kitendo kabla ya kauli, kuwa ni haki na sawa.

Basi msiwaogope watu bali niogopeni mimi. Wala msiuze Aya zangu kwa thamani chache.

Mwenye kuijua hukumu ya Mwenyezi Mungu hawezi kuhalifu ila kwa mambo mawili. Ama kwa kuhofia cheo chake kuondoka au kuwa na tamaa ya mali. Mwenyezi Mungu ameliashiria la kwanza kwa kusema: 'Basi msiwaogope watu, bali niogopeni mimi'

Na la pili ameliashiria kwa kauli yake: 'Wala msiuze Aya zangu kwa thamani chache.' Yaani, Enyi Maulama wa Kiyahudi! Fanyeni lile mnaloliona ni haki wala msiogope lawama na wala msibadilishe kwa tamaa ya rushwa.

Ikiwa msemo huu kwa dhahiri yake unaelekezwa kwa maulama waliobadilisha hukumu ya mzinifu ya kurujumiwa kuwa ya viboko, basi kwa uhakika unamhusu kila mwenye kujaribu kugeuza kwa kuhofia au kwa tamaa.

Kwa ufasaha zaidi wa kutafsiri Aya hii ni kauli ya Ali, Amirul-muminin ^(a.s) katika kuwasifu mawalii wa Mwenyezi Mungu: "**Kwa ajili yao kimesimama Kitabu na kwa ajili ya Kitabu wamesimama, hawaoni matarajio zaidi ya wanayotarajia wala hofu zaidi ya wanayohofia**"

Yaani hawamtaraji zaidi ya Mwenyezi Mungu wala hawamwogopi isipokuwa yeeye.

Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri.

Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Aya inayofuatia hii (45) anasema: "Basi hao ndio Madhalimu," katika Aya 47, anasema: "**Basi hao ndio Mafasiki.**" Katika Aya hiyo tutabainisha kupatikana sifa ya ukafiri, dhuluma na ufasiki kwa mmoja.

TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

﴿وَكَتَبْنَا عَلَيْهِمْ فِيهَا أَنَّ النَّفْسَ إِلَيْهَا تُنْفَسُ وَالْعَيْنَ بِالْعَيْنِ وَالْأَنفَ بِالْأَنفِ وَالْأَذْنَ بِالْأَذْنِ دُنْ وَالسِّنْ بِالسِّنِ وَالْجُرُوحَ قِصَاصٌ فَمَنْ تَصَدَّقَ بِهِ فَهُوَ كَفَارَةً لَهُ وَمَنْ لَمْ يَحْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ﴾

45. Na tuliwaandikia humo ya kwamba nafsi kwa nafsi na jicho kwa jicho na pua kwa pua na sikio kwa sikio na jino kwa jino na majeraha yana kisasi, Lakini atakayesamehe, basi itakuwa kafara kwake. Na wasiohukumu kwa yale aliyyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu.

﴿وَقَفَّيْنَا عَلَى آثَارِهِمْ بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمْ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التُّورَةِ وَآتَيْنَا إِلَيْهِمْ حُكْمَهُ دَهْرِيَّ وَتُورُّ وَمُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التُّورَةِ وَهُدًى وَمَوْعِظَةً لِلْمُتَّقِينَ﴾

46. Na tukamfuatishia Isa bin Maryam katika nyao zao kuyasadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Tawrat, na tukampa Injil ndani yake mna mwongozo na nuru, na isadikishayo yaliyo kabla yake katika Tawrat, na mwongozo na mawaidha kwa wenye takua.

﴿وَلَيَحْكُمْ أَهْلُ الْإِنْجِيلِ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فِيهِ وَمَنْ لَمْ يَحْكُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

47. Na watu wa Injil wahukumu kwa yale aliyyateremsha Mwenyezi Mungu. Na wasiohukumu kwa yale aliyyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio mafasiki.

MTU KWA MTU

Aya 45 - 47

MAANA

Na tuliwaandikia humo ya kwamba nafsi kwa nafsi na jicho kwa jicho na pua kwa pua na sikio kwa sikio na jino kwa jino na majeraha yana kisasi.

Aya hii ni mionganini mwa Aya za hukumu, na maudhui yake ni kisasi, Katika Fiqh ya kiislamu kuna mlango mahsus. Hukumu hii, mtu kwa mtu, iliteremshwa katika Tawrat na sheria ya kiislamu haikuifuta. Yametangulia maelezo ya kisasi katika kufasiri (2:178)

Lakini atakayesamehe basi itakuwa kafara kwake.

Yaani mwenye kukosewa akimsamehe mkosa, basi Mwenyezi Mungu (s.w.t) ataujaalia msamaha huo ni kafara ya dhambi zake.

Na wasiohukumu kwa yale aliyyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu.

Maelezo yatakuja katika Aya inayofuatia;

Na tukamfuatishia Isa bin Maryam katika nyao zao kuyasadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Tawrat.

Dhamir katika kuwafuatishia inawarudia mitume, Yaani tulimtuma Isa baada ya mitume waliokuwa wakihukumu kwa Tawrat, na yeze akaithibitisha kwa kauli yake na vitendo vyake. Amenukuliwa katika Injil

yao kuwa yeye alisema: "Mimi sikuja kuitangua Tawrat bali nimekuja kuitimiza," (Mathayo 5:17) yaani nizidishe hukumu na mawaidha.

Na tukampa Injil, ndani yake mna mwongozo na nuru.

Ni hali ya kila Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Mitume wa Mwenyezi Mungu. Injil aliyoisifu Mwenyezi Mungu kwa uwongozi na nuru ni Injil ile iliyotamka Tawhid (umoja wa Mwenyezi Mungu), ikakanusha utatu na ikathibitishia utume wa Muhammad (**s.a.w.w**)

Na isadikishayo yaliyo kabla yake katika Tawrat.

Ambayo inaanrisha uadilifu na hisani; wala sio kuua na kunyang'anya.

Na mwongozo na mawaidha kwa wenye takua.

Unaweza kuuliza: kuwa, Mwenyezi Mungu (s.w.t) ameisifu Injil aliyoiteremsha kwa Isa kwa uwongozi na nuru; tena akaisifu mara ya pili kwa uwongozi na mawaidha kwa wamchao Mwenyezi Mungu; sasa kuna wajihii gani wa kukaririka sifa za uwongozi katika Aya moja?

Jibu: Neno mwongozo la kwanza limekuja kusifu hali halisi ya Injil hiyo yenye tu bila ya kuangalia kuitumia, na neno mwongozo la pili ni la kusifu kuitumia; yaani Injil hii atanufaika nayo na kuwaiddhika na mawaidha yake yule amchaye Mwenyezi Mungu; sawa na kusema: Ananufaika na mwangaza mwenye macho! Imam Ali ^(a.s) amesema: "**Huenda mwenye elimu akauliwa na ujinga wake na elimu anayo, isimfae kitu.**"

Tunarudia tena kuwa makusudio ya Injil katika Aya ni Injil ambayo inamwepusha Mwenyezi Mungu na mtoto na kukana Uungu wa Isa ^(a.s) na kubashiria utume wa Muhammad.

Na watu wa Injil wahukumu kwa yale aliyyateremsha Mwenyezi Mungu.

Watu wa Injil ni Wakristo, watu wa Tawrat ni Mayahudi na watu wa Qur'an ni Waislamu. Mwenyezi Mungu amememwamrisha kila mwenye dini na kuamini Kitabu katika vitabu vya Mwenyezi Mungu, basi akitumie na kushikamana na hukumu zake.

Yeyote mwenye kwenda kinyume, basi atakuwa ni mzushi mwongo, awe Yahudi, Mkristo au Mwislam, hayahu kundi fulani; wamehusishwa kutajwa watu wa Injil kwa vile mazungumzo ni yao.

UKAFIRI, UFASIKI NA DHULUMA

Na wasiohukumu kwa yale aliyyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio mafasiki.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amesema katika Aya iliyotangulia, 44: "Na wasiohukumu kwa yale aliyyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio Makafiri." Katika Aya ya 45 amesema: "Na wasiohukumu kwa yale aliyyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu." Na katika Aya hii amesema: "Na wasiohukumu kwa yale aliyyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio Mafasiki."

Sifa zote tatu zinasifu hali moja. Wafasiri wametofautiana katika wajihii na taawili; nasi tunaziacha kauli zao kwa kuepuka kurefusha kurasa.

Ama rai yetu ni kama ifuatavyo:- Hakika dini ni itikadi na sharia. Itikadi ni sifa za moyoni, nayo ina misingi yake ambayo ni kumwamini Mwenyezi Mungu na sifa zake, na kuamini Vitabu vyake, Mitume yake, Malaika wake na Siku ya Mwisho. Na sharia ni amali inayoambatana na kauli na vitendo.

Tamko la Ukafiri likitamkwa peke yake bila ya kuambatana na jingine; kama kusema: fulani ni kafiri, basi itaeleweka kuwa yeye anakana misingi ya kiitikadi yote au baadhi.

Ikisemwa: Fulani ni fasiki, itafahamika yeye anakubali dini kwa misingi yake na matawi yake, lakini anapuuza tu na kuaacha kutenda sharia zote au baadhi. Hii ni ikiwa matamko yote mawili yametajwa peke yake bila ya kutegemezwu kwenye kitu chochote. Ama ukitegemezwu ufasiki kwenye itikadi, kama kusema: Fulani ni fasiki wa itikadi, basi makusudio ya ufasiki hapo yatakuwa ni ukafiri. Hiyo imetumiwa katika Qur'an pale Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema.

﴿وَلَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ وَمَا يُكَفِّرُ بِهَا إِلَّا الْفَاسِقُونَ﴾

"Hakika tumekuteremshia ishara zilizo wazi, na hawazikufuru ila mafasiki" (2:99)

Na kama neno ukafiri likitegemezwu kwenye amali na si katika itikadi, basi makusudio yake yatakuwa ni ufasiki. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

﴿وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ عَنِّي عَنِ الْعَالَمِينَ﴾

"Na ni haki ya Mwenyezi Mungu juu ya watu kuhiji nyumba hiyo kwa mwenye kuweza njia ya kuiendea. Na atakaye kufuru basi Mwenyezi Mungu si muhitaji wa viumbe" (3:97)

Mwenyezi Mungu amemsifu na ukafiri mwenye kuacha Hijja pamoja na kuwa anaamini misingi yote. Kwa hiyo hapo makusudio ya ukafiri yanakuwa ni ufasiki.

Ama neno dhuluma, inajuzu kulitumia kwa ukafiri na ufasiki, kwa sababu kafiri na fasiki anakuwa ameihdhumu nafsi yake kwa kuitia katika adhabu jambo isiloliweza. Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema: "Na waliokufuru ndio madhalimu" (2:254)

Na akasema tena: "Na ni nani dhalimu mkubwa kuliko yule afichaye ushahidi alionao utokao kwa Mwenyezi Mungu" (2:140)

Kuficha ushahidi kwa ujumla hakuwajibishi ukafiri kwa maafikiano ya Waislamu wote.

Kwa hali hii inatubainikia kuwa ukafiri ufasiki na dhulma ni maneno yaliyokuja katika Qur'an kwa maana moja. Kwa hiyo basi, inafaa kusifiwa nayo asiyehukumu kwa aliyoiteremsha Mwenyezi Mungu.

Makusudio ni kutilia mkazo, makemeo kwa asiyehukumu kwa haki, ni sawa awe amehukumu kwa batili au aliacha kuhukumu.

Vile vile anaambiwa hayo yule aliyehukumiwa kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu akaacha kutekeleza.

Kwa mnasaba huu, tunaashiria kuwa mafakihi wameafikiana kuwa mwenye kukana hukumu ya kisharia iliyothibiti kwa Ijmai ya Waislamu wote; kama vile wajibu wa Swala na uharamu wa zina basi yeye ni kafiri; na mwenye kuihalifu lakini anaikubali, basi ni fasiki.

﴿وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحُقْقِ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ الْكِتَابِ وَمُهَمِّيَّنَا عَلَيْهِ قَاضِيَّكُمْ بَيِّنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعُ أَهْوَاءَهُمْ عَمَّا جَاءَكُمْ مِنَ الْحُقْقِ لِكُلِّ جَعْلَنَا مِنْكُمْ شُرْعَةً وَمَنْ هَاجَأَ وَلَوْ

شَاءَ اللَّهُ لَجْعَلَكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَكِنْ لَيَبْلُوْكُمْ فَإِنْتُمْ حَسِيرَاتٍ إِلَى اللَّهِ
مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٤٨﴾

48. Na tumekuteremshia Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Kitabu na kuyalinda. Basi hukumu baina yao kwa yale aliyoysteremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao kwa kuacha haki iliyokufikia. Na kila (Umma) katika nyinyi, tumeujalia sharia yake na njia yake. Na kama Mwenyezi Mungu angelitaka, angewafanya umma mmoja, lakini ni kuwajaribu katika hayo aliyowapa. Basi shindaneni katika mambo ya kheri, marejeo yenu nyote ni kwa Mwenyezi Mungu; naye atawaambia yale mliyokuwa mkihitilafiana.

﴿وَأَنِ احْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ وَامْرُّهُمْ أَنْ يَقْتُلُوكُمْ عَنْ بَعْضِ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ إِلَيْكُمْ فَإِنْ تَوَلُّوْ فَاعْلَمْ أَنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُصِيبَهُمْ بِبَعْضِ ذُنُوبِهِمْ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ لَفَاسِقُونَ ﴾

49. Na hukumu baina yao kwa yale aliyoysteremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate mapenzi yao. Nawe jihadhari nao wasije wakakutia kwenye fitna ukaacha baadhi ya yale aliyokuteremshia Mwenyezi Mungu. Na kama wakikengeuka, basi jua kwamba Mwenyezi Mungu anataka kuwasibu kwa baadhi ya dhambi zao. Na hakika wengi katika watu ni wafasiki.

﴿أَفَحُكْمُ مَا الْجَاهِلِيَّةِ يَبْعُونَ وَمَنْ أَحْسَنْ مِنَ اللَّهِ حُكْمًا لِّقَوْمٍ يُوقَنُونَ ﴾

50. Je wanataka hukumu za Kijahiliya. Na ni nani aliye mzuri zaidi kwa hukumu kuliko Mwenyezi Mungu; kwa watu wenye yakini.

KILA UMMA NA SHARIA YAKE

Aya 48 - 50

MAANA

Na tumekuteremshia Kitabu kwa haki kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake katika Kitabu na kuyalinda.

Makusudio ya Kitabu kilichotajwa kwanza ni Qur'an na Kitabu kilichotajwa mara ya pili ni jinsi ya vitabu vyote vya Mwenyezi Mungu; ikiwemo Tawrat, Injil n.k.

Baada ya Mwenyezi Mungu (s.w.t) kutaja Tawrat na Injil, na Musa na Isa ^(a.s), amefuatishia kutaja Qur'an na Muhammad (s.a.w.w).

Ameisifu Qur'an kwa sifa mbili:

Kwanza: kwamba hiyo inasadikisha vitabu vyote vilivyoteremshiwa Mitume.

Pili: kuwa ni mlinzi wa wa vitabu vilivyotangulia. Maana ya ulinzi wa Qur'an kwa Tawrat na Injil ni kwamba: inashuhudia kuwa vitabu viwili hivyo ni haki na ukweli na inatolea habari, misingi na hukumu zilizopotoshwa ndani yake, ili mtu apambanue ya asili na ya kuongezwa ambayo viongozi wa dini wameyanasibisha kwa Mwenyezi Mungu kwa uzushi na uwongo.

Basi hukumu baina yao (yaani Mayahudi) kwa yale aliyoysteremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao.

Kimsingi ni kuwa Mtume (s.a.w.w) hahukumu ila kwa haki, wala haghafiliki na dogo au kubwa, na ni muhali kufuata matamanio ya viumbe.

Vipi isiwe hivyo na kauli yake na vitendo vyake ni kipimo cha kupimia haki na uadilifu. Lau tukikadiria kutokea mlaghai anayejaribu kumhadaa Mtume kwa kujionyesha, na Mtume akurubie, kuhadaika kwa kuzingatia kuwa yeze ni mtu, basi hapo Mwenyezi Mungu (s.w.t) atamlinda kwa msaada wake na kumfahamisha haki halisi kabla ya kutokea chochote cha mlaghai. Mwenyezi Mungu anasema:

"Na kama tusingelikuimarisha ungelikuribia kuwaelekeea kidogo" (17:74)

Unaweza kuuliza: Maadamu mambo yako hivyo, kwa nini Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume wake aliye Maasum hivi?

Jibu: Kwanza, tumekwisha bainisha katika sehemu zilizotangulia kuwa maneno yakinoteka kwa mkubwa haiangaliwi hali na cheo cha anayeambwa. Hilo litaangaliwa ikiwa maneno yametoka kwa aliye sawa na anayeambwa au mdogo zaidi yake.

Pili: hakika Mwenyezi Mungu (swt) anajua kuwa maulama waovu katika umma wa Muhammad (**s.a.w.w**) wataboresha hukumu potofu kwa vijisababu vya kishetani. Ndipo akamwambia Mtume wake Mtukufu maneno haya, kumhadharisha na wanaochezea dini kwa kufuata mapenzi ya watawala.

Na kila (umma) katika nyinyi, tumeujaalia sharia yake na njia yake.

Dhamir katika nyinyi inawarejea watu wote au makundi matatu (Mayahudi, Wakristo na Waislamu). Na sharia ni hukumu za kimatendo wanazozifuata binadamu kwa kumtii Mwenyezi Mungu na kutaka radhi zake na malipo yake. Kwa hakika hasa ni kuwa neno halienei zaidi kuliko neno 'Dini', kwa sababu dini inakusanya sharia na misingi ya itikadi.

Maana ya njia, ni njia iliyowazi; yaani Mwenyezi Mungu amejaalia kila umma sharia iliyowazi isiyokuwa na mkanganyo wowote.

Aya hii, ni kauli wazi kuwa sharia ya Mwenyezi Mungu haikuwa moja kwa watu wote na wakati wote; na kwamba wakati ulioupita ilikuwa ya muda maalum; na kwamba dini zinaafikiana na kuwa moja katika misingi ya itikadi tu, si katika sharia.

Utauliza; Ikiwa mambo ni hayo, kwa nini sharia ya kiislamu imehusika na hukumu na kuendelea?

Hawezi kujua jibu la swali hili ila yule aliyesoma sharia za kiislamu, ambapo ataziona zimesimama kwenye misingi thabitii; ni muhalii kubadilika kwa kubadilika zama na hali. Kwa sababu, zinaoana na mwanadamu akiwa ni mwanadamu, si akiwa ni wa zamani au wasasa. Mfano wa hayo ni kama ifuatavyo:-

Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi ila uweza wake, 'Kila mtu ni mwema mpaka uthibiti ubaya wake.' 'Suluhu ni bora', 'Inajuzu wenye akili kujithibitisha wenyewe', 'watu wako kwenye masharti yao,' Haddi hukingwa na shubuha,' 'Hapana madhara wala kudhuriana,' 'Dharura inahalalisha haramu,' 'Yakini haivunjwi ila na yakini mwenzake.' Kinga ni bora kuliko kuponya' 'Dhara haiondolewi na dhara mwenzake,' 'Asiyekuwepo anahoja mpaka aje' na mengineyo katika misamiati ya fiqh ambayo mafakihi

wameiorodhesha katika mijalada ya vitabu nya fiqh. Kwa hiyo misingi hii ni muhali kuweza kugeuka ila litakapogeuka umbile la binadamu.¹

Na kama Mwenyezi Mungu angelitaka, angewafanya umma mmoja.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewatofautisha watu na viumbe wengine kwa kuwafanya kuwa na mwelekeo wa ujinga na ujuzi, kuwa nyuma na kuen delea na kwa kufanya heri na shari; Kisha akamkataza hili akamwamirisha lile.

Kwa hiyo natija ya mwelekeo huu, amri na makatazo, ni kutofautiana watu, katika kuutumia mwelekeo huu, na katika kumtii Mwenyezi Mungu na kumwasi.

Lau Mwenyezi Mungu angelitaka asingempa mtu kipawa hiki, na kama angelifanya hivyo, basi watu wote wangelikuwa katika hali moja tu, sawa na wanyama, ndege na wadudu, wanajiendea tu hawajui heri wala shari au kufaulu au kufeli.

Lakini ni kuwajaribu katika hayo aliowapa.

Yaani Mwenyezi Mungu ametupa kipawa hiki, akatuamrisha na kutukataza ili atufanyie mtihani: Ni nani mzuri wetu wa matendo? Ingawaje yeze anajua siri na dhamiri, lakini hamlipi mtu ila kwa amali wala hamwadhibu ila baada ya maonyo.

Basi shindaneni katika mambo ya kheri. Marejeo yenu nyote ni kwa Mwenyezi Mungu; naye ataawambia yale mliyokuwa mkihitilafiana.

Yaani akiwa Mwenyezi Mungu amempa binadamu kipawa hiki, na akaweka sharia mbali mbali kwa umma, ili yadhihirike matendo anayostahiki mtu kupata thawabu, basi ni juu yetu wote kuharakia mambo ya heri, kwa sababu ndiyo makusudio ya kwanza ya sharia. Na yeze atakayefanya tofauti za sharia ndio chombo cha kuleta chuki na uadui, basi Mwenyezi Mungu (s.w.t) kesho atamhisabu na kumlipa atakachostahiki.

Na hukumu baina yao kwa yale aliyyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate mapenzi yao. Nawe jihadhari nao wasije wakakutia kwenye fitna ukaacha baadhi ya yale aliyokuteremshia Mwenyezi Mungu.

Aya hii ni kuikariri Aya iliyoitangulia. Baadhi ya wafasiri wamesema kuwa iliyoitangulia ilishuka katika kuhukumiana Mayahudi katika zina, na hii imeshuka katika kuhukumiana katika kuua.

Lakini hakuna dalili yoyote katika mwelekeo huu wala mwengineo ulioko katika baadhi ya vitabu nya tafsir.

Tumebainisha katika kufasiri Sura (2:47) kwamba Qur'an inatumia kukaririka, kwa sababu ni njia yenye nguvu ya kueneza jambo. Zaidi ya hayo ni kwamba dhamir katika 'mapenzi yao' inawarudia Mayahudi. Ni katika njia ya Qur'an kulikariri na kulisisitiza jambo linalowahusu Mayahudi zaidi kuliko jambo jingine.

Na hii inafahamisha tu kuwa Mayahudi ni umma wa shari katika hali zote. Historia yao ya zamani na sasa inalishuhudia hilo. Hakuna yeze anayewaona kuwa si washari ila watu wa shari tu. Hakika hii imedhihirini, kwa maana yake, kwa wote baada ya tukio la 5 Juni 1967.

1 Zaidi ya hayo ni kwa kuzingatia kuwa Mtume Muhammad ni wa mwisho, hakuna mwengine atakayekuwa. Hapana budi sharia yake iwe itaendelea hadi siku ya mwisho --- Mtarjumu

Na kama wakikengeuka, basi jua kwamba Mwenyezi Mungu anataka kuwasibu kwa baadhi ya dhambi zao.

Yaani wakikengeuka na hukumu ya Mwenyezi Mungu, basi kutawaletea hizaya na balaa.

Unaweza kuuliza: kwa nini Mwenyezi Mungu amesema: "kwa baadhi ya dhambi zao" na wala asiseme 'kwa dhambi zao.' Je, hii inamaanisha kuwa Mwenyezi Mungu atawaadhibu kwa baadhi ya dhambi na nyingine atawasamehe?

Jibu: Kauli yake Mwenyezi Mungu kwa 'baadhi ya dhambi zao,' ni ishara ya kupinga kwao hukumu waliyohukumiwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (**s.a.w.w**). Maana yake ni kuwa; "Ewe Mtume! Kupinga kwa Mayahudi kusikuzuie kuhukumu, kwani Mwenyezi Mungu atawadhibu kwa dhambi yao."

Na hakika wengi katika watu ni wafasiki.

Fasiki ni yule anayemwasi Mwenyezi Mungu katika hukumu moja mionganoni mwa hukumu zake. Watu wengi wako hivi, bali ni watu wote; isipokuwa wachache lakini neno wengi hutumika katika wingi na sio kinyume.

Je wanataka hukumu za Kijahiliya?

Kila hakimu anayehalifu hukumu ya Mwenyezi Mungu, basi amehukumu hukumu za kijahiliya, awe katika wakati wa Jahiliya au baada yake.

Na ninani aliye mzuri zaidi kwa hukumu kuliko Mwenyezi Mungu, kwa watu wenye yakini.

Hapana mwenye shaka kwamba kila hukumu yenyе masilahi fulani kwa watu, basi hiyo ni hukumu ya Mwenyezi Mungu, ni sawa iwe imeelezewa na kauli wazi mahsus ya Qur'an au Hadith au iwe haikuelezea. Na kila yenyе madhara fulani kwa watu, basi Mwenyezi Mungu ni muhali kuiridhia.

Hata haki ya Mwenyezi Mungu inaondoka ikiwa italeta madhara. Inatosha kuwa ni dalili, kuwa kila hukumu inayonufaisha watu ni ya Mwenyezi Mungu, kauli yake Mwenyezi Mungu:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِبُو لِلَّهِ وَلِرَسُولِهِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحِبِّيكُمْ﴾

"Enyi mlionamini! Mwitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume wake anopowaita katika yale yatakayowapa uhai." (8:24).

Kwa sababu maana yake ni kuwa kila mwito wa uhai ni mwito wa Mwenyezi Mungu na wa Mtume wa Mwenyezi Mungu.

NAHW

wametofautiana wafasiri katika maana ya herufi 'lam' katika neno; kwa watu wenye yakini. Baadhi wamesema kuwa ni kwa maana ya mbele ya, yaani kwao watu wenye yakini. Wengine wakasema ni ya ubainifu.

Ilivyo hasa ni ya kuhusisha, kama vile kusema; Pepo ni kwa wenye kumcha Mwenyezi Mungu, kwa sababu, wenye yakini peke yao ndio wanaohukumu na kuitumia hukumu ya Mwenyezi Mungu.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَشْخُدُوا الْأَيُّهُ وَدَ وَالْتَّصَارَىٰ أُولَئِكَ بَعْضُهُمْ أَزْيَاءُ بَعْضٍ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مَنْ كُنْ فِإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ﴾

51. Enyi mlionamini! Msiwafanye kuwa marafiki Mayahudi na Manaswara; wao kwa wao ni marafiki. Na mionganoni mwenu atakayewafanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao, Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.

﴿فَتَرَى الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرْضٌ يُسَارِعُونَ فِيهِمْ يَقُولُونَ نَخْشَى أَنْ تُصِيبَنَا دَائِرَةٌ فَعَسَى اللَّهُ أَنْ يَأْتِي بِالْفَتْحِ أَوْ أَمْرٍ مِّنْ عِنْدِهِ فَيُصِبِّحُوا عَلَىٰ مَا أَسْرُوا فِي أَنْفُسِهِمْ نَادِمِينَ﴾

52. Utawaona wale wenyewe maradhi nyoyoni mwao wanakimbilia kwao wakisema: Tunaogopa yasitusibu majanga. Huenda Mwenyezi Mungu akaleta ushindi au jambo jingine litokalo kwake, wakawa wenyewe kujuta kwa yale waliyoyaificha katika nafsi zao.

﴿وَيَقُولُ الَّذِينَ آمَنُوا أَهْلُؤُلَاءِ الَّذِينَ أَفْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ إِنَّهُمْ لَمَعْكُثُمْ حَيْطَنْ أَعْمَالَهُمْ فَأَضْبَحُوا خَاسِرِينَ﴾

53. Na watasema walioamini: Hivi hawa ndio wale walioapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwa viapo vyao vigumu, ya kwamba wao wako pamoja nanyi? Zimepomoka amali zao na wamekuwa wenyewe hasara.

MAYAHUDI NAWAKRISTO MSIWAFANYE KUWA MARAFIKI

Aya 51 - 53

MAANA

Enyi mlionamini! Msiwafanye kuwa marafiki Mayahudi na Manaswara.

Neno rafiki limefasiriwa kutoka neno walii ambalo hapa lina maana ya rafiki au msaidizi, Dini ya kiislamu iko wazi kwa dini zote na jinsi zote.

Hakuna tofauti baina ya mweusi na mweupe wala baina ya mwarabu na asiyekuwa mwarabu wala baina ya Mwislamu na asiyekuwa Mwislamu katika usawa mbele ya kanuni.

Mtu yoyote, vyovoyote atakavyokuwa, ana haki ya kuishi huru na kwa amani, yeye na mali yake, Wala hakuna haja ya kumchunga yeote maadamu hawaudhi wengine.

Akikeuka mipaka na akafanya ufisadi, atahukumiwa. Mwislamu akimfanya uovu asiyekuwa Mwislamu, ni wajibu wetu sisi Waislamu kumwadhibu na kujitenga naye. Myahudi au Mkristo akiufunga mkono wake na asituudhi, basi tutamnyooshea mkono wa heri na wema, hata kama anakana utume wa Muhammad na Qur'an. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿لَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ أَنْ تَبْرُرُوهُمْ وَقُتِّلُوكُمْ إِلَيْهِمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُفْسِطِينَ ﴿٨﴾ إِنَّمَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ قَاتَلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ وَظَاهَرُوا عَلَىٰ إِخْرَاجِكُمْ أَنَّ تَوَلَّهُمْ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَلُولَتِكُمْ هُوَ مُّظَلَّمُونَ﴾

"Mwenyezi Mungu hawakatazi kuwafanya hisani na uadilifu wale ambao hawakupigana nanyi kwa ajili ya dini, wala hawakuwafukuza katika nchi zenu, Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao uadilifu.

Isipokuwa Mwenyezi Mungu anawakataza kuwafanya marafiki wale wanaopigana nanyi katika dini, na wakawafukuza katika nchi zenu na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu, na wawafanyao marafiki, basi hao ndio madhalimu" (60: 8 - 9)

Tukiziunganisha Aya hizi ambazo zimewahimiza Waislamu kuwafanyia wema na hisani watu wa mataifa yote na wa dini zote, ambao hakuwafanyia uadui Waislamu, pamoja na Aya hii tunayoifasiri, tukizichanganya katika mazungumzo mamoja, basi maana yake yanakuwa: Enyi mliaoamini! Msiwafanye mawalii Mayahudi na Wakristo, kama wakiwafanyia uadui na kuwapiga vita. Ama wakiwa na usalama, basi tangamaneni nao kwa wema.

Muishi nyote kwa kujuana na kuzoeana; bali muwfanyie wema na uadilifu, kwa sababu Mwenyezi Mungu anapenda uadilifu na wema kwa viumbe vyake vyote, wanomwamini na wanaomkufuru; kwa sharti moja tu, kutomfanyia ubaya yejote.

Kwa sababu watu wote ni wa Mungu, na anayependeza zaidi kwake ni yule awanufaishaye zaidi watu wake Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo mbele ya Mwenyezi Mungu, utengamano mzuri na mtu yejote ni kujizuia na kumfanyia uovu na kumwudhi. Ama mwenye kukanusha na akakufuru, basi ni juu yake kufuru yake.

Umetangulia ufanuzi kuhusu aina za urafiki na kafiri na hukumu zake katika kufasiri (3:30)

Kwa mnasaba huu tunaishiria kuwa kuchukia kwetu Mayahudi sisi Waislamu hakuna sababu nyengine ila kwamba wamepigana nasi nchini mwetu, waliwatoa wanawake wetu na watoto wetu; kama ambavyo sababu ya kwanza na ya mwisho ya kuchukia kwetu na uadui wetu kwa Amerika na Uingereza na mataifa mengineyo, katika mataifa ya kikoloni yanayosaidia Israil, ni kuwa mataifa haya yamesaidia kutolewa Wapalestina nchini kwao. Kwa mara nyingine tunarudia anavyotuambia Mwenyezi Mungu;

﴿إِنَّمَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُمْ مِّنْ دِيَارِكُمْ وَظَاهِرُوا عَلَىٰ
إِخْرَاجِكُمْ أَنَّ تَوَلَّهُمْ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ﴾

"Isipokuwa Mwenyezi Mungu anawakataza kuwafanya marafiki wanaopigana nanyi katika dini, na wakawafukuza katika nchi zenu na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu, na wawafanyao marafiki, basi hao ndio madhalimu" (60: 9)

PETROLI NA MAYAHUDI NAWAKRISTO

Wao kwa wao ni marafiki.

Wafasiri wamekongamana kuwa makusudio yake ni baadhi ya Mayahudi ni marafiki wa baadhi ya Wakristo, na wala sio Makusudio kwamba kila kundi ni rafiki wa kundi jingine. Kwa sababu, makundi hayo mawili yana uadui zaidi kuliko uadui uliopo baina ya Wakristo na Waislamu. Kwani Mayahudi wanamzulia Maryam na zina na Waislamu wanamtukuza na kumtakasa na kila aibu.

Hakuna mwenye shaka kwamba wafasiri wametoa maana haya kutokana na wakati walioshi, ambapo hakukuwa na mashirika ya kimataifa ya petroli wala taasisi za ulangazi na ulafi wa kunyonya mali za wananchi.

Ama leo baada ya kuweko mashirika hayo na taasisi hizo, wenye mashirika hayo, Wakristo wameona kuwa Mayahudi ndio njia bora ya kutegemea kuunga mkono ulangazi wao na tamaa yao.

Kwa ajili hii wakaweka taifa la Kiisrail ndani ya Palestina na wakalisaidia na kulihami, wakalipangia njia za kufanyia uchokozi na kujipanua, wakaliahidhi kusimama upande wake katika Umoja wa mataifa na

Baraza la usalama, wakalifunga kwenye milki yao na kuzunguka kwenye sayari yao.

Kwa hiyo Israil ikawa inatekeleza mipango ya kikoloni na kufuata amri za kiuadui, baada ya kugundua kuwa uhai wake uko kwenye rahani ya kusikiliza na kutii amri za wakoloni na kutekeleza mipango yake, vinginevyo litakimbiwa na kutawalishwa taifa jingine.

Ikiwa wakoloni wameweka tamaa yao kwenye makucha ya waisrail, basi tunamtegemea Mwenyezi Mungu na kijiandaa na vita ili kurudisha haki iliyoporwa.

Na mionganoni mwenu atakayewafanya urafiki nao basi huyo ni katika wao pamoja nao.

Yaani mwenye kuwafanya marafiki Mayahudi na Wakristo walio na uadui na Uislamu basi yeye yuko katika hukumu yao, atahisabiwa hisabu yao na kuadhibiwa adhabu yao, Kwa sababu, 'mwenye kuwaridhia watu, basi yeye ni katika wao.' Aya hii ni dalili mkato kuwa vibaraka wa wakoloni wanaolinda masilahi ya wakoloni, wana makosa zaidi na hatari zaidi kuliko wakoloni wenyewe, au angalau ni kama wakoloni wenyewe. Kwa sababu wao ndio nguzo ya unyoyaji wao na uadui wao.

Utawaona wale wenyewe maradhi nyoyoni mwao wanakimbilia kwao. Inaonyesha, kutokana na mfumo wa Aya, kuwa hilo ni tukio halisi lililotokea. Kwa ufupi ni kuwa baadhi ya wanafiki, wenyewe maradhi nyoyoni mwao, walikuwa wakifanya urafiki na Mayahudi amba walikuwa waki Tafsir ficha uadui kwa Uislamu na Waislamu na kuwaeleza mapenzi yao. Wakilaumiwa juu ya hilo husema: Unajuwaje pengine mambo yatageuka na Waislamu wawe wanyonge na nguvu iwe kwa Mayahudi na washirikina, kama hatukujipangia, tangu sasa na kuwaunga mkono, tutapata hasara na majanga.

Hii ndio maana dhahiri ya kauli yake Mungu Mwenyezi kwa Mtume: **Wakisema: Tunaogopa yasitusibu majanga.**

Na hivi ndivyo walivyo wazabizabina, wanajitia huku na kule, ili watakao shinda wawaambie sisi tulikuwa nanyi. Kwa maneno mengine ni kwamba wanafiki wako na wote kwa midomo, na kumbe hawana ila matamanio yao.

﴿يَخْلُقُونَ لَكُمْ مَا تَرْضَوْنَ عَنْهُمْ فَإِنْ تَرْضَوْنَ عَنْهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَرْضَى عَنِ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ﴾

"Wanaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba wao ni katika nyinyi wala wao si katika nyinyi, bali wao ni watu wanaoogopa" (9:56)

Yaani wanahofia nafsi zao na masilahi yao.

Unaweza kuuliza: kwanini amesema wanakimbilia kwao na wala asiseme wanawakimbilia.

Jibu: Kusema 'kwao' ni kusisitiza, Kwa sababu mwenye kuingia katika kitu anatalizana ndani yake zaidi. Huenda Mwenyezi Mungu akaleta ushindi au jambo jingine litokalo kwake, wakawa wenyewe kujuta kwa yale waliyoyaficha katika nafsi zao. Makusudio ya ushindi, ni Waislamu kuwashinda Mayahudi na Washirikina.

Na makusudio ya jambo jingine litokalo kwake ni kudhihirisha waliyo nayo wanafiki na kuwadhalilisha hao wanafiki na kuwafedhehesha. Maana ni kuwa wanafiki walijipangia kuwa maadui wa Uislamu, kwa kudhani kwamba Waislamu watafikwa na majanga kutoka kwa makafiri. Lakini

mambo yalipogeuka na janga likawapata maadui wa Uislamu, walijuta wanafiki, lakini hakutafaa kujuta kwao! Na watasema walioamini: Hivi hawa ndio wale walioapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwa viapo vyao vigumu, ya kwamba wao wako pamoja nanyi?

Mwenyezi Mungu alipoudhihirisha ushindi wa Waislamu kwa maadui zao, wanafiki hawakuweza kuficha uchungu wao, midomoni mwao na nyusoni mwao. Waumini wakastaajabu kutokana na hali ya wanafiki ilivyofichuka, wakaambiana.

Hivi hawa si ndio wale waliokuwa wakiapa kwa nguvu jana kuwa wao wako nasi? Ni mahodari sana wa uwongo na ria. Zimepomoka amali zao na wamekuwa wenyehasara.

Arrazi na mwenye Al-Manar anasema inawezekana jumla hii kuwa ni katika maneno ya Mwenyezi Mungu na inawezekana kuwa ni katika maneno ya waumini. Lakini ilivyo hasa haiwezekani kuwa ni maneno ya Mwenyezi Mungu kabisa. Kwa sababu, mfumo wa Aya unafahamisha kuwa ni katika maneno ya waumini na wala sio habari inayoanza upya kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t).

Maana yake nikuwa baada ya waumini kustajabia hali ya wanafiki na aibu yao walisema: Zimebatilika amali za wanafiki walizokuwa wakituonyesha, kama vile Saumu, Swala n.k. na wala hawakupata chochote katika thawabu. Wamekuwa wenyehasara duniani, kwa vile wamedhalilika, na wamepata hasara akhera kwa adhabu kali waliyoandaliliwa.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَنْ يَرْتَدَّ مِنْكُمْ عَنِ دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ جُبْنُهُمْ وَيُجْبِنُهُمْ أَذْلَلَةً عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعْزَّةٌ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَ لَا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لَائِمٍ ذَلِكَ فَضْلُ اللَّهِ بُوئْتِهِ مَنْ يَكْسَبُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلَيْهِمْ﴾

54. Enyi mlionamini! Atakayeritadi dini yake mionganini mwenu, basi Mwenyezi Mungu atawaleta watu anaoawapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa waumini, wenyehasara juu ya makafiri, wenyehasara jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaogopi lawama ya anayelaumu. Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu humpa amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa, mwenye kujua.

WANYENYEKEVU KWA WAUMINI WENYE NGUVU KWA MAKAFIRI

Aya 54

MAANA

Enyi mlionamini! Atakayeritadi dini yake mionganini mwenu, Kuritadi ni kuwa kafiri baada ya kuwa Mwislamu.

Tumemtaja Murtadi na mafungu yake katika kufasiri (2:217).

Kukataza kuritadi, baada ya kukataza kufanya urafiki na maadui wa dini, kunatambulisha kuwa kufanya urafiki huko kunasababisha kuritadi. Kuna Hadith isemayo: "Lau mchungaji atachunga kandokando ya ugo, hataweza kuwadhibiti mbuzi wake kuingia ndani" Watu wa sera na wanahistoria wanasesma, kuwa watu watatu waliritadi na kudai utume, wakati wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (**s.a.w.w**), baada ya kuwa Waislamu.

Wa kwanza ni As-wad Al-Ansi, alidai utume katika Yemen na akawatoa wajumbe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (**s.a.w.w**) huko, Aliuawa siku moja kabla ya kufa Mtume (**s.a.w.w**).

Wa pili ni Musaylamatul Kadhdhab. Alidai Utume na akamwandikia Muhammad (**s.a.w.w**) hivi: "**Kutoka kwa Musailama, Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwenda kwa Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu. Ama baada ya hayo, mimi ni mshirika wako katika jambo hili na ardhi baina yetu iko nusu kwa nusu**" Aliuawa wakati wa Abubakr. Watatu ni Twalha bin Khuwalid alidai utume, kisha akarudi kwenye Uislamu.

Ama Sajah ni mwanamke aliyedai utume wakati wa ukhalifa wa Abubakar na akaolewa na Musailama. Katika ndoa hii Abdalla alitunga shairi hili: "Saja na Musaylamu wamekwisha kupatana, waongo wa duniani tena ni waongo sana."

Unaweza kuuliza: kuwa baadhi ya masheikh hawana sharti za mujtahid (uongozi) alizozikusudia Imam Ali ^(a.s) aliposema: "**Mwenye kuichunga nafsi yake, mwenye kuihifadhi dini yake, mwenye kukhalifu hawaa yake, na mwenye kutii amri ya Mola wake**"

Lakini pamoja na hivyo wanadai kuwa ni manaibu wa Maasum, na kwamba kuwapinga ni kumpinga Mwenyezi Mungu. Je, hukumu yao ni sawa na ya Muislama, Kwa sababu wote wanamzuilia Mwenyezi Mungu?

Jibu: atakuwa kama Musailama kwa masharti mawili:

Kwanza: kudai unaibu wa Maasum naye anajua kuwa yeze ni mzushi mwongo na kwamba yeze hastahiki.

Pili: kutoona kuwa ijitahidi na uadilifu ni sharti za msingi za unaibu wa Ma'sum na huku anajua kuwa ni wajib kwa hukumu za kimsingi za dini. Kukadiria huku kuko mbali sana, kwa sababu mwenye kudai unaibu wa Maasum anajiona kuwa ni katika watu waadilifu na wenye kujitahidi hata kama hamtii Mola wake na kuhalifu hawaa yake.

Hakuna mwenye shaka kwamba huyu anatofautiana na Musailama kwa upande wa kuritadi, lakini anaungana naye katika upande wa uwongo na ghururi.

Kimsingi ni kuwa elimu na ghururi ni vitu viwili tofauti visivyokutana, sawa na uwongo na uadilifu. Kwa sababu ghururi inamtenga mtu wake na hali halisi ilivyo, na kumpeleka kwenye ulimwengu wa dhana na ndoto, Na atakayekuwa hivi, hawezo kuongoka kwenye usawa, Basi atawaleta Mwenyezi Mungu watu.

Wametofautiana wafasiri kuhusu waliokusudiwa katika neno 'watu' Arrazi amenukuu kauli sita, Mwenyezi Mungu hakuwataja majina yao, bali amewashiria kwa sifa zao.

Kwa hivyo, kila mwenye sifa tano, zilizotajwa katika Aya, basi ndiye aliyekusudiwa, Sifa zenyewe ni:-

1. Anaowapenda nao wanampenda.

Mwenyezi Mungu kumpenda mja wake, ni kumwinua kesho na kumneemesha kwa pepo na radhi. Ama pendo la mja kwa Mwenyezi Mungu, haliepukani na kuwapenda waja wa Mwenyezi Mungu, sawa na ambavyo kuipenda haki hakuepukani na kuwapenda wanaoitumia, na kuichukia batili kusivoepuka na kuwachukia watu wa batili.

2. Wanyenyeketu kwa waumini.

kwa sababu kumnyenyeka mumini ni kuitakasa na kuitakuza imani na ikhlasi na sio mtu mwenyewe. Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume wake: "**Na uinamishe bawa lako kwa yule anayekufuata katika walioamini**" (26:215).

Ilivyo ni kuwa wao hawakustahiki heshima hii ila kwa imani na ikhlasi yao kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

3. Wenye nguvu juu ya makafiri. Kwani kuwa na nguvu juu yao ni kuwa na nguvu kwa itikadi na misingi. Mfano wa Aya hii ni ile isemayo: "**Wenye nguvu kwa makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao.**" (48:29)

Aya hii na ile isemayo "Na uinamishe bawa lako", zinatuongoza kwenye hakika mbili:

Kwanza, kila mwenye kuwanyeyekea matajiri na wenye nguvu walio mataghuti na kujitakuza kwa mafukara waumini, basi hana chochote katika dini, hata kama akisimama usiku na akifunga mchana.

Hakika ya pili: msimamo wa maadili mema katika Uislamu sio unaotakiwa huo wenyewe isipokuwa Mwenyezi Mungu ameuamrisha kwa ajili ya watu na wala hakuwaamrisha watu kwa ajili yake. Kuanzia hapo, kunyenyeyekea wenye kiburi ni uduni na kuwanyeyekea wanyenyeketu ni utukufu. Imamu Ali anasema: "**Ni uzuri ulioje wa matajiri kuwanyeyekea mafukara kwa kutaka yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu, na uzuri zaidi kuliko huo ni mafukara kuwabeza matajiri kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu**"

4. Wenye kupigana jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Kila tendo la kutekeleza haja au kuondoa dhuluma, basi ni jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu. Kuna hadith isemayo: "**Mtume alikuwa amekaa na baadhi ya Sahaba zake wakamwangalia kijana wa miraba mine, wakasema angalia huyu! Lau ujana wake na nguvu zake angezitumia katika njia ya Mwenyezi Mungu.**" Mtume akasema: "**Ikiwa anaihangainia nafsi yake ili asiombe watu, basi hiyo ni njia ya Mwenyezi Mungu; ikiwa anawahangaikia wazazi wake wadhaifu au ndugu (zake) wadhaifu ili awatosheleze, basi hiyo ni njia ya Mwenyezi Mungu na ikiwa anahangaikia kwa kutaka kujifakharisha ili aonekane ni tajiri basi hiyo ni njia ya Shetani**"

5. Wala hawaogopi lawama ya anayelaumu. Hakika ya imani haidhihiri ila wakati wa misukosuko. Ndio ushindani sahihi wa imani ya mumini, anakanusha maovu kwa kumridhisha Mola wake na dhamira yake, Ama yatakayotokea hayajali. Hii ndiyo nembo ya wenye ikhlasi hawaogopi lawama ya mwenye kulaumu; au kama asemavyo Mtume wa rehema; "Ukitonikasirikia sitajali." Chimbuko la matatizo ya ulimwengu leo, kuanzia vita vya Vietnam mpaka vya Mashariki ya kati, na kuanzia serikali ya kibaguzi ya Rhodesia¹ na Afrika kusini hadi tatizo la wamarekani weusi katika Amerika, chimbuko lake ni kunyamazia haki tu, katika magazeti na idhaa, na katika Umoja wa mataifa na Baraza la usalama, kwa kuhofia wafalme wa dhahabu nyeusi (petroli) na wahami wao waliochodishwa.

1 Sasa ni Zimbabwe. Mwandishi aliandika tafsiri hii wakati nchi hiyo ikikaliwa kimabavu na makaburu

Kwa hiyo basi, kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu inatoa picha hai ya mwenye dini na malengo anayopasa kuyaenda na kujitolea mhanga kwayo.. Limebaki swalii hili jepesi: Je, baada ya haya mtu anaweza kusema kuwa dini ni mambo ya ghaibu na kuswalia maiti tu?" Hiyo ni fadhila ya Mwenyezi Mungu humpa amtakaye.

Tumeona kwa hisia kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) hataki kumpa fadhila zake ila mwenye kwenda kulingana na sababu na desturi ambayo ameiwekeea nidhamu ya ulimwengu Yeye ambaye kwake hekima imetukuka. Lau angelitaka tutembee bila ya miguu, tufanye kazi bila ya mikono na tuone bila macho asingelikuwa na haja ya kuumba chochote katika hivyo. "Na ameumba kila kitu akakikadiria kwa kipimo (chake)" (25:2)

TATIZO LA MAADILI

Anasema Nietzsche, mwenye falsafa ya upeo wa juu zaidi wa Binadamu: "Hakuna kitu kinachoitwa, thamani ya maadili. Kwa hiyo uhuru, uadilifu na usawa ni maneno tu waliyoyatengeneza wanyonge ili kuzuia kutawaliwa na wenyewe nguvu. Marks naye anasema kinyume na hayo:

Maana yake, kwa wote wawili, ni kuwa neno thamani halina mshiko isipokuwa ni hawaa na masilahi tu ya dhati; na maadam hawaa haifikiani na utu na upeo wake basi matamko hayo yatakuwa ni uwongo na unafiki. Sisi tunaamini kwamba chimbuko la thamani ni masilahi, lakini ni masilahi yanayotokana na asili ya binadamu kama binadamu, si kutockana na tabaka aliyo na kundi aliloko. Hapana mwenye shaka kwamba masilahi haya yanaafikiana na binadamu na upeo wake, Ndipo yakaitwa thamani ya binadmau sio ya tabaka.

Kwa hiyo basi yanakuweko kwa kuweko binadmau mwenyewe, wala hayaondolewi na mnyonyaji au atakayeyageuza kulingana na matakwa yake. Vinginevyo, basi isingefaa kuwagawanya watu, mwenye haki na mbatilifu anayebadilisha maneno na mwenye ikhlasi na mnafiki anajifunika ngozi ya watu wema. Zaidi ya haya hakuna katika historia ya binadamu au jamii yoyote iliyowahi kusema: Fanya utakavyo kwa sababu wewe huna jukumu lolote, ukiua au ukiiba, Ndio kuna madheehbu mbalimbali ya kupanga thamani ya maadili, ambayo hatuna nafasi ya kuayataja. La muhimu ni kuyaeleza, kama ilivyo katika mtazamo wa kiislamu. Kalamu za wenyewe ghera zimeandika mpango wa kiislamu kuwa una lengo la kuweka mtu mwema katika jamii njema.

Lakini mpango huu unahitaji mpango, Kwa sababu, msomaji hafahamu kitu wazi atakachokuwa nacho wakati wa kufuutilia na kutekeleza, Kwa kuepuka matatizo hayo, kwanza tutaanza kutaja baadhi ya mifano, kisha tutoe, katika dalili zake, mpango ulio wazi unaowezekana kutekekelezwa kila siku, Uislamu umeamrisha ukweli, utekelezaji ahadi, kujitolea, kunyenyeka, uvumilivu, kusamehe n.k.

Lakini uwajibikaji wake katika hayo umewekewa mpaka ambao haifai kuukiuka kwa hali yoyote ile. Mpaka wenyeve ni kuwa uwajibikaji huo usisababishe kwenda kinyume na lengo liliookusudiwa.

Ukweli ni wajibu maadamu uko kwenye masilahi ya binadamu, lakini kama ukileta dharau, kama vile kumpa adui siri za kiulinzi au kunakili maneno kwa kukusudia fitina, basi hapo ukweli utakuwa ni haramu. Uwongo ni haramu isipokuwa kuutumia katika vita na adui wa dini na wa

nchi, katika kusuluhisha wawili na kuhifadhi mtu asiyekuwa na hatia na mali.

Kutekeleza kiapo ni wajibu maadamu muapaji hapati manufaa yoyote kutokana na kiapo chake, vinginevyo ataacha, kutokana na hadith isemayo" Ukipata heri kutokana na kiapo chako basi kiache" Kutoa mali sabili ni kuzuri, lakini ikiwa mwenyewe ataihitajia basi haifai.

Uvumilivu unatiliwa nguvu, lakini haufai kwenye dhulumu na tabia mbaya. Na kusamehe ni fadhila, lakini hakufai ikiwa ni sababu ya kuleta vurugu na kuendeleza utendaji makosa.

Kwa hivyo basi, imetubainikia kuwa thamani ya maadili katika Uislamu hupimwa na masilahi yatakayopatikana au kukinga madhara. Maana yake ni kuwa thamani hiyo iko kwa ajili ya binadamu, na wala sio kuwa binadamu yuko kwa ajili ya hiyo thamani, ili aiabudu. Thamani ya kimaadili ni ile inayodhibiti matumizi ya mtu katika kuleta masilahi yake na masilahi ya jamii au kutodhurika nayo au kumdhuru mtu mwengine. Unaweza kuuliza: Ni kipi kitakachodhibiti kupambanua manufaa na madhara. Tunajibu kwa ufupi: Mdhibiti ni hisia za ujumla kwamba hili linadhuru na hili ni la manufaa. Hisia zikiona tu basi 'kwisha maneno' hakuna swali wala jawabu, kwa sababu hisia za ujumla ndio msingi wa dhati.

TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

﴿إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا إِنَّمَا يُقْبِلُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْثِرُونَ الرَّكَأَةَ وَهُمْ رَاجِعُونَ﴾

55. Hakika walii wenu hasa ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini ambao husimamisha Swala na hutoa Zaka wakiwa wamerukui.

﴿وَمَنْ يَتَوَلَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا فَإِنَّ حِزْبَ اللَّهِ هُمُ الْغَالِبُونَ﴾

56. Na atakayemtawalisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini, basi kundi la Mwenyezi Mungu ndio watakaoshinda.

HUTOA ZAKAWAKIWA WAMERUKUI

Aya 55-56

MAANA

Hakuna hata mmoja anayebishana kuwa makusudio ya neno walii kwa Mwenyezi Mungu na Mtume ni kuwa msimamizi na kutawalia mambo ya Waislamu na wala sio mapenzi na usaidizi tu. Mwenyezi Mungu anasema: "Nabii ana haki zaidi kwa waumin kuliko nafsi zao" (33: 6)

Aya hii ni ubainifu na tafsiri ya neno (walii) katika Aya tulio nayo. Na wale walioamini ambao husimamisha Swala na hutuoa Zaka wakiwa wamerukui: Yaani wilaya ambayo imethibiti kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, imethibiti vile vile kwa aliyetoa zaka huku amerukui.

Amenukuu Tabari kutoka kwa Mujahid Utaba bin Hakim na Abu Jafar kwamba Aya hii ilishuka kwa sababu ya Ali bin Abu Talib.

Katika Kitabu Gharaibul-Qur'an wa raghaibul-furq'an cha Nidhamuddin, Ali-Hassan bin Muhammad Annaisaburi, katika Maulama wa sunni, imeandikwa hivi (ninamnukuu): "Aya imeshuka kwa Ali, kwa maafikiano ya wafasiri wengi" Vile vile katika tafsiri Arrazi imeandikwa (ninamkuu): "Imepokewa kutoka kwa Abu Dharr, (r.a) kwamba yeye amesema: "Niliswali na Mtume wa Mwenyezi Mungu (**s.a.w.w**) siku moja, akaja mtu kuomba, lakini hakuna yejote aliyempa kitu. Ali alikuwa amerukui, akamwashiria kidole chake cha pete cha upande wa kuume.

Yule mwombaji akachukua pete huku Mtume (**s.a.w.w**) akiwa anamuangalia. Akasema Mtume: 'Ewe Mola wangu ndugu yangu Musa alikuomba kwa kusema:' Ewe Mola Wang! Nikunjilie kifua changu na unifanyie waziri katika jamaa zangu, ndugu yangu Harun, nitie nguvu kwaye' 'Basi Ewe Mola wangu! Na mimi ni Muhammad Mtume wako na mteule wako, basi nikunjue kifua changu na unisahilishe jambo langu, unifanyie waziri katika jamaa zangu na unitie nguvu kwaye", Abu Dharr anasema: Hakumaliza maneno haya na Jibril akashuka, na akasema "Ewe Muhammad! Soma: Hakika walii wenu ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake Mpaka mwisho wa Aya."

Lakini Razi amefasiri neno (walii) hapa kwa maana ya msaidizi, sio mtawala. Shia nao wakasema: Tamko la Mwenyezi Mungu na Mtume na mwenye kutoa zaka akiwa amerukui limekuja katika Aya moja na wilaya ya Mwenyezi Mungu na Mtume, maana yake ni utawala. Kwa hiyo ni lazima

vile vile maana ya wilaya ya mwenye kukusanya sifa mbili hizi ni utawala vile vile. Vinginevyo, basi neno wilaya litatumika kwa maana mbili tofauti wakati mmoja, jambo ambalo haliwezekani. Na mwenye kumtawalisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake na waumini, basi kundi la Mwenyezi Mungu ndio watakaoshinda.

Aya hii ni kauli wazi isiyokubali taawil kwa hali yoyote kwamba maana ya makusudio ya kumtawalisha Mwenyezi Mungu na Mtume na waumini ni moja isiyokuwa na tofauti na kwamba mwenye kuichunga wilaya hii na wala asitofautishe baina ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na mwenye kutoa zaka akiwa amerukui, basi yeze yuko katika kundi la Mwenyezi Mungu litakaloshinda; kutokana na mantiki ya haki na hoja yake.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَنْخُذُوا الَّذِينَ اتَّخَذُوا دِينَكُمْ هُرُوا وَلَعِبًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَالْكُفَّارُ أُولَئِكَ وَأَنَّهُمْ مُّؤْمِنُونَ﴾

57. Enyi mlionamini! Msiwafanye marafiki wale walioifanyia mzaha na mchezo dini yenu katika wale walioopewa Kitab kabla yenu na makafiri. Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni waumini.

﴿وَإِذَا نَادَيْتُمْ إِلَى الصَّلَاةِ اتَّخَذُوهُ اهْرُوا وَلَعِبًا قَوْمٌ لَا يَعْقِلُونَ﴾

58. Na mnaponadi Swala, wanaifanyia mzaha na mchezo. Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasiokuwa na akili.

﴿فُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ هَلْ تَقْمُونَ مَنَا إِلَّا أَنَّ آمَنَّ بِاللَّهِ وَمَا أُنْزِلَ إِلَيْنَا وَمَا أُنْزِلَ مِنَّا بَلْ وَأَنَّ أَكْثَرَكُمْ فَاسِقُونَ﴾

59. Sema: Enyi watu wa Kitab! Hivyo mnatuchukia kwa kuwa tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale yaliyoteremshwa zamani na ya kwamba wengi wenu ni mafasiki.

DINI YENU WAMEIFANYIA MZAHNA MCHEZO

Aya 57 - 59

MAANA

Enyi mlionamini! Msiwafanye marafiki wale walioifanyia mzaha na mchezo dini yenu katika wale walioopewa Kitab kabla yenu na makafiri.

Kwa mara ya pili Mwenyezi Mungu (s.w.t) anakataza kuwafanya maadui wa Mwenyezi Mungu kuwa marafiki, lakini hapa amebainisha sababu ya kukataza. Sababu yenyewe ni kuwa wao wameifanya dini ya kiiislamu na Swala ya waislam ni vitu vyta kuchezewa.

Ndivyo alivyo safihi anayeshindwa kujibu hoja, Wala haielekei kwa mwenye akili kumfanya walii safihi hasa yule anayechezea dini na utakatifu wake. Vilevile Mwenyezi Mungu (s.w.t) amezidisha, katika Aya hii, kuunganisha makafiri na watu wa Kitab, katika hali ya kuungisha mahsus kwenye ujumla. Qur'an huunganisha mahsus kwenye ujumla, kama Aya hii; na ujumla kwenye mahsus kama Aya isemayo:

"Angalieni sana Swala na ile Swala ya katikati" (2:238)

Na pia huunganisha kitu kwenye mfano wake; kama pale aliposema. "Basi hao atawaingiza katika rehema itokayo kwake na fadhila" (4:175)

Na mcheni Mwenyezi Mungu kama nyinyi ni waumini.

Ndani yake mna utambulisho kuwa mwenye kumfanya mwenye kuchezza dini kuwa ndiye mwenzake na walii wake, basi huyo yuko mbali na watu. Kwa sababu mwenye kushahibiana na kitu kuvutiwa nacho.

Na mnaponadi Swala, wanaifanyia mzaha na mchezo.

Makanisa ya wakristo yanawaita wafuasi wake kwenda kuswali kwa kupiga kengele, na masinagogi ya Mayahudi huwaita wafuasi wake kwa kupiga tarumbeta. Ama Waislamu, huwaita wafuasi wake kwenye Swala kwa sauti ya mwadhini anayelingania kwa Mwenyezi Mungu peke yake asiye na mshirika, na kwenye amali njema ya kufaulu: Mwenyezi Mungu ni mkubwa Hapana mola isipokuwa Mwenyezi Mungu Njooni kwenye kufaulu Njooni kwenye amali njema Baadhi ya watu wa Kitab walikuwa na bado wanaendelea kuidharau adhan hii na mwito huu. Ingefaa basi wazidharau kengele zao na tarumbeta zao.

Wakati huo huo Wakristo wasiokuwa na kasumba wanaifadhilisha adhan kuliko kengele. Mwenye Al-manar anasema: "Tuliwasikia baadhi ya wakristo wasiokuwa na kasumba nchini mwetu, yaani Lebanon, wakisifu maneno ya adhan na kuifadhilisha kuliko kengele. Katika mtaa wa Kalamon mjini Tripoli, baadhi ya jamaa wa kikiristo walikuwa wakisimama. Wanawake na wanaume wakawa wanasmama madirishani kusikiliza sauti ya mwadhini, ambaye alikuwa na sauti nyororo.

Ilikuwa mtoto wao anaweza kuhifadhi adhan na kumwigiza vizuri mwadhini, hapo mama hukasirika na kumkataza, lakini baba hucheka na kufurahia adhana ya mtoto wake, kwa sababu alikuwa yuko huru na wasaa." Hayo ni kwa sababu wao ni watu wasio na akili.

Wamesema wafasiri, akiwemo Razi na mwenye Al-Manar, kuwa makusudio ya Wasio na akili ni kwamba wao hawajui hakika ya Uislam. Lau wangeijua hakika yake wasingeufanyia mchezo, Ama sisi tunasema kuwa wanaujua Uislamu, na wanaujua lengo lake. na kwamba wale walioupiga vita, walifanya hivyo kwa sababu waliona hatari yake kwa manufaa yao. Walijua kuwa Uislam ni mapinduzi ya kujikombua na dhulma, unyonyaji, ufukara, ujinga na ubaguzi, na kwamba hakuna ubora wa kiumbe yejote kumzidi kiumbe mwengine ila kwa kuwashudumia watu na kufanya kazi kwa ajili ya masilahi ya wote, Hili ndilo kosa la Uislam kwao. Ndio maana wakaupiga vita kwa silaha zote walizonazo, hata kebehi na dharau.

Mwito wa kiislamu unadhihiri kwa maana yake kamili katika wito wa mwadhini. Mwenyezi Mungu ni mkubwa, hapana Mola isipokuwa Mwenyezi Mungu. Kwani maana ya Mwenyezi Mungu ni Mkubwa ni kwamba hakuna mkubwa wala adhimu ila yeye peke yake hana mshirika. Na maana ya Hapana mola isipokuwa Mwenyezi Mungu, ni kwamba mali na cheo na nasabu sio mungu wa kuabudiwa wala nguvu ya kunyenyekekewa, ni haki peke yake, na watu wote katika haki ni sawa, hakuna yejote mwenye ruhusa ya kuugusa uhuru wa mwengine vyovoyote atakavyokuwa. Hili linatosha kuwa ni kosa kwa maadui wa binadamu. Na kwa ajili ya uadui wao huu, si kwa ajili ya kutojua uhakika wa Uislamu, ndipo Mjuzi mwenye hekima akawasifu kwamba wao ni watu wasiokuwa na akili.

Sema: Enyi watu wa Kitab! Hivyo mnatuchukia kwa kuwa tumemwamini Mwenyezi Mungu na yale yaliyoteremshwa zamani, na ya kwamba wengi wenu ni mafasiki?

Ndio! Wao hawamridhii ila yule wanayemwamini wao na unyonyaji wao. Huyo ndiye mtakatifu wa watakatifu, katika vipimo vyao, hata ikiwa anamkufuru Mwenyezi Mungu na Mitume wote. Ama mwenye kukana dhulma yao na utagħuti wao, basi huyo kwao ni mshari wa mwanzo na wa mwisho, hata kama ni walii wa mawalii.

Dalili kubwa ya hilo ni kuwa wao wanawatuhumu wazalendo na kuwazulia kuwa wametoka katika dini, si kwa lolote ila ni kwa kuwa wanapinga siasa za kikoloni na za ubaguzi. Pamoja na tuhuma zao hizi, wao wanadai kuwa ni wahami na walinzi wa dini na walahidi.

Unaweza kuuliza: Kauli yako hii ndivyo mambo yalivyo, tunavyoyaona na tunavyoyashuhudia, lakini hayafai kuwa ni tafsiri ya Aya hii. Kwa sababu wao wanahasimiana na Waislam kwa sababu ni Waislamu wanaomwamini Mwenyezi Mungu Qur'an, Tawrat na Injil?

Jibu: Dhahiri ya Aya inafahamisha waziwazi kuwa, Mwenyezi Mungu (s.w.t) alimwamrisha Mtume wake Mtukufu kuwaambia Je sisi tunakosa linalotusababisha kuwa na uadui na nyinyi kwa vile tu ni kuwa sisi tuko kwenye haki na nyinyi mko kwenye batili; sawa na mzalendo halisi anavyomwambia kibaraka mhaini: 'Je, unanichukia kwa vile mimi ni mzalendo na wewe ni kibaraka'

Hakuna shaka kwamba maana haya yanafikiana na tafsir yetu ya Aya, bali hiyo ndiyo iko dhahiri zaidi. Ameyaelezea hayo mwenye Majmaul-bayan alipoeleza kwenye Tafsir yake: "Maana ya Aya hii ni: Je, mnatuchukia kwa imani yetu na ufasiki wenu;" yaani mmeichukia imani yetu na nyinyi mnajua tuko kwenye haki na kwamba nyinyi mko kwenye dini yenu kwa kupenda kwenu ukubwa na kuchuma mali? Kisha akaendelea kusema: "Na maana ya ufasiki ni kuwa wao wametoka katika amri ya Mwenyezi Mungu kwa kutaka ukubwa."

﴿قُلْ هُنَّ الَّذِينَ يُشَرِّكُونَ مِنْ ذُلِّكَ مَثُوبَةً عِنَّدَ اللَّهِ وَمَنْ لَعَنَهُ اللَّهُ وَغَضِبَ عَلَيْهِ وَجَعَلَ مِنْهُمْ الْقِرَدَةَ وَالْحَنَّازِيرَ وَعَبَدَ الطَّاغُوتَ أُولَئِكَ شَرٌّ مَّكَانًا وَأَضَلُّ عَنْ سَوَاءِ السَّبِيلِ﴾

60. Sema: Je, niwaambie yule mwenye malipo mabaya kuliko haya mbele ya Mwenyezi Mungu? Ni ambaye Mwenyezi Mungu amemlaani na kumkasirikia na akawafanya mionganu mwao manyani na nguruwe na akamwabudu Tagħuti. Hao ndio wenze mahali pabaya na wapotofu sana na njia iliyo sawa.

﴿وَإِذَا جَاءُوكُمْ قَاتُلُوا آمَنًا وَقَدْ دَخَلُوا بِالْكُفَّارِ فَرَّ وَهُمْ قَدْ حَرَجُوا بِهِ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا كَانُوا يَكْتُمُونَ﴾

61. Na wanapowajia husema: Tumeamini hali wao wameingia na ukafiri wao na wametoka nao. Na Mwenyezi Mungu anayajua sana wanayoyaficha.

﴿وَتَرَى كَثِيرًا مِّنْهُمْ يُسَارِعُونَ فِي الْإِثْمِ وَالْعُذُولَةِ وَأَكْثُرُهُمُ السُّكْنَى لَتَرَى مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾

62. Na utawaona wengi katika wao wanakimbilia kwenye dhambi na uadui na kula kwao haramu. Hakika ni mabaya waliyokuwa wakiyatenda.

﴿لَوْلَا يَنْهَاهُمُ الرَّبَّانِيُّونَ وَالْأَحْبَارُ عَنْ قَوْلِهِمُ الْإِثْمَ وَأَكْثُرُهُمُ السُّكْنَى لَتَرَى مَا كَانُوا يَصْنَعُونَ﴾

63. Mbona watawa wao na maulama wao hawawakatazi maneno yao ya dhambi na uadui na ulaji wao wa haramu? Hakika ni mabaya waliyokuwa wakiyafany.

AKAWAFANYA WENGINE MANYANI NA NGURUWE

Aya 60 - 63

MAANA

Sema: Je, niwaambie yule mwenye malipo mabaya zaidi kuliko hayo mbele ya Mwenyezi Mungu?

Yaani sema Ewe Muhammad kuwaambia maadui wa haki na wa dini ambao wanaucheza shere Uislamu na adhan kuwa, ikiwa kumwamini Mwenyezi Mungu na vitabu vyake ni shari inayowajibisha chuki, basi mimi ninawapa habari ya shari kuliko hii, nayo ni ambao Mwenyezi Mungu amewaalani na kuwakasirikia na kuwafanya manyani na nguruwe na wakamwabudu Taghut. Sifa zote hizi ni za mayahudi, ambazo Mwenyezi Mungu amewaorodheshea katika ziada ya Aya hii na akawasifu kwa kuabudu Taghut.

Aya zilizo mfano wa Aya hii ni kama zifuatavyo:-

- 1."...kama tulivyowalaani watu wa Sabato (Jumamosi). (4:47)
 - 2."Kwa hiyo wakastahili ghadhabu juu ya ghadhabu" (2:90)
 - 3."Basi tukawaambia kuweni manyani wadhalilifu." (2:65)
- Na analosema Mwenyezi Mungu kuwa, huwa
4. "Wanaamini sanamu na taghut" (4:51).

Imesemekana, makusudio ya taghuti ni shetani na ikasemekana ni ndama, na sahihi ni kuwa kila anayemtii mja katika kumwasi Mwenyezi Mungu, basi huyo amemwabudu yeye.

Arrazi amesema: " wametoa hoja masihabu zetu- yaani Ash-ari- kwa Aya hii, kwamba ukafikiri ni maajaliwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu makadirio hapa ni, Na akawajalia Mwenyezi Mungu kuabudu Taghut." Lakini usahihi ni kuwa hayo yanaungana na laana ya Mwenyezi Mungu, yaani: Je, niwaambie yule mwenye malipo mabaya kuliko haya ni ambaye Mwenyezi Mungu amewaalani na akamwabudu Taghut; kwa hivyo haifai kutoa dalili na Aya hii kwamba ukafiri unatokana na Mwenyezi Mungu na sio mja.

Hao ndio wenyenye mahali pabaya na wapotofu sana na njia iliyo sawa.

Hao ni ishara ya Mayahudi, kwa dhahiri. Na ilivyo hasa inawachanganya wote wanaopiginga haki.Wala haitoshelezi kauli ya kusema: Hapana mola ila Allah na Muhammad ni mtume wa Mwenyezi Mungu.Kwani hakuna imani bila ya Takua.

Na wanapowajia husema: Tumeamini hali wao wameingia na ukafiri wao na wametoka nao.

Wanafiki wa kiyahudi walikuwa wakiingia kwa Mtume na kumwambia: sisi tumekuamini; na hali wao ni waongo.Mwenyezi Mungu anauelezea unafiki wao huu kwamba wao wameingia kwa Mtume na ukafiri na wakatoka kwake na ukafiri. Ibara hii inafahamisha kuwa lau kama wao walikuwa wanaitafuta haki kweli wangelitoka mbele za Mtume wakiwa waumini baada ya kusikia na kuona dalili na ubainifu.

Na Mwenyezi Mungu anayajua sana wanayoyaficha katika ukafiri na unafiki na kuwalipa wanayostahiki.

Na utawaona wengi wao wanakimbilia katika dhambi na uadui na kula kwao haramu. Hakika ni mabaya waliyokuwa wakiyatenda.

Kukimbilia ni kuashiria kushindana katika dhambi na kula haramu.

Sifa hii hawaepukani nayo Mayahudi, na ndio maana watu wa zamani na wa sasa wamewachukia isipokuwa yule atakayewatumia kufanyia shari, sawa na sumu kwa muuaji. Hata huko Marekani, ambako ni kiota cha Uyahudi, pia wako wengi wanaowachukia Mayahudi.

Mbona watawa wao na maulama wao hawawakatazi maneno yao ya dhambi na uadui na ulaji wao wa haramu? Hakika ni mabaya waliyokuwa wakiyafanya.

Kutahayarizwa huku, kunakofahamishwa na neno, mbona na ubaya, kwa dhahiri kunaelekezwa kwa viongozi wa dini katika watu wa Kitab, na kwa hali halisi, kunaelezwa kwa kila aliyejua haki na akainyamazia. Kwa hakika mwenye kumjua Mwenyezi Mungu kikweli na kumfanyia Ikhlasi yeye tu peke yake, hupinga udhalimu kwa nyenzo zote.

Akiwa na yakini kuwa kifo chake katika njia hii kitawazindua waliolala na kuwapinga madhalimu anakuwa tayari na kuueleza upinzani wake kwa kufa shahidi. Historia ya mashahidi wote ni historia ya kupinga makosa ya dhulma na uadui.

﴿وَقَالَتِ الْيُهُودُ يَدُ اللَّهِ مَغْلُولَةٌ عُلِّتَ أَيْدِيهِمْ وَأَعْنُوا بِمَا قَالُوا بَلْ يَدَاهُ مَبْسُوطَاتٍ يُنِيبُ فَ قُرْبَانٌ كَيْفَ يَشَاءُ وَلَيَزِيدَنَّ كَثِيرًا مِنْهُمْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رِبِّكَ طُغْيَانًا وَكُفْرًا وَالْقِيَامَةُ بَيْنَهُمُ الْعَدَاؤُ وَالْبَعْضَاءُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ كُلُّمَا أَوْقَدُوا نَارًا لِلْحَرْبِ أَظْفَاهَا اللَّهُ وَيَسِّعُونَ فِي الْأَرْضِ فَسَادًا وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الْمُفْسِدِينَ﴾

64. Walisema Mayahudi: Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba. Mikono yao ndiyo iliofumba, na wamelaaniwa kwa waliyoyasema, Bali mikono yake iko wazi hutoa apendavyo. Kwa hakika yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako yatawazidisha wengi katika wao uasi na kufru. Na tumewatilia uadui baina yao na chuki mpaka siku ya Kiyama. Kila mara wanapowasha moto wa vita Mwenyezi Mungu anauzima, Na wanajitahidi kuleta ufisadi katika ardhi, Na Mwenyezi Mungu hawapendi wafisadi.

﴿وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْكِتَابِ آتَمُوا وَاتَّقَوْا لَكَفَرْنَا عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَلَا دُخُلْنَاهُمْ جَنَّاتُ النَّعِيمِ﴾

65. Na lau kwamba watu wa Kitab wangeliyamin na wakamcha Mungu, tungeliwafutia makosa yao na kuwaingiza katika bustani (pepo) zenye neema.

﴿وَلَوْ أَنَّهُمْ أَقَامُوا الْوَرَأَةَ وَالْإِنْجِيلَ وَمَا أُنْزِلَ إِلَيْهِمْ مِنْ رَبِّهِمْ لَا كُلُّوا مِنْ فَوْرِ قِيهِمْ وَمَنْ تَحْتِ أَرْجُلِهِمْ مِنْهُمْ أُمَّةٌ مُّقْتَصِدَةٌ وَكَثِيرٌ مِنْهُمْ سَاءَ مَا يَعْمَلُونَ﴾

66. Na lau wangelisimamisha Tawrat na Injil na yale yaliyoteremshwa kwao kutoka kwa Mola wao kwa hakika wangelikula vy a juu yao na vy chini ya miguu yao. Miogoni mwao wato walio sawa na wengi wao wanayoyafanya ni mabaya.

MAYAHUDI WALISEMAMKONO WAMWENYEZI MUNGU UME FUMBA

LUGHА

Neno 'mkono' lina maana nyingi ikiwemo hizi zifuatazo:-

- i. Kiungo, yaani huu mkono wa kawaida ninaoandikia maneno haya.
- ii. Neema, kama kusema fulani ameniunga mkono, ninamshukuru.
- iii. Uwezo.

iv. Milki, hutumiwa kutoa na kuzuia kulingana na hali ilivyo.

Unaweza kusema: Amenyoosha mkono wake; kama ukikusudia kutoa.

Na kusema: Ameufumba mkono wake; kama ukikusudia kuzuia.

MAANA

Walisema Mayahudi: Mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba.

Hii ni picha mionganoni mwa picha kadhaa zinatolewa na Qur'an kwa Mayahudi, kama vile kusema kwao: "Hakika Mwenyezi Mungu ni fukara na sisi matajiri."

Kulingana na makisio yao ni kuwa wao wawe waungu. Mwenyezi Mungu umetukuka ukuu wake. Utovu wao huu wa haya na ufidhuli, ulidhihiri ubaya wa maana yake katika kukiuka kwao makubaliano ya kimataifa kwa kuivamia Quds mnamo mwaka 1967.

Baadhi ya mapokezi yanasema kuwa aliyetamka neno hili la kufuru, ni Mayahudi mmoja anayeitwa Finhas. Inawezekana kuwa riwaya hii ni sahihi, na ni kweli kuwa kauli ya mtu mmoja haiwakilishi kundi la watu wote; na pia ni kweli kwamba baadhi ya Waislamu dhaifu husema hivi wanapozongwa na masaibu wakiwa hawana la kufanya.

Yote haya yanaweza kuwa kweli, lakini mwenye kuichunguza sera ya Mayahudi atajua kuwa wao wanalisema neno hili kwa lugha ya vitendo ingawaje hawatamki kwa mdomo. Wao wanataka Mwenyezi Mungu awape dunia yote na vilivyomo, vinginevyo basi Mwenyezi Mungu ni bakhili aliyefumba mkono.

Mikono yao ndiyo ilifumba na wamelaaniwa kwa yale waliyoyasema

Na waliyoyafanya ya kushindana katika dhambi, uadui na vile vile kula kwao mali ya haramu.

NJAMA ZA MAYAHUDI NA WANAZI¹

Mwenye Tafsir Al-Manar anasema: "Mikono yao ndiyo iliyofumba, ni maapizo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa ubakhili wao. Na bado wao ndio mabakhili zaidi, Yeyote katika wao hawezি kutoa kitu mpaka awe na faida sana."

Ilikuwa faida yao pekee ni mali. Na kwa ajili ya mali wanahalalisha kila la haramu. Ama leo, hawana faida bora kuliko kumwua Mwarabu hata kama ni mtoto. Nembo takatifu ya kidini ya jumuia zao za kujitolea ni 'Toa Dola moja itamwua Mwarabu,' awe Mwislamu au Mkiristo. Bali wao, wake kwa waume na hata watoto wanatoa roho zao ili wawatoe wapalestina nchini mwao na wachukue mahali pao. La kushangaza katika niliyoyasoma ni kwamba viongozi wa Kizayuni akiwemo. Wiseman, Moses Sarit, David ben

1 Nazi ni chama kilichoanzishwa na Hitler

Gorin na viongozi wa Custavo, walikula njama pamoja na wanazi kuwachinja Mayahudi na kuwatesa kwa malengo mawili:

Kwanza: Wayahudi wawe na sababu ya kuhamia Palestina,

Pili: kupatikane sababu ya kuunda serikali ya Kiisraeli. Hayo yamo katika kitabu kilichofasiriwa kwa kiarabu na Asal kwa jina la Itlaql-hamama 5 Julai, kilichotungwa na Belyalev, Costanchenko na Primakov.

Ikiwa Mayahudi wanaweza kupanga njama pamoja na maadui zao wakubwa na kuwatoa mhanga maelfu katika wao ili tu isimame dola ya Israil, je watashindwa kusema kuwa Mwenyezi Mungu ni fukara na wao ni matajiri na kwamba mkono wake umefumba hautoi. Kuna ajabu kusema: Sisi tunaihami amani na waarabu wanachochea vita na uharibifu, baada ya kuwa washasema Mwenyezi Mungu ni fukara na sisi ni matajiri?

Ikiwa mkono wa Mwenyezi Mungu umefumba kwa vile hakuwapa dunia na vilivyomo, basi waarabu kwao watakua ni mataghuti na wachokozi kwa vile hawakuwachia Mayahudi. Mimi sisemi maneno haya kama ngonjera au kwa sababu ya hamaki. Kwani si ni hao mayahudi waliowang'ang'ania waarabu waitambue Israil?

Je,kuna maana nyingine ya kutaka kutambuliwa huku zaidi ya kutaka waachiwe wao tu?

Bali mikono yake iko wazi.

Makusudio ya mikono ni yale makusudio ya mkono wake wa kuume katika Aya isemayo:

"Na mbingu zitakunja kwa mkono wake wa kuume" (39:67)

Yaani kwa uwezo wake. Amesema Mikono na wala sio mkono kwa sababu ndiyo picha ilio fasaha zaidi na inayokusanya zaidi maana.

Hutoa apendavyo.

Kwa kuleta sababu yenye kuwajibisha hilo:

﴿هُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ ذَلِيلًا فَامْشُوا فِي مَنَاكِبِهَا وَكُلُّوا مِنْ رِزْقِهِ وَإِلَيْهِ التُّشْرُقُ﴾

"Yeye ndiye aliyeidhalisha ardhi kwa ajili yenu, Basi nendeni katika pande zake zote na kuleni katika riziki yake Na kwake yeye ndio kufufuliwa" (67:15)

Kwa hakika yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako yatawazidisha wengi katika wao uasi na kufuru.

Makusudio ya wengi ni viongozi na wapenda anasa ambao hawatoi mwito wa haki kwa kuhofia vyeo vyao. Na mwito huu umewazidishia chuki kwa Muhammad (**s.a.w.w**), kwa sababu umefichua aibu zao na maovu yao, yakiwemo kubadilisha maneno ya Mwenyezi Mungu na mahali mwake, kula kwao mali ya haramu na kuacha kukataza maovu.

Ni kawaida ya mwenye kujigamba kuzidisha ujeuri akifichuliwa aibu yake na madhambi yake.

Na tumewatilia uadui na chuki baina yao mpaka siku ya Kiyama.

Mwenye Tafsir Al-Manar amesema: "Hajui katika Tafsiri zilizopokelewa kutoka kwa waliotangulia ila ni kuwa dhamiri katika 'Baina yao' inawarudia mayahudi na wakristo walioelezwa katika kauli yake Mwenyezi Mungu: "Enyi mliaoamini msiwafanye mayahudi na manaswara marafiki."

Na katika Tafsir za kisasa wanasema kuna uwezekano wa kuwa dhamiri ni ya mayahudi peke yao. Sisi tuko kwenye rai ya waliotangulia kwa sababu mbili:

Kwanza: kwa sababu wao ndio wajuao zaidi misamiati ya Qur'an na Hadith kuliko waliokuja baadaye. Kwani wao wako karibu zaidi na zama za mtume na kushuka Qur'an.

Pili: kwa sababu uadui baina ya mayahudi na manaswara upo. Mayahudi wanaitakidi kuwa Masih ni mdanganyifu, mwenye hila na mtoto wa zina - Mungu apishe mbali - Na manaswara (Wakristo) wanaitakidi kuwa yeye ni mwana wa mungu, ambapo Waislamu wanaitakidi kuwa yeye ni Mtume aliyetakaswa na ujinga na maasi. Kwa hiyo ni muhali kuondoka uadui baina ya mayahudi na wakristo maadam kila upande una itikadi yake.

Alijaribu Papa wa Roma mnamo mwaka 1965 kuyasogezza pamoja makundi mawili, lakini Mayahudi bado wanang'angania rai yao kwa Bwana Masih ^(a.s). Hata hivyo kuna aina ya ushirikiano wa kitamaa, bali wakuu wa mashirika wameungana pande zote mbili lakini kwa misingi ya kibiashara tu, sio misingi ya dini.

MAYAHUDI NA MOTO WA VITA

Kila mara wanapowasha moto wa vita Mwenyezi Mungu anauzima. Neno 'vita' tangu mwanzo lilipowekwa liliwekwa kwa maana ya kupigana na kuuana. Limetumika kwa maana haya karne kwa karne. Siku zilipoendelea kupita nalo likakua mpaka hivi sasa limekuwa na maana ya kutokuwepo amani na raha.

Nchi yoyote inayohofia kuvamiwa na nchi yenye nguvu zaidi au maisha yake yakapanda kwa sababu ya vita viliwyoko nchi nyingine, basi nayo iko katika hali ya vita, hata kama halimwagiki tone la damu katika ardhi yake. Kwa sababu imeathirika na vita na vikaikosesha amani na raha.

Baada ya ishara hii, hebu tujiulize Je, Makusudio ya vita katika Aya ni kuhusu kuaana tu, au ni pamoja na kukosekana amani na raha? Kisha ikiwa makusudio ni mayahudi, kama waliwyosema wafasiri, kutakuwa na majibu gani kuhusu vita vya 5 Juni 1967 viliwyowashwa na Mayahudi na ambavyo moto wake hauzimiki mpaka sasa?

Jibu: Neno Vita katika Aya makusudio yake ni kuuana. Kwa sababu neno hili wakati huo halikuwa na maana zaidi ya haya. Ama kuhusu vita vya 5th Juni, tunajibu kama ifuatavyo:

1. Wameafikiana wafasiri kuwa makusudio ya mayahudi ni kuwahuusu mayahudi waliokuwa wakimfanyia vitimbi Mtume wa Mwenyezi Mungu na waislam. Katika vitabu vya sera imeelezwa kuwa mayahudi wa Madina waliungana na washirikina dhidi ya Mtume na Sahaba zake na kwamba wengine walikuwa wakiwasaidia maadui zao.

2. Lau tukichukulia kuwa makusudio ni mayahudi katika kila zama kwa kuchukua dhahiri ya ujumla, basi tukio la tarehe 5 Juni, halikuwa ni vita kwa maana yaliyo maarufu ya neno hili isipokuwa yalikuwa mauaji ya siri na usaliti wa woga. Kwani hata usiku huo huo Israil na Washington zilikuwa zikisisitiza kwamba hazikuanza mashambulizi, bali hata baada yake Israil ilitangaza kuwa Waarabu ndio walioanza vita.

Kisha baadaye uhakika ukadhihiri kwamba vita hivyo vya mwaka 1967 havikuwa baina ya waarabu na mayahudi isipokuwa vilikuwa hasa ni baina ya waarabu na waamerika. Amerika ndiyo iliyokuwa mhandisi, mwamrishi na mtoaji silaha na mali. Vile vile ilikuwa ndio mpangaji wa udanganyifu na mlinzi, Israil ilitekeleza kazi ya askari mtiifu.

Mtungaji wa kitabu tulichokielezea punde hivi, anasema: "Magazeti ya Ufaransa na Ujerumani yalieleza kuwa majasusi wa Kiamerika, kabla ya uchokozi kuanza, waliipa Israil habari zote muhimu, kuongezea faili maalum la Mashariki ya kati walilokuwa nalo viongozi wa Umoja wa NATO. Na kwamba aliyetua amri kwa Israil kushambulia Waarabu kwa niaba ya Rais Johnson, ni mshauri wake myahudi. Na kamanda wa Kiamerika mfukoni mwake alikuwa na amri ya kutekeleza maandalizi ya vita katika sehemu zote zilizo chini yake. Ama meli ya ujasusi USS liberty, ilikuwa ikifanya kazi kwa ushirikiano wa Amerika na Israil.

3. Moto wa vita uliowashwa na Washington au kibaraka wake, Israil, ameuzima Mwenyezi Mungu bila ya shaka yoyote. Waliouwasha moto huo walikiri mara nyingi na kutangaza magazetini na kwenye idhaa kwamba haukutimiza lengo lililotakiwa - kumaliza uongozi wa kuwakomboa waarabu na kuwafanya wasalimu amri bila ya masharti yoyote, na hatimae kutatua matatizo ya Israil ya kisiasa.

Wakati huo huo tukio la mwaka 1967 liliwa ni mtihani mgumu kwa waarabu na kusisitiza dharura ya kutatua matatizo ya kimsingi. Vile vile kufahamu ni nani maadui zao na ni nani marafiki zao. Hata kama tukio hilo limeleta faida ya kufichuka vibaraka tu, inatosha.

Na wanajitahidi kuleta ufisadi katika ardhi.

Kwa sababu lengo lao la dhambi haliwezi kuthibitika ila kwa kuleta uharibifu na fitina. Wakuu katika Israil wamesema wazi kuwa kubakia kwa dola yao na uhai wake kumewekwa rahani na mizozo ya viongozi wa nchi za Kiarabu, 'Je yuko mwenye kukumbuka?'

Na Mwenyezi Mungu hawapendi wafisadi.

Hapo ndio mwisho wao - Maangamivu - hata kama muda utarefuka.

Na lau kwamba watu wa Kitab wangeliamini na wakamcha Mungu, tungeliwafutia makosa yao na kuwaingiza katika Bustani (pepo) zenye neema.

Huu ni mwito kutoka kwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) kwa Mayahudi na Wakristo kuwa watubie na waingie katika Uislam. Na kama wataitikia mwito wako atawafutia madhambi yao yote, hata yakiwa makubwa; Kwa sababu Uislamu unafuta yaliyokuwa kabla yake; kama ilivyoolewa katika Hadith: "Na wakimcha Mwenyezi Mungu baada ya kusilimu kwao, basi Mwenyezi Mungu atawaingiza katika bustani ambazo hupita chini yake mito."

RIZIKI NA UFISADI

Lau wangalisimamisha Tawrat na Injil na yale yaliyoteremshwa kwao kutoka kwa Mola wao, kwa hakika wangelikula vyatuu yao na vyatuu chini ya miguu yao.

Kuisimamisha Tawrat na Injil ni kufanya vitendo kulingana na vitabu hivyo. Makusudio ya yaliyoteremshwa kwao, ni mafunzo waliyokuwa wakiyasikia kutoka kwa Mitume, yanayojudikana kama Hadith za Mtume. Vilivyo juu yao, ni fumbo la riziki kubwa, sawa na unavyosema: Fulani amejawa na neema kuanzia utosini hadi unyayoni. Kuna Aya nyingi zilizo katika maana ya Aya hizi, kama hivi ifuatavyo:-

﴿وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ آمَنُوا وَاتَّقُوا لَفَتَحْنَا عَلَيْهِمْ بَرَكَاتٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ﴾

"Na lau watu wa miji wangaliamini na wakawa na takua, hakika tungaliwafungulia baraka kutoka mbinguni na ardhini" (7:96)

﴿إِنَّ اللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko kwa kaumu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao" (13:11)

﴿ظَاهِرُ الْفَسَادِ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ﴾

"Umedhihiri ujisadi barani na baharini kwa iliyoyachuma mikono ya watu" (30:41)

﴿وَمَا أَصَابَكُمْ مِّنْ مُّصِيبَةٍ فَإِمَّا كَسَبَتْ أَيْدِيْكُمْ﴾

"Na misiba inayowasibu ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu" (42:30)

Aya zote hizi zinatuongoza kwenye mambo mawili:

Kwanza: kudhihiri ujisadi, ukiwemo umasikini maradhi na ujinga ni hukumu kutoka duniani na wala si hukumu ya mbinguni. Na ni kutokana na mikono ya watu walioiua haki na kuihuisha batili, na wala sio kutokana na kadha na kadari ya Mwenyezi Mungu. Na kwamba kundi lolote litakalojua haki na kuitumia litaishi kwa raha na wema.

Pili: Ibara ya kaumu na watu katika Aya hizo tukufu, inafahamisha kuwa uovu utakuwa katika hali yote kwa ujumla; na kwamba kuwa mwema mtu mmoja hakusaidii kitu maadamu wako watu wafisadi, bali wema wake utamwingiza kwenye balaa na Mashaka. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿وَأَنْذَلُوكُمْ فِتْنَةً لَا تُصِيبَنَّ الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْكُمْ خَاصَّةً﴾

"Na iogopeni fitna ambayo haitawasibu waliodhulumu tu kati yenu (8:25)"

Yaani athari ya ujisadi na uovu katika jamii mboru inaenea kwa wote wema na waovu. Hakuna mwenye shaka kwamba taifa vivu linalonyenyeka dhuluma, halina budi kuishi maisha ya udhalili na unyonge. Kwa hiyo basi makusudio ya imani inayoleta riziki ni kumwamini Mwenyezi Mungu pamoja na kutumia hukumu zake zote na misingi yake yote na wala sio kusimamisha Swala tu, bali na kutoa Zaka na kuwakomboa wanaokandamizwa na kusimamisha uadilifu katika kila kitu. Pia hakuna mwenye shaka kuwa uadilifu ukienea na ukawa juu, basi hali nayo itakuwa nzuri na umasikini na uovu utakwenda zake, Hili ndilo lengo la Qur'an.

Uislamu umegundua kuwa kuna mfungamano mkubwa baina ya ujisadi na maendeleo. Na Uislamu umemtangulia, katika kujua hakika hii, kila mtaalamu katika wataalamu wa elimu ya jamii ni kila kada katika makada wa ujamaa, wa kidemokrasia na wengineo.

Wote hawa wakiwa wana kitu cha kutaja, basi watakuwa wamechukua kutoka katika Uislamu, Lakini kuna hila gani kwa ambaye anakimbia kila linalolenga kwenye dini, kwa vile tu lina jina la dini?

Miongoni mwao wako watu walio sawa, na wengi wao wanayoyafanya ni mabaya.

Dhamiri ya katika wao inawarudia watu wa Kitab walijotajwa kwa uwazi katika Aya amba ni mayahahudi na wakristo. Na amba Mwenyezi Mungu ameiwasifu kuwa wako sawa ni wale waliokubali Uislamu katika mayahudi na wakristo, baada ya kuwadhihirikia wao dalili ya haki na ubainifu wa

ukweli. Watu wa historia na sera wametaja majina mengi ya watu wa Kitab waliosilimu. Ama wale walioung'ang'ania ukafiri baada ya kuwabainikia wao haki, ndio waliokusudiwa katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: "Na wengi wao wanayoyafanya ni mabaya"

9

TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

﴿يَا أَيُّهَا الرَّسُولُ بَلَغْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَغْتَ رِسَالَةَ اللَّهِ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ﴾

67. Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako; na kama hutafanya, basi hukufikisha ujumbe wake. Na Mwenyezi Mungu atakulinda na watu, Hakika Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri.

FIKISHA ULIYOTEREMSHIWA

Aya 67

MAANA

Dhahiri ya Aya inafahamisha kuwa kulikuwa na jambo muhimu aliloteremshiwa Mtume (**s.a.w.w**) na kuamriwa kulifikisha kwa watu. Akawa anaona uzito kulifanya, kwa sababu ni zito katika nafsi zao. Akasitasita akingoja hali na minasaba maalum, kwa kuepuka migongano na wale wanaopindua mambo, lakini Mwenyezi Mungu (**s.w.t**) akamuhimiza kulifikisha wakati huo huo bila ya kufikiria lolote. Na Mwenyezi Mungu (**s.w.t**) atamuhami na kumlinda na machukivu yote.

Unaweza kuuliza: kauli yake Mwenyezi Mungu "Na kama hutafanya basi hukufikisha ujumbe wake" haina faida yoyote, kwani jawabu lake ni hilo hilo swalii. Ni kama kusema: Kama hukufanya basi hukufanya, Je, kuna wajihii gani?

Jibu: Kauli hii inafahamisha kuwa jambo hili ambalo Mtume anasitasita nalo, katika kulifikisha kwa kuhofia watu, limefikia umuhimu kuweza kulinganishwa na kufikisha ujumbe wote, kiasi ambacho, akiacha kulifikisha basi ni kama ameacha kufikisha ujumbe wote; sawa na unavyomwambia mtu aliyekufanya hisani kama hutafanya hivi, basi hujanifanya hisani kabisa.

Kwa hiyo maana yake ni kuwa kama hukufikisha jambo hili, basi ni kama hukutekeleza chochote katika risala yangu, na malipo yake ni malipo ya aliyeficha hukumu zake zote.

Swali la pili: Je, ni jambo gani hilo lililofikia kiwango hiki mpaka Mwenyezi Mungu akalipima na risala yote katika kulifikisha kwake, na likamfanya Mtume asitesite kulifikisha na hali yeye ni mwenye kupupia kudhihirisha aliloamrishwa kwa vyovyyote iwavyo?

Jibu: Baada ya kuafikiana wafasiri wa Kishia na Kisunni kuhusu tafsir ya Aya hii kwa maana tuliyoyataja wamehitafiana katika kulielezea jambo hilo lililomfanya Mtume (**s.a.w.w**) kusitasita kulifikisha na ambalo Mwenyezi Mungu hakulitaja kwa uwazi.

Shia wanasema kuwa Aya hii ilishuka kwa Ali bin Abu Talib na jambo lenyewe lilikuwa ni utawala wake kwa watu, na kwamba Mtume alisitasita

katika kulifikisha si kwa kuhofia nafsi yake, hapana si hivyo! Yeye alivikabili vigogo vya Kiquraish na ukubwa wao akawatukana miungu yao na kuwaabisha wafu wao na hali wao wana nguvu na hadhi za kijahiliya.

Aliyafanya yote haya Mtume na hakuogopa lawama ya mwenye kulaumu hata siku moja.

Itakuwaje aogope kufikisha hukumu yoyote miongoni mwa hukumu baada ya kuwa Uislamu una ngome kubwa ya jeshi lenye nguvu? Isipokuwa Mtume (**s.a.w.w**) alihofia kumuelezea Ali kuwa Khalifa, kutuhumiwa kuwa na upendeleo kwa kuwa ni mkwewe na binamu yake, na kwamba makafiri na wanafiki wanawenza kulifanya hili ni jambo la kueneza propaganda dhidi ya Mtume (**s.a.w.w**) na kuingiza shaka katika Utume wake na isma yake. Na ilivyo hasa ni kuwa propaganda kama hii wanaikubali wenyewe akili hafifu na wajinga.

Kwa muhtasari, haya ndiyo waliyoyasema Shia na kuyatolea dalili kwa hadith zilizopokelewa kutoka hata kwa Sunni. Wamezinukuu baadhi, Razi na mwenye Tafsir Al-manar .

Ama Sunni, wametofautiana; kuna wenyewe kusema kuwa Mtume alinyamazia baadhi ya hukumu zinazohusiana na Mayahudi, wengine wakasema kuwa hukumu aliyoinyamazia Mtume inaambatana na kisa cha Zaid na Zainab bint Jahsh.

Kundi kubwa katika Sunni wamesema kuwa Aya ilishuka katika ubora wa Ali bin Abu Talib na si katika ukhalifa wake. Na kauli hii alinukuu Razi na mwenye Tafsir Al- Manar.

Anasema Razi: " Ya kumi- yaani kauli ya kumi- ni kuwa Aya imeshuka kuhusu ubora wa Ali bin Abu Talib. Iliposhuka Aya hii Mtume aliushika mkono wa Ali na akasema: "Ambaye mimi ni bwana wake basi Ali ni bwana wake. Ewe Mwenyezi Mungu mpende mwenye kumpenda na muhasimu mwenye kumhasimu" Umar akamkabili na kusema: "Pongezi Ewe bin Abu Talib, umekuwa bwana wangu na bwana wa kila mumin mwanamume na mwanamke." Hiyo ni kauli ya Ibn Abbas, Barrau bin Azib na Muhammad bin Ali".

MWENYE AL-MANAR NAAHLUBAYT

Amesema mwenye Tafsir Al-Manar: "Ama Hadith isemayo: Ambaye mimi ni bwana wake basi Ali ni bwana wake, ameipokea Ahmad katika Musnadi yake. Vilevile Tirmidh, Nasai, Dhiyai katika Mukhtar na Ibn Maja na baadhi yao wameifanya ni Hasan; na Dhahabi akaifanya Sahih kwa tamko hili na akaitilia nguvu Isnad ya mwenye kuzidishia: "Ewe Mwenyezi Mungu mpende mwenye kumpenda na mhasimu mwenye kumhasimu."

Kuna Riwaya nyingine isemayo kuwa yeche Mtume aliwahutubia watu, akataja misingi ya dini, akawausia Ahlu bayt wake na akasema: "Mimi ninawachia vizito viwili: Kitab cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu Ahlubayt wangu, basi angalieni vile mtakavyonifuata nyuma yangu katika viwili hivi, kwani havitaachana mpaka vinijie katika birika (siku ya kiyama). Mwenyezi Mungu ni Bwana wangu na mimi ni Bwana wa kila mumin.

Kisha akashika mkono wa Ali na akasema maneno hayo: yaani; ambaye mimi ni bwana wake basi Ali ni bwana wake". Kisha mwenye Al-Manar akaendelea kurefusha maneno akasema katika aliyejasema: " Makusudio ya

Wilaya katika Hadith ni kumsaidia na kumpenda". Lakini tafsir yake hii alifuatishia na kauli hii. "Mfano wa mjadala huu umetofautisha baina ya waislam na kuwaingizia uadui na chuki, maadamu ubaguzi na madhehebu una nguvu kwa watu basi hakuna matumaini ya kuitofanyia utafiti haki katika masuala ya ukhalifa."

Haya ni sahihi anayakubali kila mwenye akili, Lau si kung'ang'ania batili isingelitokea tofauti baina ya Waislamu, wala yasingeliandikwa marundo ya vitabu katika suala moja. Mwenye Tafsir Al-Manar anaendelea kusema: "Ama Hadith ya ambaye mimi ni bwana wake basi Ali ni bwana wake, sisi tunaifuata na tunampemda Ali Al-Murtadha, tunampenda amependaye na tunamchukia amchukiaye. Hilo tunalihisabu kama kumpenda Mtume wa Mwenyezi Mungu (**s.a.w.w**) na tunaamini kuwa kizazi chake Mtume (**s.a.w.w**) hakitafarikiana na Kitab ambacho Mwenyezi Mungu amemteremeshia Mtume wake (**s.a.w.w**), na kwamba Kitab na kizazi cha Mtume ni Makhalifa wawili wa Mtume. Hadith imekua sahihi kwa hilo katika matukio mengine yasiyokuwa kisa cha Ghadir. Kwa hiyo wakikubaliana katika jambo fulani tunalikubali na kulifuata na wakitofautiana katika jambo basi tutalirudisha kwa Mwenyezi Mungu na Mtume."

﴿قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَسْتُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ حَتَّىٰ تُقْبِلُوا التَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ مِّنْ رَّبِّكُمْ وَلَيَزِدَنَّ كَثِيرًا مِّنْهُمْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَّبِّكَ طُغْيَانًا وَكُفْرًا فَلَا تَأْسُ عَلَىٰ الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ﴾

68. Sema: "Enyi watu wa Kitab! Hamna chocrote, mpaka muisimamishe Tawrat na Injil na yaliyoteremshwa kwenu kutoka kwa Mola wenu. Kwa hakika yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola wako yatawazidisha wengi katika wao uasi na ukafiri, Basi usiwasakiitikie watu makafiri.

﴿إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالصَّابِئُونَ وَالنَّصَارَىٰ مِنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَعَمِّ لَ صَالِحًا فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ﴾

69. Hakika wale walioamini na wale walio mayahudi na wasabai na wanaswara, watakao mwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na wakafanya amali njema, basi wao hawatakuwa na hofu wala hawatahuzunika.

KUSIMAMISHA TAURAT NA INJIL

Aya 68 - 69

MAANA

Sema: Enyi Watu wa Kitab! Hamna chocrote.

Wala hayatawafaa mambo ya dhahiri haya ya kidini mpaka muisimamishe Tawrat na InjilImekwisha tangulia tafsiri ya Aya hii katika Sura hii Aya 64.

Hakika wale walioamini na wale walio mayahudi na wanaswara na wasabai.

Pia imetangulia tafsir yake katika (2:62)

﴿لَقَدْ أَخَذْنَا مِيشَاقَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَأَرْسَلْنَا إِلَيْهِمْ رُسُلًا كُلَّمَا جَاءُهُمْ رَسُولٌ بِمَا لَا تَهْوَى أَنفُسُهُمْ فَرِيقًا كَذَّبُوا وَفَرِيقًا يَقْتُلُونَ﴾

70. Hakika tulifanya agano na Wana wa Israil na tukawapelekea Mitume. Kila alipowafikia Mtume kwa yale zisiyoyapenda nafsi zao kundi moja wakalikadhibisha na kundi jengine wakaliua.

﴿وَحَسِبُوا أَلَا تَكُونُ فِتْنَةٌ فَعُمُوا وَصَمُوا ثُمَّ تَابَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ ثُمَّ عَمُوا وَصَمُوا كَثِيرٌ مِّنْهُمْ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ﴾

71. Na walidhani kwamba haitatokea fitna, basi wakawa vipofu na viziwi. Kisha Mwenyezi Mungu akawatakabalia toba, kisha tena wengi katika wao wakawa vipofu na viziwi; na Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyatenda.

AGANO LAWANAWA ISRAIL

MAANA

Hakika tulifanya agano na Wana wa Israil.

Imekwishatangulia tafsir yake katika Sura hii hii Aya 12 na 13. Wafasiri wamesema kuwa Mwenyezi Mungu (s.w.t) amekariri kufanya agano na Mayahudi na kuvunja kwao ahadi na maagano kwa kuwaa Mitume, kwa kusititiza ujeuri na uasi wao. Nasi tunaongeza kwa kusema kuwa vilevile Mwenyezi Mungu Mtukufu amekusudia kwa kukaririka huku - Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi - kuvihadharisha vizazi nya kiislam, kutokana na vizazi nya kiyahudi. Ambapo alikwishajua kuwa Waislamu watatawanyika kwenye makundi na vijidola, na kwamba Mayahudi watautumia mgawanyiko huu kwa kuanzisha dola ndani ya miji ya kiislam, na kuwa kama ilivyokuwa.

Na tukawapelekea Mitume wawabainishie haki na uongozi, lakini kila walipowajia Mitume kwa yale zisiyoyapenda nafsi zao, kundi moja wakaliadhibisha na kundi jengine wakaliua.

Mapenzi ya nafsi tu, ndiyo mwamrishi na mkatazaji kwa mayahudi. Wala hakuna malipo kwa atakayewahalifu, hata akiwa ni Mtume, ila kumuua wakiweza au kumkadhibisha wakashindwa kuua. Sifa hizi hawahuksiki nazo mayahudi tu, ingawaje maneno ni yao. Kila mwenye kuhadaika na mapenzi yake anafanya kama walivyofanya; awe myahudi, Mwislamu au Mkiristo.

Na walidhani kwamba haitatokea fitna.

Makusudio ya fitna hapa ni shida, kama vile kukandamizwa na waliokuwa na nguvu zaidi kwa kuuliwa na kufukuzwa. Yaani walidhani Mayahudi kuwa wao hawatashindwa kabisa, kwa vile wao ni taifa la Mwenyezi Mungu lililoteuliwa kama wanavyodai. Zamani walitegemea madai yao haya, lakini hivi sasa wanategemea nguvu za wakoloni, hali ya ujinga wa watu, mashirika ya ulangazi na kueneza fitina, ufisadi na kuwatofautisha watu.

Basi wakawa vipofu na viziwi.

Kila mwenye kuchukia jambo anakuwa kipofu wa mazuri yake. Mayahudi walichukia kila jambo isipokuwa linalopendeza nafsi zao, Kwa hiyo wamekuwa vipofu wa njia ya haki na kuwa viziwi wa sauti ya uadilifu. Ndipo Mwenyezi Mungu akawasalitia babilon, wakawaua wanaume wao na kunyang'anya mali zao na kuwateka wanawake wao na watoto wao.

Kisha Mwenyezi Mungu akawatakabalia toba.

Baada ya kutubia kutokana na shida waliyoipata kutoka kwa Nebukadnezza ya kudhalilishwa na kudharauliwa.

Kisha tena wengi katika wao wakawa vipofo na viziwi.

Yaani baada ya Mwenyezi Mungu kuwaokoa na adhabu ya kutekwa, wengi wao walirudia ujisadi na dhulma. Wakamuwa Zakariya na Yahya; wakamkadhibisha Masih na kujaribu kumuua na wakasema kuhusu yeye na mama yake mambo makubwa. Ndipo Mwenyezi Mungu akawasalitia

Wafursi na Waroma, wakawafanya kama walivyofanywa na Nebukadnezza.

Na Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyatenda.

Ya kumwaga damu, kuipotosha, haki, kupanga njama na kutekekeleza kila njia na inayopangwa na taghuti na dhalimu, Mwenyezi Mungu (s.w.t) anayajua yote naye atawalipa udhalili hapa duniani kabla ya akhera. Sifa zote hizi alizozielezea Mwenyezi Mungu kuhusu mayahudi zinalingana sawa kabisa na mwenye kudhahirisha Uislamu kisha anazunguka kwa wale wanaoingwa mkono Israil na kuwasaidia.

﴿لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ وَقَالَ الْمَسِيحُ يَا بَنِي إِسْرَائِيلَ اعْبُدُوا اللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ إِنَّهُ مَنْ يُشْرِكُ بِاللَّهِ فَقَدْ حَرَمَ اللَّهُ عَلَيْهِ الْجَنَّةَ وَمَأْوَاهُ النَّارُ وَمَا لِلظَّالَّمِينَ مِنْ أَنْصَارٍ﴾

72. Kwa hakika wamekufuru wale waliosema Mwenyezi Mungu ni Masih mwana wa Maryam. Na Masih alisema: Enyi wana wa Israil! Mwabuduni Mwenyezi Mungu Mola Wangu na Mola wenu: kwani anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu amemharamishia pepo na makazi yake ni motoni. Na madhalimu hawatakuwa na wakuwanusuru.

﴿لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ ثَلَاثَةٍ وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا إِلَهٌ وَاحِدٌ وَإِنْ لَمْ يَنْتَهُوا عَمَّا يَقُولُونَ لَيَسَّنَ الَّذِينَ كُفَّارُوا مِنْهُمْ عَذَابُ أَلِيمٍ﴾

73. Kwa hakika wamekufuru wale waliosema, Mwenyezi Mungu ni wa tatu wa utatu. Hakuna Mungu ila Mungu Mmoja. Na kama hawataacha hayo wayasemayo, kwa hakika itawapata, wale waliokufuru mionganini mwao, adhabu iumizayo.

﴿أَفَلَا يَتُوبُونَ إِلَى اللَّهِ وَيَسْتَغْفِرُونَهُ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

74. Je, hawatubu kwa Mwenyezi Mungu na kumwomba maghfira? Na Mwenyezi Mungu ni mwangi wa maghfira mwenye kurehemu.

﴿مَا الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ وَأُمُّهُ صِدِّيقَةٌ كَانَا يَأْكُلُانِ الظَّعَامَ ا�ُظْرَ كَيْفَ نُبَيِّنُ لَهُمُ الْآيَاتِ ثُمَّ انْظُرْ أَنَّى يُؤْفَكُونَ﴾

75. Masih mwana wa Maryam hakuwa ila ni Mtume, Wamepita kabla yake Mitume. Na mama yake ni mkweli, Wote wawili walikuwa wakila chakula, Angalia jinsi tunavyowabainishia ishara, kisha angalia jinsi wanavyogezuwa.

MWITO WA MASIH KWAWANAWA ISRAIL

Aya 72 - 75

MAANA

Kwa hakika wamekufuru wale waliosema: Mwenyezi Mungu ni Masih mwana wa Maryam.

Mayahudi walipita kiasi kumdharaau Masih na mama yake na wakristo nao wakapita kiasi katika kumsifu, mpaka wakampandisha kwenye cheo cha uungu. Kupita kiasi, katika mtazamo wa Uislam, ni ukafiri kwa aina zake zote. Imam Ali ^(a.s) anasema: "**Watu wawili wataaangamia kwa ajili yangu: Mwenye kunipenda kupita kiasi, pendo likampelekea kusiko na haki, na mwenye kunichukia kupita kiasi, chuki ikampelekea kusiko haki. Mbora wa watu kuhusu mimi ni yule mwenye hali ya katikati, basi shikamaneni naye**".

Na Masih alisema: Enyi wana wa Israil, mwabuduni Mwenyezi Mungu Mola Wangu na Mola Wenu; kwani anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu amemharamishia pepo na makazi yake ni motoni. Na madhalimu hawatakuwa na wa kuwanusuru.

Masih ni katika Wana wa Israil na aliowaonya kwanza ni jamaa zake. Akawaaamrisha kumwabudu Mwenyezi Mungu peke yake, akikiri kuwa yeye ni Mola wake na Mola wao, na kuwaonya wanaomshirikisha Mwenyezi Mungu kuwa watapata adhabu kali, lakini Wakristo wamekataa hayo, isipokuwa Isa ni Mwenyezi Mungu tu, na mwenye kupinga hayo, basi amempinga muumbaji wa ulimwengu, katika itikadi yao.

Kwa hakika wamekufuru wale waliosema Mwenyezi Mungu ni wa tatu wa utatu.

Kwanza Mwenyezi Mungu (s.w.t) amewakanushia Manasara uungu wa Bwana Masih, kisha katika Aya hii amewakanushia kumfanya kwao Mwenyezi Mungu ni mmoja kati ya watatu.

Kwa kusema kwao kuwa Mwenyezi Mungu ni baba na Masih ni Mwana, kisha baba na Mwana wakachanganyika na kuungana akawa roho mtakatifu. Kila mmoja kati ya hawa watatu ni mwengine na huyo mwengine ni yeye. Yametangulia maelezo ya hilo katika tafsir ya (4:170) na tafsir ya Aya 17 ya Sura hii tulio nayo.

Hakuna mungu ila Mungu Mmoja.

Imam Ali aliulizwa kuhusu Tawhid na Uadilifu wa Mungu, akasema: "Tawhid ni kutomuwazia, na uadilifu ni kutomtuhumu." Yaani kumpwekesha Mwenyezi Mungu ni kutomfanya picha yoyote katika mawazo yako kwa sababu kila linalowaziwa lina mpaka na Mwenyezi Mungu hawezি kuwekewa mpaka na mawazo. Na uadilifu ni kutomtuhumu Mwenyezi Mungu kwa hekima yake kwamba yeye amefanya lisilotakiwa kufanya.

Na kama hawataacha hayo wayasemayo, kwa hakika itawapata, wale walio kufuru mionganoni mwao, adhabu iumizayo.

Unaweza kuuliza kuwa: katika Aya neno 'mionganoni mwao' kwa dhahiri linafahamisha kwa mionganoni mwao wako makafiri na waumini; na inajulikana kuwa wote wanasema uungu wa Isa, na Mwenyezi Mungu (s.w.t) anasema: "Hakika wamekufuru wale waliosema: Mwenyezi Mungu ni Masih mwana wa Maryam?"

Wafasiri wamejibu kuwa: neno 'mionganoni mwao' linawatoa waliotubia na kusilimu na kuwabakisha wanaoendelea na ukafiri. Lakini ilivyo ni kuwa

mwenye kusilimu hawezi kuhisabiwa kuwa ni mionganini mwao. Ilivyo ni kuwa Wakristo walikuwa na itikadi ya Tawhid (Umoja wa Mungu) kwa muda mrefu, kisha wakagawanyika makundi mawili: Lile linaloamini Tawhid na jingine linaloamini idadi ya waungu. Wakaendelea hivyo, kisha wakaafikiana wote na neno la utatu. Kwa hiyo, basi neno mionganini mwao linatoa kundi lile lililoamini Utume wa Isa na sio Ungu wake. Yametangulia maelezo kwa ufanuzi katika kufasiri Aya 17 ya Sura hii.

Je, hawatubu kwa Mwenyezi Mungu na kumwomba maghufira? Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa maghufira mwenye kurehemu?

Maneno yako wazi kabisa, lakini pamoja na uwazi wote huo baadhi ya wafasiri wamekataa ila kufafanua tu, na kusema kuwa hapa kuna maneno yaliyokadiriwa, kuwa hawasikii tunayowaambia wakatubia, Hivi ndivyo kinavyokuwa kitu baridi kilichoganda kikiwa mahali pasipokuwa kwake.

Masih mwana wa Maryam hakuwa ila ni Mtume, Wamepita kabla yake Mitume.

Kama vile Nuh, Ibrahim, Musa na wengineo. Mwenyezi Mungu alidhihirisha miujiza mikononi mwao, kama alivyoidhihirisha mikononi mwa Isa. Kwa hiyo kauli ya Uungu wake haina nguvu yoyote. Na mama yake ni mkweli. Mwenyezi Mungu ameibaini maana ya kuwa mkweli aliposema:

﴿وَصَدَّقْتُ بِكَلِمَاتِ رَبِّهَا وَكُنْبِهِ وَكَانَتْ مِنَ الْقَانِتِينَ﴾

"Na akayasadikisha maneno ya Mola wake, na vitabu vyake, na alikuwa mionganini mwa wanyenyeku" (66:12)

Wote wawili walikuwa wakila chakula.

Kila mwenye kuhitajia kitu chochote, ijapokuwa ni mahali, au wakati, basi huyo ni kiumbe aliyeumbwa. Kwa sababu anahitajia kwa hali yoyote, vinginevyo itakuwa ni muumbaji asiyembwa; kama ambavyo kujitosheleza ni sifa inayolazimiwa na Muumbaji na wala haepukani nayo, vinginevyo atakuwa ameumbwa.

Ilivyo ni kuwa anayekula chakula huwa ni muhitaji sana, kwa hiyo huyo ni kiumbe na wala siye muumba. Ni jambo la kushangaza kufichika uwazi huu kwa mwenye akili. Na kwa mantiki haya na ufasaha wake, anaifuatishia msimamo wao huo kwa kauli yake: **Angalia jinsi tunayvowabainishia ishara**.

Na mionganini mwa ishara hizo ni kwamba Masih na mama yake walikuwa wakila chakula, basi vipi watakuwa waungu? Kisha Angalia jinsi wavavyogeuzwa, yaani kuicha haki na kuikadhibusha kwao.

﴿قُلْ أَتَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَمْلِكُ لَكُمْ صَرَّارًا وَلَا نَفْعًا وَاللَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ﴾

76. Sema: Je, mniamwabudu badala ya Mwenyezi Mungu, ambaye hawezi kuwadheru wala kuwanufaisha? Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia, mwenye kujuu.

﴿قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لَا تَغْلُبُوا فِي دِينِكُمْ غَيْرُ الْحُقْقَى وَلَا تَتَّبِعُوا أَهْوَاءَ قَوْمٍ قَدْ ضَلُّوا مِنْ قَبْلٍ وَأَخْضُلُوا كَثِيرًا وَضَلُّوا عَنْ سَوَاءِ السَّبِيلِ﴾

77. Sema: "Enyi watu wa Kitab! Msipite kiasi katika dini yenu bila haki, wala msifuate matamanio ya watu waliokishapotea tangu zamani; na wakawapoteza wengi, na wenyewe wakapotea njia iliyo sawa.

﴿لِعْنَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ بَنِي إِسْرَائِيلَ عَلَى لِسَانِ دَاؤُودَ وَعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ ذَلِكَ بِمَا أَعْصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ﴾

78. Walilaaniwa wale waliokufuru mionganoni mwa wana wa Israel kwa ulimi wa Daud na wa Isa mwana wa Maryam. Hayo ni kwa sababu waliasi, nao walikuwa wakiruka mipaka.

﴿كَانُوا لَا يَتَأَهَّلُونَ عَنْ مُنْكَرٍ فَعَلُوهُ لَيْسَ مَا كَانُوا يَفْعَلُونَ﴾

79. Walikuwa hawakatazani mambo mabaya waliyokuwa wakiyafanya. Hakika ni maovu waliyokuwa wakiyafanya.

﴿تَرَى كَثِيرًا مِّنْهُمْ يَوَّلُونَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَيْسَ مَا قَدَّمْتُ لَهُمْ أَنفُسُهُمْ أَن سَخَطَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَفِي الْعَذَابِ هُمْ خَالِدُونَ﴾

80. Utawaona wengi katika wao wanawafanya marafiki wale waliokufuru. Kwa hakika ni mabaya waliyotanguliziwa na nafsi zao; ya kwamba Mwenyezi Mungu amewakasirikia na watadumu katika adhabu.

﴿وَلَوْ كَانُوا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالرَّبِّيِّ وَمَا أُنْزِلَ إِلَيْهِ مَا اتَّخَذُ دُوْهُمْ أُولَئِيَّةً وَلَكِنَّ كَثِيرًا مِّنْهُمْ قَاسِقُونَ﴾

81. Na lau wangelikuwa wanamwamini Mwenyezi Mungu na Nabii na yale yaliyoteremshwa kwake wasingeliwfanya hao kuwa marafiki. Lakini wengi katika wao ni mafasiki.

HAWAWEZI KWADHURU WALA KUWANUFAISHA

Aya 76 - 81

NAHW

Qur'an hutumia herufi Ma katika kisichokuwa na akili na kilicho na akili na katika vyote viwili. Hata hivyo matumizi ya herufi Ma katika visivyo na akili ni zaidi.

MAANA

Sema Je, mnambabudu badala ya Mwenyezi Mungu, ambaye hawezi kuwadheru wala kuwanufaisha? Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia mwenye kujua?

Hoja juu ya Wakristo katika Aya hii ni kwamba Mwenyezi Mungu mwenye kuabudiwa ni yule anayeweza kuwadheru waja wake au kuwanufaisha.

Ama anayeshindwa na hayo, basi ni muhali kuwa Mungu. Injili zimetaja kuwa Isa, wanayedai kuwa ni Mungu, alidharauliwa, akasulubiwa na kuzikwa baada ya kuvishwa kilemba cha miba kichwani mwake, Ambaye hawezi kujikinga yeye mwenyewe basi atawezwa wapi kumkinga mwengine? Basi ambaye yuko hivyo, hawezi kuabudiwa na mwenye akili. Ibrahim alimwambia baba yake:

﴿يَا أَبَتِ لَمْ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبَصِّرُ وَلَا يُغْنِي عَنْكَ شَيْئًا﴾

"Ewe baba yangu! Kwa nini unaabudu kisichosikia na kisichoona na kisichokufaa chochote"(19:42)

Bedui mmoja alikuwa na sanamu lake analoliabudu na kulitukuza. Siku moja alikwenda kulisujudia kama kawaida yake, Akaona kicheche karibu naye, Akadhani kuwa kicheche kimekuja kutabaruku.

Alipotaka kusujudia akaona kinyesi cha kicheche kwenye kichwa cha sanamu, akapata akili akalivunja sanamu huku akisema: "Kicheche kinamkojolea Mungu kichwani, akojolewaye na vicheche amekua duni."

Sema Enyi watu wa Kitab! Msipite kiasi katika dini yenu bila haki.

Msemo huu kwa dhahiri unaelekezwa kwa watu wa Kitab na kwa undani hasa unawakusanya watu wa dini zote. Upambanuzi asili wa Uislamu ni kwamba unayaweka madhara na manufaa mikononi mwa Mwenyezi Mungu peke yake, na unamweka binadamu mbele ya muumba wake bila ya kuweko mwingiliaji kati wa kiroho au wa kimaada. Mwenyezi Mungu anasema:

﴿مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَى بِهِ وَلَا يَجِدْ لَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا﴾

"Mwenye kutenda uovu atalipwa kwa uovu huo, Wala hatajipatia mlinzi wala msaidizi zaidi ya Mwenyezi Mungu" (4:123)

Wala msifuate matamanio ya watu waliokwishapotea tangu zamani; na wakawapoteza wengi, na wenyewe wakapotea njia iliyosawa. Makusudio ya watu ni viongozi wa dini ambao wanaifanyia biashara na kuipotoa vile wanavyo taka.

Kwanza: Mwenyezi Mungu Mtukufu amewasifu kuwa wao wenyewe ni wapotevu.

Pili: ni wapotezaji. Kisha akabainisha aina ya kupotea na upotevu kwamba ni kupotea kufuata njia iliyosawa. Njia iliyosawa ni kuwa katikati na kuacha kupita kiasi katika dini. Huu ndio Uislamu hasa, dini ya sawa sawa na njia iliyonyooka. Ili Waislam wasiseme kuhusu Muhammad (s.a.w.w), kama walivyosema wakristo kuhusu Masih ^(a.s), Mwenyezi Mungu alimwaamrisha Mtume wake awaambie waumini:

﴿قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَى إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمْ إِلَهٌ وَاحِدٌ فَقَنْ كَانَ يَرْجُو لِقَاءَ رَبِّهِ فَلَيَعْمَلْ عَمَلاً صَالِحًا وَلَا يُشْرِكُ بِعِبَادَةَ رَبِّهِ أَحَدًا﴾

"Sema hakika mimi ni mtu kama nyinyi tu. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu mmoja. Basi anayetarajia kukutana na Mola wake na afanye matendo mema, wala asimshirikishe yoyote katika ibada ya Mola wake." (18:110)

Mtu mmoja aliingia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, akawa anatetemeka kutokana na haiba ya Mtume. Mtume akampigapiga mabegani kwa upole na kumwambia: "Poa, Mimi ni mtoto wa mwanamke ambaye alikuwa akila mtanda huko Makka."

Walilaaniwa wale waliokufuru mionganoni mwa wana Waisrail kwa ulimi wa Daud na wa Isa mwana wa Maryam.

Wafasiri wanasema kuwa Daud aliwakataza Wana wa Israil kuvua samaki siku ya Jumamosi (Sabato), kwa wahyi wa Mwenyezi Mungu. Walipoasi amri yake aliwaalani na kuwaapiza wakawa manyani. Ama Isa alitakiwa na watu elfu tano (5000) awateremshie meza ya chakula kutoka mbinguni, wale, ndipo wamwamini. Walipoteremshiwa wakala na wasimwamini. Isa akasema: "**Ewe Mwenyezi Mungu walaani kama**

ulivywalaani watu wa Sabato (Jumamosi)," Lakini katika Aya hakuna kitu kinachoashiria ufanuzi huu.

Maana yaliyo dhahiri ni kuwa Daud na Isa waliwalaani waliokufuru katika Wana wa Israil Hayo ni kwa sababu waliasi na wakapituka mipaka. Na Mwenyezi Mungu (s.w.t) alinyamaza kueleza aina ya uasi na upitukaji mipaka, sio kwa ujinga au kusahau.

Nasi tunayanyamazia yale aliyoyanyamazia Mwenyezi Mungu. Wakati huo huo tukiamini kuwa laana ya Mwenyezi Mungu na nakama yake inamshukia kila mwenye kupetuka mpaka na kila anayemwasi, awe Mwisrail au kutoka uko wa Hashim.

Walikuwa hawakatazani mambo mabaya waliyokuwa wakiyafanya, Hakika ni maovu waliyokuwa wakiyafanya.

Aya hii inafahamisha kwamba mambo mabaya hayakuwa kwa watu fulani katika jamii ya Mayahudi, isipokuwa ilikuwa ni kazi ya watu wote na kwamba mambo maovu yalienea kwao mpaka yakawa ni mambo ya kawaida yaliyozoleka kwa wakubwa na wadogo. Kwa hiyo hakupatikana mionganoni mwao anayekataza mabaya na kuyapinga.

Katika Sahih Muslim na Bukhari kuna Hadith inayosema kuwa Mtume alisema: "**Mtawafuata waliokuwa kabla yenu vile vile wafanyakyo, hata wakiingia tundu ya kenge nanyi mtaingia**". Wakasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, ni mayahudi na wakristo?" Akasema: "Kumbe, ni nani tena."

Utawaona wengi katika wao wanawafanya marafiki na wale waliokufuru.

Dhamir ya katika wao inawarudia mayahudi, na ya wale waliokufuru hapa, ni washirikina wa kiarabu. Wengi katika mayahudi walikuwa marafiki pamoja na washirikina dhidi ya Mtume (**s.a.w.w**) na kuwachochea. Bali walikuwa ni maadui wakubwa wa Mtume, ingawaje Mtume alikuwa aki-aamini Mwenyezi Mungu na Utume wa Musa ^(a.s) na yale aliyoteremshiwa; na washirikina ni waabudu masanamu wasioamini Musa wala Kitabu chochote mionganoni mwa Vitab vyta Mwenyezi Mungu. Usawa kwa Mayahudi ni kuwa pamoja na waumini dhidi ya waabudu masanamu sio pamoja na waabudu masanamu dhidi ya waumini.

Lakini Mayahudi walikuwa na bado wako kwenye msingi ya faida na biashara, sio kwenye misingi ya dini. Mayahudi wa Madina walikuwa wanatawala biashara ya ndani na washirikina wa kiarabu walikuwa wakitawala biashara ya nje.

Mtume akafanya kazi ya ukombozi ya tawala hizo mbili, Hapo mayahudi na washirikina wakaungana na kuwa na mshikamano mmoja dhidi ya Waislamu; sawa na ilivyo leo walivyounsgana mayahudi na wenye mashirika ya unyonyaji mionganoni mwa wakiristo dhidi ya wazalendo na wanyonge, Yamelezo maelezo katika Sura hii Aya 51.

Kwa hakika ni mabaya waliyotanguliziwa na nafsi zao; ya kwamba Mwenyezi Mungu amewakasirikia, na watadumu katika adhabu.

Hii ni natija ya ujisadi wao na uadui wao. Na kila mtu atalipwa kutokana na aliyoyafanya awe Mwislamu au mshirikina.

Na lau wangelikuwa wanamwamini Mwenyezi Mungu na Nabii na yaliyoteremshwa kwake wasingeliwafanya hao kuwa marafiki.

Mwenyezi Mungu (s.w.t) ametaja katika Aya iliyotangulia kwamba mayahudi au wengi wao walikuwa wakifanya urafiki na washirikina, kisha akabainisha Mwenyezi Mungu (s.w.t), katika Aya hii kwamba hao mayahudi hawakumwamini Mwenyezi Mungu wala Musa wala yaliyoteremshwa katika Tawrat kama wanavyodai. Lau wangelikuwa wakweli katika madai yao, wasingeliwafanya washirikina kuwa marafiki badala ya Waislamu. Kwa sababu hilo ni haramu katika sharia ya Tawrat.

Lakini wengi katika wao ni mafasiki.

Kwamba maswala kwao sio maswala ya dini na itikadi, isipokuwa ni maswala ya masilahi na manufaa; kama tulivyotangulia kueleza.

MWISHO WA JUZUU YA TANO

12

SHARTI YA KUCHAPA

au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imam Husein ^(a.s)

Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini ^(a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

1

YALIYOMO

1	TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA KIMEANDIKWA NA: SHEIKH MUHAMMAD JAWAD
1	MUGHNIYYA
1	KIMETAFSIRIWA NA: SHEIKH HASAN MWALUPA
1	KIMEHARIRIWA NA: USTADH ABDALLAH MOHAMED
1.	KUPANGWA KATIKA KOMPYUTA NA: UKHT PILI RAJABU
1	UTANGULIZI WA MCHAPISHAJI
2	MAKOSA YA CHAPA
3	TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA
3	DHALIMU HAHESHIMIWI
3	MAANA
4	WANAAMINI BAADHI NA KUKANUSHA BAADHI
5	MAANA
5	WALISEMA TUONYESHE MWENYEZI MUNGU WAZIWAZI
5	LUGHA
6	MAANA
7	KUVUNJA KWAO AHADI
7	MAANA
10	DHULMA YA MAYAHUDI
11	IRABU
11	MAANA
13	TUMEKULETEAWAHYI
13	MAANA
14	JE MITUME WOTE NI WA MASHARIKI?
19	TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA
19	WALIKUFURU NA KUZUILIA
19	MAANA
20	MSIPETUKE MIPAKA KATIKA DINI YENU
20	MAANA
21	QUR'AN NA WANAOHUBIRI UTATU
24	IMEWAFIKIA HOJA KUTOKAKWA MOLA WENU
24	MAANA
26	MWENYEZI MUNGU ANAWAPA FATWA JUU YA MKIWA
26	MAANA
28	TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

KWA JINA LAALLAH MWINGI WA REHEMA MWENYE	
28	KUREHEMU TEKELEZENI MAPATANO
28	MAANA
30	MAPINDUZI NA KUPINGA MAPINDUZI
31	MMEHARAMISHIWA MFU
31	MAANA
33	KUKAMILISHWA DINI NA KUTIMIZWA NEEMA
35	NA MLICHOWAFUNZAWANYAMAWA MAWINDO
35	MAANA
36	UTWAHARAWAWATU WA KITABU
36	LUGHA
36	MAANA
40	TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA
40	UDHU NA TAYAMMAM
40	IRABU
40	MAANA
43	UADILIFU NDIO UNAOKURUBISHA KWENYE TAKUA
43	MAANA
45	KUMBUKENI NEEMA YA MWENYEZI MUNGU
45	MAANA
46	KUFANYAAGANO NAWAISRAIL
46	MAANA
49	IMEKWISHAWAFIKIA NURU
49	MAANA
50	UISLAMU NAWAPIGANIAAMANI
51	WALISEMA MWENYEZI MUNGU NI MASIH
51	MAANA
52	ASHAIRA NAWAKRISTO
55	TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA
55	MUSA NAWATU WAKE
55	MAANA
58	QABIL NA HABIL
58	MAANA
59	MMOJA NA WENGI
59	MAANA
61	TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA

61	MALIPO YA UFISADI
61	MAANA
63	TAFUTENI NJIA YA KUMFIKIA
63	MAANA
64	MWIZI MWANAMUME NAMWANAMKE IRABU
64	IRABU
64	MAANA
66	WASIKILIZAO SANA UWONGO
66	MAANA
69	USIWAOGOPE WATU
69	MAANA
71	TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA
71	MTU KWA MTU
71	MAANA
72	UKAFIRI, UFASIKI NA DHULUMA
74	KILA UMMA NA SHARIA YAKE
74	MAANA
77	NAHW
78	MAYAHUDI NAWAKRISTO MSIWAFANYE KUWA MARAFIKI
78	MAANA
79	PETROLI NA MAYAHUDI NAWAKRISTO WANYENYEKEVU KWA WAUMINI WENYE NGUVU KWA
81	MAKAFIRI
81	MAANA
84	TATIZO LA MAADILI
86	TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA
86	HUTOA ZAKAWAKIWAMERUKUI
86	MAANA
87	DINI YENU WAMEIFANYIA MZAHA NA MCHEZO
87	MAANA
90	AKAWAFANYA WENGINE MANYANI NA NGURUWE
90	MAANA
90	MAYAHUDI WALISEMAMKONO WAMWENYEZI MUNGU UME
92	FUMBA
92	LUGHA
92	MAANA
92	NJAMA ZA MAYAHUDI NA WANAZI

94	MAYAHUDI NA MOTO WA VITA
95	RIZIKI NA UFISADI
97	TAFSIRI YA QURANI AL-KAASHIF JUZUU YA SITA
97	FIKISHA ULIYOTEREMSHIWA
97	MAANA
98	MWENYE AL-MANAR NAAHLUBAYT
99	KUSIMAMISHA TAURAT NA INJIL
99	MAANA
100	AGANO LAWANAWA ISRAIL
100	MAANA
101	MWITO WA MASIH KWAWANAWA ISRAIL
102	MAANA
104	HAWAWEZI KUWADHURU WALA KUWANUFAISHA
104	NAHW
104	MAANA
107	MWISHO WA JUZUU YA TANO
107	SHARTI YA KUCHAPA